Alhamisi Julai 11, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579967

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Baba matatani tuhuma za kubaka, kulawiti mwanawe

UKURASA 3




UKURASA 13

# Kicheko mabasi kusafiri usiku



• **Taboa** yatoa ya moyoni, wasafiri nao wafurahia , polisi yawatoa hofu abiria kuhusu usalama...*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**MATATANI TUHUMA ZA KUTAKA KUMTAPELI DC**
TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoa wa...

UKURASA WA 4
**MAPYA YAIBULIWA KESI YA KIGOGO TAKUKURU**
SHAHIDI wa 20 katika kesi ya kutakatisha fedha inayomkabili Mhasibu...

UKURASA WA 4
**DED AKALIA KUTI KAVU**
KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ameelezea..


## Kibano NGO usajili mpya

UKURASA 3



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipeana mkono na Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Abdel Fatah Al Sisi, katika Ikulu ya Rais, mjini Cairo jana. **PICHA OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Kiama chaja benki kandamizi wakopaji

UKURASA 2




**MICHEZO** YANGA KUSHUSHA MASHINE MPYA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kicheko mabasi kusafiri usiku

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), kilielezea kufurahishwa na hatua ya serikali kusikia kilio chao cha miaka mitatu na kuruhusu mabasi kusafiri kwa saa 24.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Katibu Mkuu wa Taboa, Enea Mrutu, alisema uamuzi huo unakwenda kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya uchunguzi.

"Tunampongeza sana Waziri (wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola), kwa kuwa tumekuwa na maombi ya muda mrefu sana lakini sasa ametusikiliza na sasa usafiri unakwenda kuanza kwenye njia mbili. Ameonyesha ni waziri anayesikiliza watu na kujali kile tulichokililia muda mrefu," alisema.

Hata hivyo, alisema ni vyema serikali ikashirikiana na wamiliki kuwadhibiti madereva wa mabasi na malori ambao wanatumia vilevi na kuendesha magari.

"Tungependekeza kwenye mizani kuwe na vifaa vya kupima vilevi kwa madereva wote kwa kuwa dereva wa basi anaweza kuwa hajanywa lakini wa lori akawa amelewa. Hii itasaidia kuwadhibiti ingawa nasi tunawaelimisha madereva wetu kuwa makini na kuacha kutumia vilevi," alibainisha.

Kwa mujibu wa Mrutu, kuna mambo yamebaki ambayo ni kurundikwa kwa muda mrefu kwa faini za madereva na kuwa mzigo kwa wamiliki pamoja na kuwapo kwa vituo vingi vya ukaguzi.

"Mfano dereva anakaguliwa Kibaha, Chalinze na Morogoro na analazimishwa kuingia kwenye vituo vya mabasi na kulipa ushuru wakati hapakii wala kushusha abiria kwenye maeneo hayo. Tunaomba watuondolee kero hii," alisema.

Pia aliwataka wamiliki wa mabasi kuhakikisha wanakuwa na madereva wawili kwa kila basi ili kuhakikisha wanapokezana na kusafiri kwa umakini zaidi na kwamba wanaongea na madereva wao kuwa makini kwa kuwa usiku kuna malori mengi yanayosafiri.

Mrutu alisema suala la ving'amuzi kwenye mabasi ni jambo jema kwa kuwa wamiliki wanalala kwa utulivu na wanafuatilia kwenye mtandao kuona mwendo wa mabasi yao kwa kuwa hawaruhusiwi kutembea zaidi kilomita 80 kwa saa.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, alitangaza kuanza kwa safari za mabasi kwa saa 24

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akijadiliana jambo na mmoja wa wadau wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, baada ya ufunguzi wa uhuishaji usajili wa mashirika hayo jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 3. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matatani tuhuma za kutaka kumtapeli DC

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dar es Salaam, inamshikilia Omary Chuma (55), mkazi wa Chamazi wilayani Temeke, kwa tuhuma za kujifanya Ofisa Usalama wa Taifa Ikulu, kwa lengo la kutaka kumtapeli Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo.

Kaimu Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Takukuru, Ally Mfuru, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Julai 2, mwaka huu, baada ya Takukuru kupokea taarifa ya kutaka kumtepeli mkuu huyo wa wilaya.

Alisema mtuhumiwa huyo alitenda makosa yaliyo chini ya sheria ya namba 11 ya mwaka 2007 kwa kosa la kujifanya Ofisa wa Serikali kinyume cha kifungu namba 100 (b) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyorekebishwa mwaka 2002.

Alisema kosa lingine ni kuomba au kushawishi au kujaribu kujipatia au kujipatia rushwa kinyume cha kifungu 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Mfuru alisema ni wiki tatu zimepita tangu Takukuru itangaze kukamata watu sita wakiwamo wanne waliojifanya maofisa wa Takukuru na maofisa wa vyombo vingine na dola na wawili kutoka kampuni za simu.

Alisema matapeli hao wana mtandao unaojusisha maofisa mbalimbali wa Serikali ambao wanafuatilia watumishi au viongozi ambao kwa namna moja nyingine wanaweza kuwa na tuhuma, hivyo kuwadai fedha au rushwa huku wakijidai wao ni maofisa wa Takukuru au Usalama wa Taifa.

"Kwa mara nyingine tena tunatoa wito kwa matapeli wanaofanya vitendo hivi kuacha mara moja kwa sababu Takukuru ipo macho na ina mamlaka kisheria kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika na utapeli," alisema.

"Mtuhumiwa huyu alitenda makosa hayo katika wilaya ya Kisarawe atafikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya hiyo leo (jana) Julai 10 kwa ajili ya kujibu tuhuma zinazomkabili," alisema.

# Kiama chaja kwa benki zinazoumiza wakopaji

**Na Elizabeth Zaya**

KIBANO kinakuja kwa benki ambazo zimekuwa zikitengeneza mikataba na masharti ya mikopo, kwa lengo la kuumiza wakopaji kwa kuwawekea masharti magumu ambayo hawawezi kuyatekeleza.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imesema kwamba lengo la benki hizo kuandaa mikataba na masharti magumu kwa wakopaji ni kupiga mnada mali zao pale wanaposhindwa kulipa kwa wakati mikopo wanayokopa.

Akizungumza na Nipashe katika banda la BoT katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika viwanja vya Sabasaba, Ofisa wa Dawati la Malalamiko ya wateja wa huduma za Kibenki wa BoT, Ramadhani Myonga, alisema kibano hicho kitaanza hivi karibuni, baada ya kumalizika kwa uandaaji wa kanuni za sheria ndogo za fedha ya mwaka 2018 na kuanza kutumika.

Myonga alisema wamebaini kwamba benki nyingi zimekuwa zikiweka masharti magumu ambayo siyo rafiki kwa wakopaji ambayo pia hayampi ahueni mkopaji kumuongeza muda mkopaji huyo kulipa mkopo wake pale anapopata mtikisiko kiuchumi.

"Kwa mfano, unaweza kukuta mteja anayekopa anaambiwa atarejesha kiasi fulani cha fedha kumbe wakati huo huo rejesho lake halijajumuishwa na fidia ya mkopo wa mwezi... mteja anapaswa ajue hata na sehemu ya marejesho, lakini hata zile document (nyaraka) za mikopo yao huwa hata hawapewi," alisema Myonga.

Alisema sehemu nyingine ya matatizo ya mikopo ni pale mteja anapotaka kuhama kutoka benki moja kwenda nyingine, kwa ajili ya kutafuta ahueni ya mkopo wake.

"Kwa hiyo huwa inafika mahali mkopaji akitaka kuhamia katika benki nyingine kwa ajili ya kutafuta ahueni ya mkopo wake, benki husika ambayo amekopa humuwekea masharti magumu ilimradi tu ashindwe, na mwisho wa siku ndiyo kutengeneza mazingira ya kukimbilia kupiga mnada mali zake," alisema Myonga.

"Mabenki mengi hayatoi fursa kwa wakopaji kurestructure mikopo yao baada ya kuyumba kiuchumi, badala yake yanakimbilia kupiga mnada mali na hiyo pia inachangia na namna ambavyo mikataba imeandikwa, haitoi fursa hiyo."

Alisema tatizo jingine linalochangia migogoro ya mikopo ni wakopaji wenyewe kukimbilia kusaini mikataba ya mikopo yao bila kusoma vilivyoandikwa katika mikataba hiyo, hivyo mwisho wa siku kujikuta wanaingia katika matatizo hususan wanapobaini kwamba walichokisaini hawawezi kukitekeleza.

"Tatizo wakopaji wengi huwa wanakimbilia kusaini kitu ambacho hawakijui, wakikimbilia kupatiwa pesa harakaharaka bila kusoma kilichoandikwa kwa hiyo baadae inawaletea matatizo," alisema Myonga.

Tatizo jingine ambalo alisema linachangia migogoro ya mikopo katika benki nyingi ni lugha inayotumika katika kuandika mikataba ya mikopo, kutokuwa na elimu ya mikopo kwa wakopaji na maandishi madogo yanayoandikwa katika mikataba hiyo.

"Kwa hiyo BoT imetengeneza sheria mpya ya 2018 ambayo inasubiri kanuni ambazo wakati wowote zitakamilika na kuanza kufanya kazi, hizi zitakuwa suluhisho la kumlinda mteja na huduma za kibenki," alisema Myonga.

Alisema pia itatoa fursa kwa mkopaji kuwa na nafasi ya kujiridhisha na kile kilichoandikwa kwenye mkataba wa mkopo kwa muda wa saa 24 hadi siku tatu na kufanya uamuzi wa kukubali au kukataa

"Pia kutakuwa na mfumo wa kurestructure mkopo kwa ajili ya kumsaidia mkopaji anapopata mtikisiko wa kiuchumi," alisema.

Pia alisema sheria hiyo itatoa fursa kwa BoT kutembelea taasisi za fedha kuangalia au kukagua na kujiridhisha kama zinatekeleza kanuni za kuwalinda wateja na muongozo wa BoT.

Kwa takribani miaka mitatu kumekuwapo na kasi kubwa ya wateja wengi wa benki kujikuta katika wakati mgumu kiuchumi, hivyo benki walizokopa kuuza kwa mnada mali zao zikiwamo nyumba, magari, mashamba na viwanja.

## HABARI KITAIFA

# Chadema kupinga uchaguzi mdogo jimbo la Tundu Lissu

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema kinajiandaa kwenda mahakamani, kupinga uchaguzi mdogo katika Jimbo la Singida Mashariki, uliotangazwa kufanyika Julai 30, mwaka huu na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, aliiambia Nipashe kwa njia ya simu jana kuwa wako katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kufungua kesi hiyo.

Alisema chama hicho hakiwezi kushiriki uchaguzi huo ambao ameuita ni batili kwa sababu sheria na taratibu hazikufuatwa za kumvua ubunge Tundu Lissu ambaye kwa sasa yuko nje ya nchi kwa matibabu.

"Tupo katika hatua nzuri kabisa za mchakato wa kufungua kesi mahakamani kupinga uamuzi wa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kumvua ubunge Tundu Lissu, ilhali yuko nje ya nchi akipatiwa matibabu. Lakini pia kesi hii inahusisha masuala ya kusafiri nje ya nchi na hali ya ugonjwa," alisema Makene.

"Kesi hii inahusu masuala ya kusafiri nje ya nchi lakini pia afya ya ugonjwa wa mtu hivyo lazima tuwe na 'document' (taarifa) kamali. Lengo letu ni kuwahi kuzuia uchaguzi kufanyika," aliongeza.

Makene alisema wanashangazwa na NEC kutangaza kufanya kampeni zinazoanza Julai 19 hadi Julai 30, kwa siku 12 ambazo alidai hata uchaguzi wa kiongozi wa kitongoji hawatumii siku chache kiasi hicho.

"Lengo letu ni kutaka kwenda mahakamani kuzui huu uchaguzi ambao ni haramu na Chadema hatuwezi kushiriki, ina maana tukisimamisha mgombea tutakuwa tunahalalisha haramu. Uchaguzi gani ambao kampeni zinafanyika kwa siku 12?" Alihoji.

INAENDELEA UK. 26




Makamu Waziri wa Kilimo na Ubora wa Chakula wa Uholanzi, Marjolijn Sonnema (kushoto), akipeana mkono na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega (kulia), baada ya kuweka saini randama ya makubaliano kukuza sekta ya uvuvi na ufugaji wa kuku nchini. Makubaliano hayo yalifanyika jana jijini Arusha. Wa pili kushoto ni Balozi wa Uholanzi nchini, Joroen Verheul na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Methew Mtigumwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba mbaroni madai kubaka, kulawiti mwanawe wa kumzaa

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MKAZI wa kitongoji cha Kimangakene, Kijiji cha Diyovuva wilayani Morogoro, Saidi Kasti (35), anashikiliwa polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kumbaka na kumlawiti mtoto wake wa kike wa kumzaa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo.

Alisema jeshi la polisi linaendelea kufanya uchunguzi wa tukio hilo licha ya kwamba taarifa za awali zinadai kuwa mtuhumiwa alifanya kitendo hicho kutokana na imani za kishirikina ili kupata utajiri kupitia shughuli zake anazofanya.

Mama wa mtoto huyo, Himaya Waziri, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Julai 7, mwaka huu, majira ya saa 7:00 usiku baada ya baba huyo kwenda kulala na watoto wake katika chumba kingine kuanzia julai 6 licha ya yeye kumzuia.

Alisema alisikia mwanawe huyo aliyebakwa akilia na ndipo alipokwenda kumbembeleza na hatimaye alilazimika kumchukua na kwenda kulala naye chumba alicholala kwa sababu mtoto alikuwa hanyamazi.

Mama huyo mwenye watoto watatu alisema anashangazwa na mumewe huyo kumtendea mtoto wao kitendo hicho cha kinyama licha ya kwamba alishamkataza kwenda kulala na watoto na yeye kudai kuwa ni watoto wake asiwe na wasiwasi, akakubali bila kujua nini kitatokea.

Himaya alisema baada ya kujifungua mtoto wa tatu waliamua kulala vitanda tofauti kwenye chumba kimoja huku yeye akiwa na watoto wawili kitandani na yeye akiwa na mtoto mchanga.

Hata hivyo, alisema Julai 6, aliamua kwenda kulala na watoto katika chumba kingine ambacho alikuwa analala mtoto wake mkubwa aliyeko safarini Dar es Salaam.

"Ilipofika usiku wa saa 7:00 nikaskia sauti kali ya mtoto analia

INAENDELEA UK. 8

# NGO zapewa miezi 2 kukamilisha usajili

**Salome Kitomari na Enock Charles**

SERIKALI imewataka wadau wa mashirika yasiyo ya kiserikali kukamilisha usajili chini ya Sheria mpya ya mashirika yasiyo ya kiserikali ndani ya miezi miwili tangu kupitishwa kwa marekebisho ya sheria hiyo.

Maelekezo hayo yametolewa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile kuhusu utekelezaji wa sheria hiyo Na 3 ya mwaka 2019.

Akizungumza katika mkutano maalum na wadau hao jijini Dar es Salaam jana, Dk. Ndugulile alisema lengo la Serikali ni kuboresha usimamizi wa asasi zisizo za kiserikali ili ziweze kuleta tija na maendeleo katika Taifa.

"Tunataka kuwe na uelewa wa pamoja wa mabadiliko ya sheria ambayo yamepelekea kuwa na utaratibu mpya wa usajili kwa sababu usajili wa NGO (Asasi) kwa siku za nyuma ulikuwa na taasisi nne... kuna watu walikuwa wanasajili Brela, wengine Rita, Wizara ya Mambo ya Ndani na wengine walikuwa wanasajili ndani ya Wizara ya Afya," Dk. Ndugulile alisema.

Alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakitoa mchango mkubwa nchini na yamekuwa yakifanya mambo mengi mazuri yenye taadhira katika utekelezaji wa mambo mbalimbali kama vile kutoa huduma za kijamii za elimu, afya, mavazi,chakula na malazi kwa wasiojiweza, utetezi wa makundi maalum na

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
10/07/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI tarehe 13/07/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha mizigo kutoka **INYONGA** kuelekea **DAR ES SALAAM kupitia TABORA-DODOMA** Magari yenye namba za usajili,

   **1. T550 BES/474 BCJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu – mita 16
   Upana - mita 2.8
   Kimo – mita 4.8

3. Njia itakayotumika **INYONGA hadi DAR ES SALAAM kupitia TABORA-DODOMA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00Jioni).**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

11517202



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
10/07/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMANNE tarehe 16/7/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha mizigo kutoka SUMBAWANGA kuelekea **KAMBANGA** kupitia **MPANDA.** Magari yenye namba za usajili,

   **1. T349 BNT/646 BCJ**
   **2. T246 DAJ/T365 CTD**
   **3. T389 BES/T668 BCJ**
   **4. T244 DAJ/995 CLX**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   **Urefu – mita 20.00**
   **Upana – mita 3.0**
   **Kimo – mita 4.8m**

3. Njia itakayotumika **SUMBAWANGA hadi KAMBANGWA** kupitia **MPANDA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00Jioni).**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

11517202

# Bil. 3.5/- kununua chopa mpya polisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi Tanzania linatarajia kutumia Sh. bilioni 3.5 kununua helikopta kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama nchini.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, alisema hayo jana alipokuwa mkoani Shinyanga katika ziara ya kukagua ujenzi wa nyumba 10 za makazi ya askari polisi ambazo zimeshakamilika na kugharimu Sh. milioni 225.

Alisema tangu mwaka 1975 Jeshi la Polisi halijawahi kununua ndege aina ya helikopta na kwamba zilizopo ni za zamani, hivyo liatarajia kununua nyingine mpya ambayo itasaidia kuimarisha ulinzi na usalama na kuendelea kulinda amani nchini.

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, akibeba tofali kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Ibwagulilo, ikiwa ni kuwahamasisha wananchi wa Kijiji cha Namalebe, Kata ya Chitengule, Jimbo la Mwibara, wilayani Bunda Mkoa wa Mara, kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo mpya. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Utendaji kazi DED wamchefua Bashiru

**Mary Mosha na Paul William,** KILIMANJARO

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ameelezea kutoridhishwa na utendaji kazi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Magreth John.

Kutokana na hali hiyo, amemtaka kwenda katika halmashauri zingine za mkoa huo zinazoongozwa na wanawake wenzake kujifunza wanavyofanya kazi.

Dk. Bashiru alitoa kauli hiyo jana wilayani Same akihitimisha ziara yake ya siku nne mkoani Kilimanjaro yenye lengo la kuimarisha chama na kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Alisema kuwa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli imeonyesha kuwajali wanawake kwa kuwapa nafasi za uongozi na miongoni mwao wamefanikiwa kwa vitendo katika kutekeleza majukumu yao.

"Lakini kwa wilaya ya Rombo sijaridhishwa na utendaji kazi wa , kurugenzi wa halmashauri hiyo na aende kujifunza kwa wakurugenzi wenzake wanawake," alisema.

"Wanawake wameonyesha wakipewa nafasi wanaweza kuzitendea haki na hii ni kwa sababu wana huruma, upendo na wako karibu na wananchi ambao ndio wanaowaongoza. Niwapongeze sana lakini kwa Mkurugenzi wa Rombo sijaridhishwa na utendaji kazi wake," aliongeza.

Katibu mkuu huyo pia aliwataka viongozi wa Same kutobweteka kwa kuwa wana safari ndefu ya kuwaboreshea wananchi maendeleo na kutatua kero zinazowakabili.

Pia alisema wako wananchi ambao wamekuwa wakifanyishwa kazi na baadhi ya watu walio nacho ambapo huwalipa ujira mdogo wakati huo huo hawapewi mikataba ya ajira na kuwataka wateuliwa wa Rais kuliangalia suala hilo kwa mapana ili wananchi wapate haki ya jasho lao.

Alisema wako watu wameanza kutikisa misingi ya ulinzi na usalama wa nchi kwa kutoa matamko ya kichochezi na kuwataka kuacha tabia hizo na kuacha kuchezea amani ya nchi.

Alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kutenda kazi zao kwa haki huku akiliagiza jeshi la polisi kuacha tabia ya kuwabambikia watu kesi pamoja na tabia za kuwanyima dhamana wakati ni haki yao.

Aidha aliwataka kutofuatilia na kuziamini taarifa zinazoandikwa katika mitandao ya kijamii kwani wakati mwingine hazina ukweli na lengo za kusambazwa ni kuvurunga amani ya nchi.




# Shahidi adai kupokea fedha za uuzaji kiwanja kwa Gugai

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa 20 katika kesi ya kutakatisha fedha inayomkabili Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai, amedai mahakamani kuwa alipokea Sh. milioni 80 na si 60 kama zilivyoandikwa kwenye mkataba wa mauziano.

Kadhalika, shahidi huyo, Abubakar Hamisi (46), amedai kuwa mkataba huo ulikuwa wa mauziano ya kiwanja kilichoko Boko Uninio, Dar es Salaam na kwamba anamfahamu Gugai kwa sababu ni jirani yake.

Ushahidi huo ulisikilizwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Awamu Mbwagwa.

Shahidi alidai kuwa anamfahamu Gugai kwa sababu ni jirani yake na pia aliwahi kufanya naye biashara.

"Tulifanya makubaliano kati ya familia yetu na ile ya Gugai ya kuuziana kiwanja namba 64 block C kilichoko Boko Ununio kwa Sh. milioni 80 na si milioni 60 zilizoandikwa kwenye mkataba wa mauziano," alidai.

"Familia zote mbili zilifanya makubaliano, Gugai alimwita mwanasheria wake alikwenda kuandaa mkataba. Jioni tulikwenda nyumbani kwake, tulipousoma tuliufiki tukalipwa fedha." alidai Abubakar.

Aliendelea kudai kuwa mauziano hayo yaliyofanyika nyumbani kwake akiwa na mwanasheria, uliandikwa hivyo ili kupata nafuu ya kodi.

Shahidi huyo aliiomba mahakama kupokea mkataba huo wa mauziano ya kiwanja kama kielelezo baada ya kuutambua kwa majina na saini.

Upande wa utetezi ukiongozwa na wakili Semi Malimi, ulipinga kupokewa kwa mkataba huo akiadai ni nakala na si halisi.

INAENDELEA UK. 8

# Serikali yatafuta mkopo nafuu kununua magari Zimamoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI ipo kwenye mazungumzo na nchi mbalimbali kwa ajili ya kupata mkopo nafuu wa kununua magari na vifaa vingine vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kukabiliana na majanga ya moto nchini.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Kamishna wa Utawala na Fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini, Mbaraka Semwanza, wakati akifungua kikao cha ndani cha kiutendaji, ikiwamo kutoa maelekezo kwa maofisa, askari na watumishi raia wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Alisema serikali inajua umuhimu wa jeshi hilo hapa nchini, ndiyo maana inafanya mazungumzo ili kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana kwa ajili ya kusaidia katika majanga mbalimbali ya moto yanayotokea.

"Serikali inatambua kazi inazofanya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, tunajitahidi kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana kusaidia utendaji kazi kwa urahisi zaidi," alisema Semwanza.

Alisema upande wa changamoto wa sare za jeshi hilo, tayari mkataba umeshasainiwa na zinaendelea kushonwa ili ziweze kutumiwa na jeshi hilo.

"Sare tayari zimeanza kushonwa naimani changamoto kwa upande huo muda si mrefu itakuwa imekwishwa," alisema Kamishna Semwanza.

Alilitaka jeshi hilo kufanya kazi kwa bidii ikiwamo kutoa ushirikiano kwa wananchi pale wanapohitajika katika matukio mbalimbali ya majanga ya moto yanapotokea. Alisema pamoja na serikali kujikita katika miradi mikubwa ya ujenzi wa nchi, wana imani italiangalia jeshi hilo kwa asilimia zote kutokana na umuhimu wa kazi ambazo wanafanya.

Akizungumzia kutokuwapo kwa vituo vya zimamoto na uokoaji katika baadhi ya wilaya, alisema tayari halmashauri zimeshawasiliana na jeshi hilo kwa ajili ya kutoa maeneo na kuongeza kuwa hivi sasa wapo katika hatua mbalimbali za kulipa fidia kwa wananchi ambao wanatakiwakupisha maeneo kwa ajili ya ujenzi.

# Muhimbili yampa msaada mashine ya kupumua mgonjwa

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila, imetoa msaada wa mashine ya kusaidia kupumua (Oxygen Concentrator) kwa Hamad Awadhi kutokana na matatizo yake ya afya ambayo yanamlazimu kutumia mashine ya oxygen muda wote ili aweze kupumua.

Akikabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Charles Majinge, amesema hospitali imempatia msaada huo kwa lengo la kuokoa maisha yake na kuimarisha afya yake.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, ameeleza kwamba mashine hiyo inathamani ya Sh. milioni 3.5 imenunuliwa na Hospitali ya Mloganzila.

Alisema mgonjwa huyo amelazwa hospitalini hapo kwa mwaka mzima kwa ajili ya kupatiwa matibabu hayo, hivyo kwa sasa tayari wamempatia mafunzo mgonjwa huyo namna ya kuitumia na kuitunza ipasavyo. Prof. Museru amemtaka Awadhi kuitunza na kuitumia vema mashine hiyo kama ambavyo ameelekezwa na wataalamu ili afya yake itakapoimarika iweze kusaidia Watanzania wengine.

"Hospitali imekupatia msaada wa mashine hii ya kukusaidia kupumua kwa lengo la kuhakikisha afya yako inaimarika zaidi hivyo tunaomba uitunze na utakapopona kabisa utairejesha hospitali ili tuwasaidie wengine," alisema Prof. Museru. Naye Daktari Bingwa wa magonjwa ya ndani MNH-Mloganzila, Dk. Patricia Munseri, alisema Awadhi kwa muda wote aliokuwapo hospitalini ameishi kwa kutegemea mashine ya oxygen ambayo inamsaidia kupumua na kwa siku alikuwa akitumia gesi wastani wa lita 5,760.

Awadhi alifikishwa Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila Julai 9, 2018 na kuruhusiwa Julai 9, mwaka huu baada ya afya yake kuimarika.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa tatu kulia), Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili na Usalama wa Chakula wa Uholanzi, Marjolyn Sonnema (katikati), pamoja na Dk. Edmond Matafu wakikata utepe ikiwa ni ishara ya kuzindua maabara ya kutembea ya upimaji udongo mjini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wafugaji samaki, kuku wakumbukwa

**Na Novatus Makunga,**

ARUSHA

UHOLANZI imekubali kuwajengea uwezo wafugaji wadogo wa samaki ili kuongeza uzalishaji katika mabwawa kwa kufikisha kiasi cha mahitaji ambacho ni zaidi ya tani 700,000 kwa mwaka.

Serikali za Tanzania na Uholanzi zilitiliana saini makubaliano ya awali hayo ya miaka mitano jijini hapa jana.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa makubaliano hayo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema hatua hiyo ni kubwa ambayo itasaidia kupunguza pengo la mahitaji ya samaki. Kwa sasa uzalishaji samaki katika mabwawa ni tani 350,000 kwa mwaka.

"Fursa ya kujenga mabwa ya samaki nchini kwetu bado kubwa sana na ya kutosha na mahitaji ni makubwa ya kitoweo cha samaki," alisema.

Ulega alisema kutokana na pengo lililopo la uzalishaji wa samaki na mahitaji, soko la ndani bado liko la kutosha pia kwa nchi za eneo la Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Licha ya ufugaji wa samaki, pia Ulega alisema wameingia makubaliano katika kuinua na kuboresha sekta ndogo ya kuku katika kipindi kama hicho cha miaka mitano.

Alisema katika makubaliano hayo, Uholanzi itasaidia kuwajengea uwezo Watanzania katika ufugaji wa samaki na wa kuku.

Ulega alisema ufugaji wa kuku ni shughuli ambayo anaweza kufanya Mtanzania yeyote na akasisitiza makubaliano hayo ya kuwajengea uwezo wafugaji wadogo, yamelenga kuwaingiza katika ufugaji wa kibiashara.

"Huu ni mwelekeo wa serikali yetu ya awamu ya nne ya viwanda. Uzuri wa sasa tumeshaingia katika nchi ya uchumi wa kati kwa hiyo mikakati hii imekuja wakati mwafaka," alisema.

Naibu waziri pia alisema kuwa sasa inatakiwa Watanzania kuondokana na mazoea ya kuchukulia kitoweo cha kuku kama anasa na badala yake kiwe cha kawaida kwa kila familia kukitumia kinapohitajika kwa bei ya kawaida ambayo kila mtu anaimudu.

Naye Naibu Waziri wa Maliasili na Chakula wa Uholanzi, Mojolijn Sonema, alisema serikali yake imelenga katika kuwawezesha Watanzania kuzalisha kuku na samaki wa kutosha lakini walio bora na salama kwa afya.

"Lengo kuu la makubaliano haya ni kujenga uwezo kwa wafugaji wadogo wa samaki na kuku ambao tunaamini ndio nguzo ya uchumi inayofika mpaka chini kabisa katika jamii," alisema Sonema.

Sonema alifafanua kwamba huu ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya serikali ya Tanzania na Uholanzi uliodumu kwa zaidi ya miaka 40.

Alisema kwa sasa serikali ya Uholanzi haitoi tena misaada ya fedha kwa Tanzania bali inawajengea uwezo wajasiriamali, wakulima na wafugaji utakaowawezesha kuongeza uzalishaji na kuinua uchumi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pongezi serikali kulinda wakopaji

**MOJA** ya mbinu chafu zilizokuwa zinatumiwa na benki kukwamisha wateja kukopa au kukandamiza wateja wanaochukua mikopo inatajwa kuwa ni kuandaa mikataba yenye masharti magumu.

Masharti hayo yalikuwa yanawabana wanaokopa na wanaoshindwa kulipa mikopo na kufanikisha kuuzwa mali zao hasa ardhi na nyumba walizoweka rehani.

Watu wameshuhudia familia zikitimuliwa kwenye nyumba kwa kudaiwa shilingi milioni chache kati ya mamilioni waliyokopa.

Japo inaweza kuwa vigumu kuthibitisha kuna wakati hata matapeli wa mikopo walidaiwa kutapeli hati miliki za watu na kuzitumia kukopa fedha ambazo baadaye hawakuzilipa na hati hizo zikatumiwa kunadi mali zao na kuwatia umaskini.

Hatuwezi kusema kulikuwa na watu waliokuwa wanakopa kwa lengo la kupata mali za wenzao kama ardhi na nyumbani kwa sababu hatuna ushahidi, lakini tunaamini lisemwalo lipo na kama halipo laja ndiyo maana sasa serikali imefungua macho.

Habari njema ni kwamba Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetoa onyo kwa benki zilizokuwa zikitengeneza mikataba na masharti ya mikopo, kwa lengo la kuumiza wateja kwa kuwawekea masharti magumu ambayo wasingeweza kuyatekeleza hivyo kushindwa kulipa madeni.

BoT inaonya kuwa pengine lengo la benki hizo lilikuwa ni kuandaa mikataba na masharti magumu kwa wakopaji ili kupiga mnada mali zao wanaposhindwa kulipa mikopo hiyo kwa wakati.

BoT inaeleza kuwa wahusika wataanza kuchukuliwa hatua wakati wowote hivi karibuni, baada ya kukamilisha kuandaa kanuni za sheria ndogo za fedha, ambazo zimeanza kutumiwa.

Benki Kuu imeeleza kuwa imebaini kwamba benki nyingi zimekuwa zikiweka masharti magumu ambayo siyo rafiki kwa wakopaji ambayo pia hawampi ahueni na kuongeza muda wa mteja kulipa mkopo wake pale anapopata mtikisiko kiuchumi.

Tunaipongeza serikali kwa kuliona hilo na kuwabana wahusika kwa kuwa baadhi wanakuwa na nia pamoja na mbinu ovu za kuwadhulumu watu waliokuwa na mikakati ya kujiondolea umaskini.

Migogoro ya mikopo imekuwa ni chanzo cha mali za familia kuuzwa na kuongeza umaskini. Watoto na wahitaji kukosa makazi, lakini wanaosoma kukwamishwa kitaaluma na kuishia katika mazingira magumu.

Tunaipongeza BoT kwa kuliona hilo na tunashauri kama inawezekana kufuatilia malalamiko ya wateja waliopoteza mali zao kitatanishi.

Pamoja na hayo tunawashauri pia wateja kusoma na kutafuta ushauri wa wataalamu ili kufahamu kwa kina masuala yote yanayohusiana na mikopo kuanzia riba, rejesho kila mwezi, jinsi ya kupata msaada endapo watapatikana na matatizo kwenye uchumi unaotishia mali walizoweka rehani.


BoT inagusia suala la lugha za kisheria na kibiashara zinazotumiwa wakati wa kuandika mikataba ya mikopo. Wengi hawafahamu lugha za kisheria wala za kitaalamu ndiyo maana wanakandamizwa, ndiyo maana wanatakiwa kutafuta wataalamu ikibidi hata kuwasiliana na BoT.

Tunaishukuru serikali kwa hatua hiyo na tunachoweza kusema ni asante BoT kuwadhibiti wanaowakandamiza wakopaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kampeni ya 'nyumba ni choo' iibadilishe jamii

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya vitu ambavyo vinaelekezwa na wataalamu wa afya ili kuepuka ugonjwa wa kipindupindu ni kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara, hasa baada ya kutumia choo na kabla ya kushika chakula. Aidha, inasisitiza kusafisha matunda kikamilifu kabla ya kula na pia kula vyakula vyenye moto.

Wataalamu wa afya wanasema kipindupindu ni ugonjwa hatari unaosababishwa na bakteria aitwaye "vibriocholerae" na huathiri hasa utumbo mwembamba na husababisha kuhara na kutapika sana pamoja na homa kali.

Kwamba kwa kawaida hupatikana katika chakula au maji machafu na kinyesi kibichi cha mgonjwa. Kadhalika wanahimiza matumizi ya vyoo wakati wote na kutumia majisafi na salama yaliyochemshwa.

Jamii inahimizwa kutumia maji yaliyochanganywa na kemikali ya kuua wadudu, au maji ya chupa kwa kunywa na pia kwa kunawa wakati wa kuandaa chakula, vinywaji, kusafisha meno, kunawa uso, mikono, vyombo, matunda na mboga. Kwa kuzingatia njia sahihi za usafi, kuna uwezekano mkubwa kwa jamii kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu ambacho kimekuwa kikiibuka mara kwa mara na kupoteza maisha ya watu.

Ili kukabiliana na ugonjwa huo nchini, zimekuwa zikifanyika kampeni mbalimbali zikiwamo za 'Nyumba ni Choo' zinazoratibiwa na serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kampeni hiyo ambayo kwa sasa ipo jijini Mwanza, inalenga kuhamasisha ujenzi na matumizi ya vyoo bora ambavyo vitasaidia jamii kuepuka ugonjwa huo hatari ambao chanzo chake ni uchafu.

Wakazi wa Mwanza wameshaelekezwa kwamba kufikia Septemba 30, 2019 kila kaya katika halmashauri zote iwe na choo bora kwa ajili ya kuondokana na magonjwa ya mlipuko yanayogharimu fedha nyingi kwa ajili ya matibabu.

Mkuu wa mkoa wa huo, John Mongella ndiye mwenye agizo hilo, na kwamba takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya kaya 600,000 hazina vyoo kabisa mkoani Mwanza, huku kaya zenye vyoo bora zikiwa ni asilimia 61, na pia kaya zenye vyoo ingawa si bora zikiwa ni asilimia 39.

Inawezekana hali kama hiyo isiwe Mwanza tu bali nchi nzima, hivyo kuna haja ya kuendelea kuhamasisha jamii kujenga na kutumia vyoo bora kupitia kampeni hiyo kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko.

Imekuwa ikidaiwa kuwa kuna baadhi ya makabila ambayo yanakumbatia mila zilizopitwa na wakati za kutotumia vyoo kwa kile kinachodaiwa kuwa ni laana katika familia kutumia choo badala yake kujisaidia vichakani.

Pamoja na mila hizo bado kuna changamoto ya kutokuwapo kwa vyoo hata kwenye shule za umma na wakati mwingine shule ikiwa na vyoo vinaweza kuwa si salama kwa wanafunzi.

Kwenye kampeni hiyo, jamii inahimizwa kujenga vyoo ambavyo ni bora vinavyozuia kuenea kwa kinyesi katika mazingira ya binadamu, kuwa na sakafu inayosafishika kwa maji, chumba chenye usiri.

Lakini baadhi ya vyoo vya shule, vya mijini na vijijini hapa nchini si salama, kwa maana ya ubovu na pia havina usiri, kutokana na ukosefu wa milango na mapaa, hivyo ni muhimu kuachana na mazoea hayo. Ni vyema jamii ikaendelea kuelimishwa ili itambue na kuthamini umuhimu wa kujenga vyoo bora na kuvitumia kuliko kuendekeza mambo ambayo yanachangia kuendelea kuwapo kwa kipindupindu.

Mwezi uliopita vyombo vya habari viliripoti kuwa watu watatu walifariki dunia baada ya kuibuka kwa kipindupindu Dar es Salaam.

Mbali na hao waliofariki dunia, wengine 55 wanaugua ugonjwa huo wakiwa kwenye kambi maalum za wagonjwa wa kipindupindu.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu ndiye aliyotoa taarifa hiyo akiwa katika ziara ya kutembelea bonde la Jangwani na kutaja maeneo korofi yenye ugonjwa huo.

Maeneo hayo korofi yaliyotajwa na waziri huyo ni Vingunguti, Tandika, Kariakoo, Keko, Buza, Kivule na Michikichini, lakini wito wake kwa jamii ukawa ni kuzingatia usafi ili kuepuka kuambukizwa ugonjwa huo.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Terack (katikati), baada ya kuwasili mkoani Shinyanga kwa ziara ya kikazi. Kushoto ni Inspekta Jenerali wa Polisi Simon Sirro. **PICHA: WMN**

# Waziri Mkuu Majaliwa, Rais wa Misri wateta

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Misri, Abdel Fattah Al- Sisi, ambapo wametumia fursa hiyo kuzungumzia masuala mbalimbali ikiwamo namna ya kuimarisha ushirikiano baina ya nchi za Tanzania na Misri.

Mbali na kuzungumzia masuala hayo ya kuimarisha ushirikiano katika nyanja mbalimbali zikiwamo za kisiasa, kiuchumi na kijamii, pia Waziri Mkuu amemfikishia Rais wa Misri salamu kutoka kwa Rais. John Magufuli.

Mazungumzo baina ya Waziri Mkuu na Rais wa Misri yalifanyika jana katika Ikulu jiji Cairo, ikiwa ni siku ya tatu na ya mwisho ya ziara yake ya kikazi nchini Misri. Katika ziara hiyo ameambatana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga. Waziri Mkuu amemaliza ziara yake ya kikazi nchini Misri, na katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Cairo aliagwa na Waziri wa Kilimo na Uhaulishaji wa Ardhi wa Misri, Dk. Ezz Eldien Abo Setit.

Akiwa katika ziara hiyo, Waziri Mkuu alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Misri, Dk. Mostafa Madbouly, katika siku yake ya kwanza ya ziara yake, ambapo aliwakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Misri waje kuwekeza nchini. Pia, Waziri Mkuu alitembelea miradi mbalimbali ya maendeleo nchini humo ambayo ni pamoja na wa ujenzi wa makao makuu mapya ya nchi hiyo, mradi wa awamu ya pili ya upanuzi wa mfereji wa Suez Canal na kiwanda kikubwa cha ngozi.

# Padri atoa neno ajali iliyoua wanahabari

**Na Mary Geofrey**

KUFUATIA ajali iliyotokea Jumatatu na kukatisha maisha ya watu saba wakiwamo wafanyakazi watano wa Azam Media, vyombo vya dola vinavyohusika na usalama barabarani vimetakiwa kuwajibishwa kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wao kikamilifu.

Hayo yalisemwa na Shemasi Severine Msavarotiani, wakati akihubiri katika ibada ya kuuaga mwili wa aliyekuwa mpigapicha wa Azam Media, Charles Wandwi iliyofanyika katika Kanisa Katoliki, Parokia ya Sinza na baadaye kuzikwa katika makaburi ya Sinza, jijini Dar es Salaam.

"Ili kulinda uhai wa maisha yetu hatuwezi kukwepa maisha ya kuwajibishana, kuleta takwimu za kusema mwaka huu ajali zimepanda au zimeshuka aisaidii kitu, kinachosaidia ni kuona jitihada za kupunguza ajali," alisema.

Alisema kila familia nchini imeguswa na janga ajali za pikipiki na magari kwa kupoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kupata viungo.

"Bila kumung'unya maneno hakuna jitihada za kupunguza ajali na kama zipo inawezekana vipi kwa sheria zetu za kuendesha kushoto dereva 'aovertake' (alipite gari) upande wa kulia na sheria zipo, watu wanaendesha maisha kiujanja ujanja tu," alisema.

Alisema vinapotokea vifo ni sarahisi watu kusema ni mapenzi ya Mungu, lakini yanapotokea majanga na ajali kama ile kunakuwa na kigugumizi.

Alisema kwenye ajali mchango wa binadamu katika kusababisha unakuwa ni mkubwa hasa katika ajali iliyosababisha vifo vya watu hao saba inaonyesha kuwa madereva hawakuonana.

"Niliangalia kwenye mitandao ajali iliyochukua ndugu zetu akiwamo Charles, inaonyesha kuwa madereva hawakuonana na wala hawakupata muda wa kukanyaga break wala hawakupata muda wa kukwepana," alisema.

Alisema walitegemea kuona somo la usalama barabarani linafundishwa shuleni lakini haifanyiki hivyo lakini pia waendesha baiskeli nao wangepata somo la udereva.

"Matokeo yake mtu anaenda kununua bodaboda anafundishwa kuwasha anaanza kuingia barabarani, anayenunua bajaji naye anajifunza kuendesha kwa muuzaji akitoka hapo anaingia barabarani, hivi ikitokea ajali tunaweza kusema ni mapenzi ya Mungu," alihoji Padri.

Alisema maisha hayawezi kuendeshwa kwa ujanja ujanja ila kila mmoja anatakiwa kutimiza wajibu wake hasa kuwa na jukumu la kulinda uhai na wa majirani.

Ajali hiyo ilitokea juzi Jumatatu asubuhi, katika eneo la Kizonzo, katikati ya Igunga mkoani Tabora na Shelui mkoani Singida na kusababisha vifo hivyo wakiwamo madereva wawili wa Coaster la kukodi ambao walikuwa wakielekea wilayani Chato mkoani Geita kikazi.

Katika ajali hiyo watu watatu walijeruhiwa vibaya na wanaendelea kupatiwa matibabu katika hospitali ya mkoani Arusha.

# Waziri aahidi kutatua mgogoro wa ardhi kwake

**Na Mwandishi Maalum**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ameahidi kuupatia ufumbuzi mgogoro wa ardhi katika Kijiji cha Ihari wilayani Kondoa, baada ya kupata malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoishi katika kijiji hicho.

Ahadi hiyo aliitoa wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji hicho ambapo wananchi na viongozi walipata nafasi ya kueleza changamoto mbalimbali zinazowakabili. Wananchi walieleza kuwa mgogoro huo umesababisha wengi wao kukosa mahala pa kuchungia mifugo yao kwa kuwa eneo lililokuwa limetengwa kwa ajili ya malisho limevamiwa na kubadilishwa matumizi kuwa mashamba.

Dk. Kijaji ambaye pia ni Mbunge wa Kondoa Vijijini, alisema taarifa za mgogoro huo ataziwasilisha kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ili aweze kutatua changamoto hiyo ambayo imekuwa kero kwa wananchi hao.

Alisema Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli ni serikali ya wanyonge na imepanga kutatua kero mbalimbali za wananchi ikiwamo migogoro yote ya ardhi nchini.

Dk. Kijaji aliwaomba wananchi hao wawe na subira katika kipindi hiki ambacho serikali inaenda kushughulikia tatizo lao, huku akibainisha kuwa utatuzi wa mgogoro huo unategemea sana utulivu wao kama walengwa. "Niwaombe ndugu zangu tuendelee kuilinda amani, tuendelee kuilinda amani ya Kondoa na nchi yetu kwa ujumla katika kipindi hiki ambacho tunamsuburi Waziri wa Ardhi ambaye anajua matumizi ya kila kipande cha ardhi nchini, atatue mgogoro huu," alisisitiza.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Ihari, Idi Lumba, amemshukuru Dk. Kijaji kwa kutenga muda wa kusikiliza changamoto zao hususan tatizo la ardhi ambalo lilianza kuwagawa wananchi wake.

# Baba mbaroni madai kubaka, kulawiti mwanawe

INATOKA UK. 3

huku yeye (baba) anasema nae. Nikamuuliza wewe vipi, akasema mtoto amejinyea, nikamwambia mbona hana tabia hiyo, akasema hata na yeye hajui kwa nini. Ikabidi niende kumchukua sababu alikuwa analia sana. Nilipofika naye ndani nilimweka kitandani akatulia kidogo nikamfunika shuka moja na baadaye nilipomwangalia vizuri niliona hayuko vizuri sehemu ya siri za nyuma," alisema.

Mama huyo alisema kulipokucha walichukua uamuzi wa kwenda Kituo cha Afya Kiroka na ndipo ilipobainika kuwa mtoto huyo alikuwa amebakwa na kulawitiwa na kutakiwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro ambako waligundua tatizo hilo na kuamua kumlaza kwa ajili ya matibabu.

Naye mjomba wa mtoto huyo, Hamisi Kiswile, alisema alipigiwa simu ya kuugua kwa mtoto huyo na alipofika hospitalini, madaktari walithibitisha kuwa mtoto kaharibiwa sehemu zote mbili.

Alisema alipoambiwa hivyo, alisema alimpa maneno laini shemeji yake ili aende Morogoro mjini kusaidia matibabu ikiwa njia ya kumdhibiti asitiroke kabla ya kutiwa nguvuni na polisi.

Kiswile alisema walipofika mjini walikwenda Kituo Kikuu cha Polisi na kupata karatasi ya kwenda nayo hospitali na kumwacha shemeji yake kituoni hapo. Mjomba huyo alisema ameumizwa sana na kitendo kilichofanywa na shemeji yake licha ya kwamba wanashukuru Mungu wamepokewa vyema hospitalini na mtoto anaendelea na matibabu.

Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa, Dk. Rita Lyamuya, alisema wamempokea mtoto huyo na kwamba amelazwa kwa ajili ya matibabu huku akiweka bayana kwamba inasemekana amefanyiwa tendo la kubakwa na hospitali imempokea na inaendelea kufanyia uchunguzi huku hali yake ikiwa inaendelea vizuri.

# Shahidi adai kupokea fedha za uuzaji kiwanja kwa Gugai

INATOKA UK. 4

"Nakala yoyote inayotolewa mahakamani lazima iwe halisi kwa mujibu wa sheria kifungu 67(1) na kama ni nakala yapo mazingira yanayoruhusu ipokewe." alidai wakili Malimi.

Hakimu Simba aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 11, 2019 atakopotoa uamuzi kama kielelezo hicho kipokewe au la.

Gugai na mwenzake watatu wanakabiliwa na mashtaka 43, yakiwamo 19 ya kughushi, 23 utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Kwa mara ya kwanza washtakiwa hao walifikishwa mahakamani Novemba 16, 2017 na walinyimwa dhamana kutokana na shtaka la utakatishaji kutokuwa na dhamana.

Gugai anakabiliwa na kosa la kumiliki mali kinyume na kipato chake, ambapo alitenda kosa hilo kati ya January 2005 na Disemba 2015.

Inadaiwa kuwa akiwa Takukuru Dar es Salaam, Gugai alikuwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake huku akishindwa kuzitolea maelezo.

# Bil. 3.5/- kununua chopa mpya polisi



INATOKA UK. 4

"Jeshi la Polisi tunampongeza sana Rais wetu John Magufuli (pichani) kwa kutujali. Ametupatia Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya kununua ndege mpya aina ya helikopta ambayo itatusaidia kuimarisha ulinzi na usalama hapa nchini," alisema Sirro.

"Napenda kutoa salama kwa Watanzania kuwa nchi yetu itabaki kuwa na amani na waharifu wote ni bora wafanye kazi halali za kuwaingizia kipato ikiwamo kujikita kwenye kilimo kwa sababu tutawakamata wote na kuwachukulia hatua kali za kisheria. Pia wasafiri wa usiku wasiwe na hofu, amani itaendelea kutawala," aliongeza.

Pia alisema jeshi linampongeza Rais Magufuli kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya kujenga nyumba 400 za makazi ya askari nchi nzima. Mpaka sasa zimeshajengwa nyumba 114 zikiwamo za mkoani Shinyanga.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, alimwomba mkuu huyo wa Jeshi la Polisi kutoa fedha ambazo zitakarabati nyumba zingine za askari ambazo zimeshachakaa ili kuwaboreshea makazi bora ambayo yatawafanya kuwa na ari ya kufanya kazi kwa bidii.

Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa nyumba hizo mkoani Shinyanga, Cosmas Taligura, alisema walipewa Sh. milioni 225 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tisa, lakini kutokana na ubanaji wa fedha hizo ikabidi waongeze nyumba nyingine na kufikisha 10.

# Kicheko mabasi kusafiri usiku

INATOKA UK. 2

kwa njia za Dar kwenda Mwanza na Dar kwenda Musoma.

**WASAFIRI WACHEKELEA**

Umoja wa Haki za Wasafiri wa Barabara, Maji, Anga na Reli (Uhawata), umeipongeza serikali kwa kuruhusu mabasi kutembea kwa saa 24 kwa kuwa itapunguza usumbufu kwa abiria wa kulala kwenye mabasi.

Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Umoja huo, Francis Mugasa, aliiambia Nipashe jana kuwa kwa miaka miwili mfululizo alikuwa akitetea haki za wasafiri likiwamo suala la mabasi yanayokwenda mikoa ya mbali kutembea kwa saa 24.

"Nilishaandika sababu 11 za kwa nini mabasi yaruhusiwe kutembea kwa saa 24, niliikabidhi hadi kwa Waziri Lugola. Nipongeze tu serikali kwa kufanya uamuzi wa kuruhusu mabasi kutembea usiku," alisema.

Alitaja sababu za kutetea uamuzi huo ni kuwa abiria walikuwa wanalazimika kulala kwenye mabasi maeneo ambako hakuna usalama, kukosa huduma muhimu kama za choo na maji.

Alisema kusafiri kwa saa 24 kutarahisisha shughuli za wananchi, kuokoa muda wao na kuongeza kasi ya kukuza uchumi kupitia shughuli wanazofanya.

"Uchumi wa wananchi utaimarika kwa sababu mtu kukaa ndani ya basi siku mbili ni kumpunguzia muda wa kuzalisha kiuchumi kwa hiyo sasa hivi kama kusafiri siku moja ina maana wasafiri watakuwa na muda mzuri wa kutimiza malengo yao," alisema.

Kadhalika, aliishauri serikali kuwasimamia wamiliki katika utekelezaji wa jukumu hilo, kama kuna vyombo vya usafiri ambavyo haviwezi kusafiri kwa muda mrefu kuwapo na mabasi ya kubadilishana.

Aidha, aliishauri serikali kushirikiana na umoja huo katika kuhakikisha wanaboresha sekta ya usafiri nchini na kupunguza malalamiko.

**POLISI YAONDOA HOFU**

Wakati hali ikiwa hivyo, Kikosi cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi kimewahakikishia abiria kuwa hakuna basi ambalo litaendeshwa kwa mwendo kasi.

Kamanda wa kikosi hicho, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Fortunatus Musilimu, aliiambia Nipashe jana kuwa wamejipanga kuhakikisha mabasi yanayosafiri saa 24 yanafika salama bila kusababisha ajali.

"Tunatekeleza maagizo ya waziri lakini pia tuna magari yetu ya doria ambayo hufanya doria usiku kucha. Wakati nyie mnalala sisi hatulali, tunazunguka usiku kucha. Hakuna shida magari yatafika salama, nawahakikishia usalama watumiaji wa vyombo vya usafiri," alisema Musilimu.

# NGO zapewa miezi 2

INATOKA UK. 3

ushawishi wa kisera.

Alizihakikishia asasi hizo kusajiliwa kwa mujibu wa sheria mpya na kuwatoa wasiwasi uliopo kwa baadhi ya asasi kudaiwa kulengwa ili kufutwa kwa kuwa zinaonekana kuikosoa Serikali.

"Baadhi ya wadau kutoka kwenye baadhi ya mashirika bado wana wasiwasi kuhusu hatma ya mashirika yao baada ya kupitishwa kwa marekebisho ya sheria, niwahakikishie hakuna Asasi ya kiraia yenye sifa itashindwa kupata usajili," Dk. Ndugulile alisema.

Sheria zilizofanyiwa marekebisho ni ya kampuni (sura ya 212), hakimiliki (sura ya 218), filamu na michezo ya kuigiza (sura ya 230), sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali (sura ya 56) ,Sheria ya vyama vya kijamii (sura 337), ya uwakala wa meli (sura ya 415), sheria ya muunganisho wa wadhamini (sura ya 318) na ya takwimu (sura 351). Akitoa ratiba ya huduma za usajili wa asasi hizo katika kipindi cha mpito, alisema Kanda ya Mashariki itakayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Morogoro huduma zitapatikana Dar es Salaam kwenye ofisi za Wizara ya Afya.

Kanda ya Kati itakayohusisha mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma, huduma zitapatikana Dodoma kwenye ofisi za Wizara ya Afya, Kanda ya Kaskazini huduma zitapatikana mkoani Kilimanjaro, Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini huduma zitapatikana Mbeya.

Hata hivyo, baadhi ya Asasi zimeeleza wasiwasi kuhusiana na muda, zikisema hautoshi.

**JUKATA YANENA**

Mkurugenzi wa Jukwa la Katiba Tanzania (Jukata), Bob Wangwe, alisema miezi mwili iliyotolewa haitoshi kukamilisha taratibu za usajili kwa asasi, na kwamba kuna uwezekano mkubwa wa baadhi ya mashirika kutokamilisha taratibu.

Tunaishauri serikali itumie busara katika suala hili kuliko kutengemeza nguvu za kisheria. Asasi zina mchango mkubwa katika jamii, hivyo kupoteza yoyote ni hasara kwa kuwa wanachangia kwenye uchumi wa nchi," alisema.

**KAULI YA LHRC**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema maeneo ya usajili ni changamoto mkubwa kwa kuwa siyo mashirika yote yana uwezo wa kusafiri kwenda kwenye ofisi za kanda.

"Wanavyoziona NGO wanafikiri zina fedha nyingi, siyo zote zina uwezo wa kusafiri kwenda kwenye maeneo ya usajili ambao wakati mwingine unaweza kuchukua muda mrefu," alisema.

Kuhusu muda, alisema hautoshi, na kwamba sheria imeruhusu waziri kuongeza muda iwapo ataona kuwa mashirika mengi hayajajiandikisha.

"Wametupa miezi miwili, lakini ni michache sana, lakini wametuambia fomu zitakuwa kwa elektroniki ambazo zinajazwa kirahisi, ikishaanza ndiyo tutajua ugumu wake," alisema.

## HABARI KITAIFA

### KESI YA KITILYA:

# Mkulo adai malipo ya Dola mil. 550 yalisitishwa

**Na Hellen Mwango**

WAZIRI wa Fedha wa zamani, Mustafa Mkulo, amedai mahakamani kwamba mpaka anaondoka katika wizara hiyo, mapendekezo ya mkopo wa Dola za Marekani milioni 550 yalisitishwa na kwamba ada ya uwezeshaji ilikuwa asilimia 1.4 na si 2.4.

Mkulo alitoa ushahidi huo juzi katika kesi inayomkabili Kamishna Mkuu wa zamani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Harry Kitilya na wenzake wanne, dhidi ya mashtaka 58 ikiwamo kula njama, kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani milioni sita.

Ushahidi huo unasikilizwa katika Mahakama Kuu Tanzania, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa iliyoketi chini ya Jaji Immaculata Banzi.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Osward Tibabyekomya, Hashimu Ngole na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Yamiko Lekana na Pius Hilla.

Awali kabla Mkulo ambaye kwa sasa ni mkulima hajaendelea kutoa ushahidi wake, mahakama hiyo ilipokea barua ya mapendekezo ya mkopo wa Dola za Marekani milioni 550. Akiongozwa na Wakili Hilla, shahidi alidai kuwa barua hiyo ya Februari 21, 2012 ilionyesha kwamba Tanzania ingepata mkopo huo kwa awamu mbili tofauti ikiwamo awamu ya kwanza Dola za Marekani 250 na ya pili Dola 300.

"Mtukufu jaji, mkopo huo ulitakiwa uwe umelipwa Aprili, 2012 kwa awamu zote mbili kwa riba ya asilimia 6.5 na waandaaji ilikuwa benki ya Standard Chartard ya nchini Uingereza" alidai na kuongeza:

"Hata hivyo, maandalizi hayakuweza kukamilika, hatukuweza kukopa kwa sababu majibu ya wataalamu yalisema mapendekezo yalichelewa kukamilika, mwaka ulikaribia kuisha walishauri tusubiri mwaka wa fedha 2012/2013," alidai Mkulo.

Alidai kuwa mwaka 2016 alitwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kueleza kilichotokea wakati nikiwa waziri kuhusu mkopo huo.

Alidai kuwa Takukuru walimhoji kama gharama za uwezeshaji zilitolewa kwa asilimia 2.4.

Hata hivyo, mpaka anaondoka wizarani Mei 4, 2015 mkopo ulikuwa umesimama na gharama za uwezeshaji zilikuwa asilimia 1.4 na si 2.4 na kwamba hakukuwa na mshauri mwingine zaidi ya Idara ya Sera na Benki Kuu Tanzania (BoT).

Mbali na Kitilya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Shose Sinare, Sioi Solomon, aliyekuwa Kamishna wa Sera na Madeni kutoka Wizara ya Fedha, Bedason Shallanda (kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu) na Alfred Misana, aliyekuwa Kamishna Msaidizi wa Sera na Madeni kutoka wizara hiyo (kwa sasa wizara ya afya).

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 49 ni ya utakatishaji fedha, mashtaka matatu ya kughushi, moja la kuongoza mtandao wa uhalifu, mawili ya kutoa nyaraka za uongo, shtaka moja la kujipatia fedha kwa njia ya udanyanyifu, kula njama ya kutenda kosa kutumia nyaraka kwa nia ya kumdanganya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango.



Mfanyabiashara Ophii Urasa akizungumza wakati wa mkutano wa NMB Business Club na wafanyabiashara wanaonufaika na mikopo ya benki hiyo wilaya za Babati, Hanang na Mbulu mkoa wa Manyara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahandisi wa maji watumbuliwa

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, awaondoe mara moja wahandisi wa maji wa Halmashauri za Wilaya za Kasulu na Kakonko mkoani Kigoma kutokana utendaji wao kutoridhisha.

Alisema wahandisi hao wawekwe pembeni ili watafutwe wengine wapya ambao watatatua changamoto za maji zilizopo katika wilaya hizo.

Aweso aliyasema hayo kwenye mkutano wa saba wa mwaka wa Bodi za Maji Mabonde uliyofanyika jana katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

"Lakini kwa eneo la Kasulu DC na Kakonko wahandisi wetu wa maji ni changamoto kwa hiyo tumeagiza Katibu Mkuu awaondoe mara moja katika kuhakikisha wanapatikana wahandisi wapya mwisho wa siku waweze kutatua changamoto za maji," alisema.

Aidha, alisema wahandisi hao wanaondolewa kwa sababu utendaji wao wa kazi hauridhishi, wakala wa maji waliyoanzisha ni kuwaweka watendaji wenye weledi wanaokubaliana na kasi ya utendaji ambayo wanakwenda nao kwa sasa.

Alisema lengo la kuanzisha wakala wa maji vijijini ni katika kuhakikisha wanaongeza utendaji ili wananchi waweze kupata maji.

# Takukuru yajinoa kwa watoa rushwa uchaguzi mitaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), Mkoa wa Dodoma, imewatahadharisha wagombea wa uchaguzi katika serikali za mitaa kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kuwa itatawanya askari kila kona.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema taasisi hiyo imejipanga ipasavyo kukabiliana na rushwa katika uchaguzi huo ili kusaidia wananchi kupata viongozi bora ambao wataliletea tija taifa.

"Hata wagombea wa uchaguzi huu kutoka vyama mbalimbali vya siasa tunawataka wasiwe wadanganyifu kwenye utoaji wa taarifa za rushwa za wagombea wenza kwa kuwa wote tutawachunguza," alisema.

Alisema wananchi wa Dodoma na maeneo mengine wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo wanapobaini kuna viashiria vya rushwa kwa wagombea kabla na baada ya uchaguzi, ili wapatikane viongozi wenye sifa.

"Naomba niwatahadharishe wagombea wa uchaguzi katika maeneo mbalimbali, Takukuru tutawakamata aliyetoa na kupokea rushwa kwa sababu wote ni wakosaji," alisema Kibwengo.

Alisema wanatakiwa kupata viongozi ambao wataleta maendeleo kipindi watakapochaguliwa na si kupata bora viongozi wanaoenda kujinufaisha wenyewe badala ya kusaidia wananchi.

Alisema wagombea wasijidanganye kuwarubuni wananchi kuwapa rushwa kutokana na kuwa tayari wameanza msako wa kubaini wapi kunafanyika vitendo hivyo ili waweze kuwashughulikia watakaobainika ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

Vile vile, alisema wameanza kutoa elimu katika vyuo na kwenye mikusanyiko mbalimbali jinsi ya kuwadhibiti watoa rushwa na wapokeaji kwa sababu wote ni wakosaji.

Alisema wameamua kutoa elimu hiyo kwa wananchi kwa sababu suala la rushwa si la Takukuru pekee bali kila mmoja anapaswa kuhusika kupambana nalo kwa namna yoyote kulingana na uwezo wake.

Katika hatua nyingine, aliwaonya watu wanaojiita maofisa wa Takukuru kuacha kuwatishia wananchi ilhali wao sio wafanyakazi katika taasisi hiyo.

Kibwengo alisema Takukuru inaendelea na uchunguzi kuhusiana na watu hao ambao watawachukulia hatua kali pale watakapobainika wanafanya vitendo hivyo.

"Naomba wananchi kuweni makini na watu wanaojiita maofisa wa Takukuru wakati sio kweli, ukiona una wasiwasi na mtu njoo utoe taarifa haraka," alisema Kibwengo.

# Wajasiriamali waiangukia serikali masoko

WAJASIRIAMALI wanaoshiriki katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, wameiomba serikali kuwatafutia soko la uhakika ndani na nje ya nchi ili kuwasaidia kuuza bidhaa zao.

Katika mahojiano na Nipashe, walisema pamoja na kuhamasika kuingia katika shughuli za ujasiriamali kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali, lakini bado hakuna soko la uhakika la kuuza bidhaa zao. Rosemary Mpanju, mjasiriamali anayelima zao lishe la Chia Seeds kutoka mkoani Kagera, alisema soko pekee ambalo bado wanalitegemea ni katika sehemu za maonyesho husussani Sabasaba na Nanenane.

"Wajasiriamali tumehamasika, tunatengeneza bidhaa mbalimbali, lakini bado hatuna soko la uhakika, tunategemea kama hivi Sabasaba na Nanenane au kwa mnunuzi mmoja mmoja," alisema Mpanju. Aliongeza: "Na wakati mwingine unakuta bidhaa kama tunazotengeneza sisi zinauzwa katika masupermakert, tunabaki tu tunashangaa wanazitoa wapi wakati kwetu hawanunui." Alisema ni vema serikali ikafanya utaratibu wa kuzuia uingizaji wa bidhaa kutoka nje ambazo pia zinazalishwa na wazawa na badala yake kuzipatia kipaumbele bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa ndani. Alitoa wito pia kwa Watanzania kuachana na kasumba ya kuthamini bidhaa za nje kuliko zinazotengenezwa ndani ya nchi.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Tigo Kanda ya Kaskazini, Aidan Komba (wa tatu kulia), akishirikiana na Diwani wa Kibaigwa, Richard Kapinye, kukata utepe kuzindua mnara wa mtandao wa 4G, katika Mji wa Kibaigwa, wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafundi wa majokofu, viyoyozi waitwa Veta

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imewataka mafundi wa majokofu na viyoyozi kusoma katika mamlaka hiyo kwa lengo la kufundishwa njia sahihi ya kufanya ukarabati wa vifaa hivyo bila kuharibu mazingira.

Akizungumza katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Mwalimu wa Chuo hicho Chang'ombe, Daudi Kadinda, alisema kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na mafundi hao wamekuja na teknolojia mpya itakayosaidia kutunza mazingira.

Alisema uharibifu mkubwa unaofanywa na mafundi hao ni pale wanapobadilisha gesi kutoka katika jokofu au kiyoyozi kilichoharibika kwa lengo la kutengeneza.

"Teknolojia hii ni ya kutunza mazingira bila kumwaga gesi unajua wanapofanya ukarabati na kumwaga gesi ni kitu hatari katika mazingira kwani gesi ile uenda juu na kusamba angani na kupanda kwenda katika anga kisha kutoboa tabaka la juu ambalo utoa mwanga wa jua moja kwa moja," alisema na kuongeza:

"Mwanga huo unaposhuka chini unawakumba watu na kusababisha kansa ya ngozi, ukame wa mimea," anasema.

Aidha, Kadinda anasema mafundi hao wanaweza kufanya ukarabati kwa njia mbadala kwa kunyonya gesi iliyomo kwenye jokofu au kiyoyozi kilichoharibika na kuweka kwenye mtungi mwingine wa gesi.

Alisema kifaa hicho kinaitwa Refrigent recover unit, na kuwa kinarahisisha kubadilisha gesi kwa usalama zaidi bila kumwaga gesi "Pia teknolojia hii inasaidia kuhifadhi gesi na ikimalizika kukarabati huirudishia katika jokofu au kiyoyozi kilichoharibika na kuendelea kutumia," anasema.

# Wananchi sasa waitwa kujifunza usafiri wa maji

SHIRIKA la Uwakala la Meli Tanzania (TASAC), limewaomba wananchi kufika katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam kujifunza mambo mbalimbali kuhusu meli na usafiri wa majini.

Akizungumza katika maonyesho hayo, Kaimu Mkurugenzi wa TASAC, Japhet Oloisimaye, alisema pamoja na uchanga wa shirika hilo lakini kuna mikakati mikubwa ambayo wamepanga kuitekeleza kwa ajili ya kuboresha zaidi ili lilete ufanisi na kuongeza uchumi wa nchi. "Kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2003, kifungu cha 21 tumepewa jukumu la kudhibiti usalama wa vyombo vya majini, hakuna chombo ambacho kitaruhusiwa kuingia majini bila kutambulika ubora wake na anayekiuka hilo lazima achukuliwe hatua za kisheria," alisema Oloisimaye.

Alisema utekelezaji wa sheria hiyo unafanyika kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Meli Duniani (IMO) ambalo linataka kila nchi mwanachama kusimamia usalama wa vyombo vya majini.

Tayari kanuni 22 zimekwisha kutengenezwa ili kusimamia sheria hiyo ya usafirishaji majini ya 2003 Nampa 21 na ya TASAC 2017 ambayo inaipa nguvu shirika hilo kusimamia vyombo hivyo vya majini.

**HABARI ZOTE NA ELIZBETH ZAYA**

## Neema ya soko kwa wazalishaji muhogo

WAZALISHAJI wa muhogo nchini, wataanza kunufaika baada ya kukutanishwa na wanunuzi wa zao hilo wa ndani na nje ya nchi na kuingia nao makubaliano ya kununua zao hilo.

Wakizungumza kwenye mkutano wa Siku Maalum ya Sekta ya Nafaka, Muhogo na Mazao Jamii ya Kunde katika Maonesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, wadau wa zao hilo walisema hatua ya kukutana ana kwa ana na wakulima wa zao la muhogo limefungua ukurasa mpya kwenye sekta hiyo.

Mwakilishi wa kampuni kutoka Rwanda inayonunua zao la muhogo, David Batty, alisema kupitia mkutano huo wamepata wasambazaji watatu wa Tanzania watakaowasambazia tani 35,000 za muhogo.

"Tunashukuru maonyesho haya ya Sabasaba yamekuwa ya maana kwetu na kwa wakulima wa zao la muhogo, tumeonana ana kwa ana na kufahamu wapi tutapata bidhaa na kwa kuanza tumekubaliana na tutaendelea kufanya mawasiliano na mawakala 10 tuliowapata leo (jana) watakaotusambazia muhogo," alisema Batty.

Alisema kampuni hiyo ya Rwanda mahitaji yake ya muhogo mbichi ni tani 75,000 hadi 150,000 kwa mwaka na kwamba nafaka hiyo wanainunua nchini Tanzania kwenye mikoa jirani na Rwanda.

"Awali tulikuwa tunanunua muhogo mbichi kutoka mikoa jirani na Rwanda, lakini sasa tumekuza hapa na tumepata soko zaidi ambalo litatosheleza mahitaji ya kampuni yetu, sisi tutachukua muhogo kutoka kwa mawakala ambao wao watakuwa wanakusanya kutoka kwa wakulima," alisema Batty.

Alisema mwaka jana walinunua tani 50,000 za muhogo mbichi kutoka Tanzania kwenye mikoa hiyo jirani na Rwanda na kwamba kampuni hiyo inazalisha bidhaa za wanga kutokana na muhogo, bidhaa za unga, vyakula vya mifugo na mbolea kiasi kinauzwa nchini Rwanda na kiwango kingine kinasafirisha nje.

Alitaja nchi wanakouza bidhaa hizo za muhogo kuwa ni Ujerumani na Ubelgiji, na kwamba baada ya kupata mawakala Tanzania wa kuwauzia zao hilo ambapo kuwakala waliowapata ni kutoka mikoa ya Morogoro, Bagamoyo na Pwani.

"Tutaanza kununua tani 35,000 kwa wakala huyo wa Bagamoyo ambaye amesema ataweza kutuletea muhogo ambao wao watakusanya kutoka kwa wakulima," alisema Batty.

Naye mkulima wa zao hilo kutoka Kigoma, Ayenko Choroka, alisema amefurahi kuhudhuria mkutano huo ambao umemsaidia kupata soko la zao hilo.

# Wafa wakimkimbia kiboko ziwani

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAVUVI wawili waliokuwa wanavua samaki katika Ziwa Babati, wamepoteza maisha baada ya mtumbwi wao kuzama wakati wanamkimbia Kiboko ili asiwashambulie.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, amethibitisha kwamba tukio hilo lilitokea Julai 7, mwaka huu, majira ya saa 9:00 alasiri huku akiwataja waliopoteza maisha kuwa ni Paul Elias(45) mkazi wa Bagara Ziwani na Nicodemus Peter (43) mkazi wa Nangara Ziwani.

"Wakati wanaopolewa ziwani walikuwa wamefariki dunia huku mtumbwi wao waliokuwa wanautumia kuvulia samaki ukiwa umepinduka," alisema Senga.

Alisema chanzo cha tukio hilo bado kinachunguzwa lakini taarifa za awali zinaonyesha watu hao walikuwa wanamkimbia mnyama kiboko ndipo mtumbwi wao ukapinduka na kusababisha vifo hivyo.

Kamanda Senga aliongeza kuwa miili ya marehemu haina majeraha popote na imekabidhiwa kwa ndugu zao kwa ajili ya maziko.

Wakati huo huo, polisi wanamshikilia Iddy Nkwabi(41) mkazi wa Kata ya Makame wilayani Kiteto, kwa tuhuma za kupatikana na nyara za serikali bila kuwa na kibali cha mkurugenzi wa wanyamapori. Senga alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na kwato mbili za twiga, mifupa minne ya twiga na nyama kavu ya twiga, gamba la kakakuona, pua mbili za nguruwe pori na mkia wa sungura. Alisema tukio hilo lilitokea Julai 3, mwaka huu na kwamba mtuhumiwa alikamatwa akiwa na silaha aina ya gobore na risasi 55 zilizotengenezwa kienyeji.

"Mbinu aliyoitumia ni kuhifadhi vielelezo kwenye mfuko wa lambo kwenye kambi haramu waliyokuwa wamejenga ndani ya hifadhi ya jamii ya Makame, kwa ajili ya shughuli zao za kijangili,"alisema Aliongeza kuwa chanzo cha tukio hilo ni kujipatia kipato na kitoweo kinyume cha sheria.



Mbunge wa Jimbo la Kiteto mkoani Manyara, Emmanuel Papian, akimsikiliza mkazi wa Kijiji cha Engusero John Mollel kwenye kikao cha kusikiliza changamoto na kuzungumza nao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# CCM yagawia kofia ngumu madereva pikipiki

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Themi, mkoani hapa, kimewapatia kofia ngumu madereva wa pikipiki( bodaboda) 100 kwa lengo la kuwanusuru na ajali zisizo za lazima na kusababisha kupunguza nguvukazi ya taifa.

Akizungumza juzi kwenye mkutano wa hadhara wa chama hicho, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Themi, Thomas Munisi, alisema mpango huo umelenga kuondoa changamoto ya kutokuwa na kofia ngumu na kusababisha baadhi ya waendesha pikipiki kukamatwa na askari wa usalama barabarani.

Munisi alisema chama kimetoa msaada huo kutokana na ombi lililotolewa wakati wa kufungua mashina katika kata hiyo. Baadhi ya vijana waliomba kupatiwa kofia ngumu ili waepukane na kamatakamata ya polisi.

"Sisi Chama tulipokea ombi lao na nikaona tunaweza kuwafadhili kupitia mpango wetu wa kuwezesha vijana na sasa tunawakabidhi kofia hizi," alisema.

Baadhi ya waendesha pikipiki, Elisha Mbise na Simon Swai walishukuru CCM Kata ya Themi kwa kuwawezesha kupata kofia hizo kwa kuwa zitawasaidia kujikinga na ajali wakati wakitekeleza majukumu yao.

Katika hatua nyingine, Munisi aliwaonya wanachama wa chama hicho, kuacha kuwabeba baadhi ya wagombea wa CCM kwa maslahi yao, kwa kuwa chama hicho kina mfumo mpya wa kupata viongozi wake.

Pia aliwataka wanachama kuacha tabia ya kutembea na majina ya wagombea mfukoni, kwa kuwa kila mwanachama anayetaka kugombea anapaswa kuja ofisini kuchukua fomu.

"Ule uongozi wa zamani wa kila mwanachama kuwa na viongozi wake mfukoni kwa sasa hilo halipo na tukigundua kuna mgombea yeyote anatumia wanachama kutaka uongozi, tutamfyekelea mbali," alisema Munisi.

Alisema CCM imewanyakua baadhi ya wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wanaokihama chama hicho, baada ya kuridhishwa na utendaji kazi wa CCM chini ya Mwenyekiti wa Taifa, Rais John Magufuli.

## Wataka mazingira rafiki kwa wakulima

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI kwa kushirikiana na taasisi za fedha zimeombwa kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha wakulima kukopesheka kwa urahisi kwa kuweka dhamana mashamba yao, ili kuboresha kilimo na kulima kibiashara zaidi.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Huduma katika Kijiji cha Kilimatembo, Kata ya Rhotia Wilayani Karatu, Fabiano Petro, alipokuwa akizungumza katika siku ya wakulima iliyolenga kutembelea mashamba darasa na kujifunza mbinu bora za kilimo na changamoto zinazowakabili.

Petro alisema wakulima wengi, hususani walioko vijijini, wamekuwa wakikabiliwa na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo hali inayosababishia kuendelea kulima kimazoea.

Kutokana na hali hiyo, waliomba kuwekewa mazingira rafiki ili kuwawezesha kukopesheka na kuendeleza kilimo bora.

"Unajua kwa sasa hivi gharama za pembejeo za kilimo ziko juu sana, hali inayowafanya wakulima kushindwa kulima kisasa na kuishia kulima kilimo cha kimazoea ambacho mwisho wake wanaishia kupata hasara na kutokuwa na ari ya kupenda kilimo," alisema.

Meneja Masoko wa kampuni ya kizalendo ya usambazaji na uzalishaji wa mbegu za mahindi ya IFFA, Luhenda Yangole, aliwataka wakulima kuyatumia mashamba darasa yalioandaliwa kama mfano, kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima, ili kulima kilimo cha kibiashara na kuondokana na kilimo cha kimazoea.

Yangole alisema changamoto kubwa iliyoko kwa wakulima wengi ni wengi wao kutofanya kilimo kama biashara kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya mbegu bora za kisasa na matumizi bora ya zana za kilimo.

Naye Ofisa Mazao wa Wilaya ya Karatu, Twilumba Ngwale, aliwataka wakulima hao kubadilika na kutumia kanuni bora za kilimo kama wanavyoelekezwa na wataalamu mbalimbali huku wakiyatumia mashamba darasa hayo kujifunza na kujua mbegu bora za kilimo zinazowafaa.

Mmoja wa wakulima katika Kijiji cha Kilimatembo, Jackson Musa, aliziomba kampuni za mbegu kuendelea kuwatembelea wakulima vijijini na kutoa elimu juu ya matumizi bora ya mbegu.



Watoto wa wafanyakazi wa kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania Plc, wakifurahia chakula katika tamasha la "Bring Your Kid to Work" lililofanyika makao makuu ya ofisi za kampuni hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashiru: Msiwachagulie waumini wenu viongozi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka viongozi wa dini kutowachagulia waumini wao viongozi wa kuwachagua katika kampeni za uchaguzi na badala yake watekeleze jukumu la kuwaandalia viongozi bora wenye hofu ya Mungu.

Dk. Bashiru alitoa kauli hiyo jana wakati alipokutana na viongozi wa dini wa madhebu mbalimbali mkoani Kilimanjaro, wilayani Moshi na kuzungumza.

Alisema jukumu kubwa la viongozi wa dini ni kuwaandalia waumini wao viongozi bora na sio kuwachagulia nani awaongoze.

Alisema, wananchi wakipata viongozi bora wenye hofu ya Mungu watakuwa mstari wa mbele kusimamia haki pamoja na kupambana na rushwa na ufisadi kwa maslahi mapana ya wananchi.

Mtendaji mkuu huyo wa CCM alisema kuwa, wapo baadhi ya viongozi wa siasa ambao wamekuwa wakitumia dini kutafuta nafasi za uongozi, lakini pia wapo baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakijiingiza katika siasa kutafuta kiki na kuwataka kubadilika.

"Viongozi wa dini mna jukumu kubwa la kuhakikisha waumini na viongozi mnaotuongoza tunafuata haki na hili litafanikiwa kupitia mahubiri yenu bila kuelekea upande wowote," alisema Dk. Bashiru.

Pia alisema viongozi wa dini nchini wana haki, uhuru na uwazi kutoa ushauri wao kwa serikali na kusaidia kuondoa migongano, mivutano na matamko ambayo hayana tija kwa nchi.

Vile vile aliwataka viongozi hao kuhubiri na kusimamia haki na kuwa endapo wakianza kusimamia na kuhubiri dhuluma amani na upendo haitakuwapo.

Alisema, haki katika rasilimali ya ardhi ni tatizo na eneo hilo limekuwa likiwagusa watu wengi kutokana na baadhi ya watu kujilimbikizia ardhi kubwa bila kuitumia.

"Tatizo la migogoro ya ardhi katika taifa letu ni kubwa hivyo viongozi wa dini niwaombe kupaza sauti zao katika mahubiri na mawaidha katika sekta ya ardhi na niwaombe msichoke endeleeni kisaidia serikali katika jambo hili," alisema Dk. Bashiru.

Akizungumzia suala la kodi, alisema wapo wananchi ambao hawana hiari wenyewe katika ulipaji kodi, lakini pia wapo wasimamizi ambao wamekuwa wakipindisha sheria za kodi ili wale rushwa na kuwaomba viongozi wa dini kuisaidia serikali katika juhudi za kukusanya kodi kwa maslahi mapana ya maendeleo ya wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi hao wa dini, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Daiyosisi ya Pare, Charles Mjema, alisema serikali ya sasa ni sikivu na wao wanaendelea kuiombea ili iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Askofu Mjema alisema, viongozi wa dini wanawajibu mkubwa wa kuishauri serikali na kudai kuwa zipo changamoto ambazo viongozi wa dini watahitaji kukaa pamoja na serikali ili kushauriana.

"Dini zimekuwa zikiisaidia serikali katika huduma mbalimbali, kama sekta ya afya, elimu, maji na kupitia wafadhili tumekuwa tukipewa misaada, lakini imekuwa ikitozwa kodi na nitumie nafasi hii kuiomba serikali kuangalia kwa jicho pana ili kutoa msamaha wa kodi," alisema Askofu Mjema.

# Kiwanda cha kahawa taabani kwa madeni

**Na Paul William,** MOSHI

KIWANDA cha kukoboa kahawa cha Moshi (The Tanganyika Coffee Curing Company), kinakabiliwa na madeni ya jumla ya Sh. bilioni 1.3 na kusababisha kukosa uwezo wa kukarabati mitambo na miundombinu pamoja na kushindwa kulipa mishahara na stahiki za watumishi.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Kandata Kimaro, alisema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya kiwanda hicho kwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alipofanya ziara kiwandani hapo.

Kimaro alisema, kiwanda hicho kwa sasa kinakabiliwa na madeni makubwa hali ambayo imekuwa ikichangia kushusha ufanisi wa kazi zake na kusababisha kushindwa kulipa tozo za kodi ya serikali kwa mujibu wa sheria.

Alisema, changamoto nyingine inayokikabili kiwanda hicho ni kushuka kwa kiwango cha mapokezi ya kahawa kiwandani kwa ajili ya ukoboaji ambao umeshuka kutoka tani 31,000 kwa mwaka 1988/89 hadi kufikia tani 11,000 mwaka 1996/97 na kuendelea kushuka hadi chini ya tani 1,000 msimu wa 2018/19.

"Sababu zinazopelekea kushuka kwa mapokezi hayo ni kuanzishwa kwa viwanda vya Mbozi na Mbinga ambavyo vinawahudumia wakulima wa Kanda za Kusini na Nyanda za Juu Kusini ambao walikuwa wakihudumiwa na kiwanda hicho," alisema Kimaro.

Alisema, kati ya mwaka 2012 na 2014 yalifanyika mauzo ya nyumba tatu za kiwanda na magari matatu vyote vikiwa na thamani ya Sh. bilioni 2.255 ambazo hazikutumiwa kwa shughuli za kiwanda inavyopasa na kudumaza maendeleo ya kiwanda hadi leo.

Aliongeza kuwa, taarifa za minada zinaonyesha kuwa kahawa iliyokobolewa kiwandani hapo hununuliwa kwa bei ya chini tofauti na iliyokobolewa kwenye viwanda binafsi kwa madaraja yaliyofanana hali inayosababisha wateja wengi wa kiwanda kukoboa kahawa yao kwenye viwanda binafsi.

Kwa upande wake, Dk. Bashiru alisema anasikitishwa na kitendo cha uongozi uliopita wa kiwanda hicho kukihujumu kwa kununua mitambo mipya isiyofanya kazi.

Alisema kitendo hicho ni ubadhirifu wa mali za umma na hakiwezi kukubalika na kuahidi kuwa wale wote waliotenda kosa hilo lazima wachukuliwe hatua stahiki.

Vile vile alisema, kushuka kwa zao la kahawa ni kutokana na kufa kwa ushirika pamoja na wale waliokabidhiwa dhamana ya kuongoza mali za umma kutokuwa waaminifu.

# Wawekezaji wazawa waomba punguzo la kodi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAWEKEZAJI wazawa mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kupunguza kodi zinazowakabili ili kuimarisha uwekezaji pamoja na kutoa ajira kwa vijana.

Akizungumza na Nipashe, Meneja Msaidizi wa Marenga Milis, Priva John, alisema kuwa serikali iangalie namna ya kupunguza mrundikano wa kodi unaowakabili wawekezaji wa ndani hali inayokwamisha wawekezaji wazawa wenye mitaji midogo.

Alisema upunguzaji wa kodi utasaidia wawekezaji wazawa kuimarisha thamani za bidhaa wanazozalisha na kuwa na bei nafuu.

"Tunaiomba serikali ikae na wizara husika pamoja na halmashauri kuangalia namna bora ya kumvutia mwekezaji mzawa ili aweze kumudu gharama za uzalishaji na kusaidia kuwapo kwa bidhaa zenye ubora kwa bei nafuu.

Mmoja wa wafanyabiashara wakubwa katika Manispaa ya Moshi, Elia Malya, alisema kama serikali ina nia ya dhati ya kwenda kwenye serikali ya viwanda ni lazima kuwatazama wawekezaji wazawa na kuwapunguzia mzigo wa kodi.

Alisema ikiwa watapunguziwa mzigo wa kodi wataweza kuzalisha kwa wakati na bidhaa zenye ubora na bei zake zitakuwa nafuu.

"Sisi wafanyabiashara tunaonekana sio wazalendo, lakini sio kweli bidhaa za kutoka nje ya nchi zinakuwa zinauzwa kwa bei nafuu zaidi kuliko zile zinazozalishwa ndani ya nchi... na hiyo ni kutokana na mrundikano wa kodi wanazotozwa wawekezaji wa ndani na kushindwa kuzalisha na kuuza bei nzuri," alisema Edward Mroso.

Mwanaisha Mzava, alisema mbali na bidhaa hizo kuzalishwa kwa gharama kubwa na kushindwa kuuza bei ambayo ni ya kawaida, wamekuwa wakishindwa kulipa wafanyakazi mishahara mikubwa kutokana na faida ndogo wanayozalisha.

Akijibu kuhusu mishahara midogo inayotolewa na baadhi ya wawekezaji kwenye viwanda vyao, Ofisa kazi Mfawidhi Mkoa wa Kilimanjaro, Mwinyimkuu Mturuya, alisema wanaendelea kutoa elimu ya haki na wajibu wa wafanyakazi pamoja na waajiri.

"Tunaendelea kufanya ukaguzi wetu wa mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya uundaji wa vyama vya wafanyakazi kazini na kutoa elimu ya haki za wafanyaki na wajibu wa waajiri...hivyo ikiwa kuna taasisi hawajatendewa haki na waajiri wao tunaomba wafike ofisini kwetu kwa wakati tutalifanyia kazi," alisema Mturuya.

# ama

ALHAMISI JULAI 11, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 15

## NEMC kuna kelele nyingi zinazotibua mazingira



Ukurasa 18

## Kuwanyima leseni mabondeni si kuondoa makazi hatarishi



Ukurasa 14

## Tabianchi yatishia kuongeza umasikini



# Kunyonyesha kikamilifu ni chanzo cha akili nyingi

Ukurasa 20

## Tabianchi yatishia kuongeza umasikini

RIPOTI mpya ya Umoja wa Mataifa imesema baa la njaa linaongezeka duniani na itashindwa kutimiza lengo la kumaliza umasikini uliokithrii ifikapo 2030 pamoja malengo mengine ya Umoja wa Mataifa.

Ripoti hiyo iliyotathmini hatua inayopigwa kuelekea kutimiza malengo endelevu 17 ya Umoja wa Mataifa ifikapo 2030, imesema juhudi kubwa zinatatizwa na mabadiliko ya tabia nchi na kuongezeka kwa ukosefu wa usawa duniani.

Ofisa wa Ofisi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Liu Zhenmin, amesema licha ya mafanikio kadhaa yaliyopatikana ikiwemo kupunguza idadi ya vifo vya watoto na ongezeko la watu wanaotumia nishati ya umeme, dunia bado inakabiliwa na changamoto za kutisha.

Anasema mabadiliko ya tabianhi ndiyo kitisho kikubwa zaidi ambacho kinaathiri mafanikio yaliyokwishapatikana hususan katika kupunguza hali ya umasikini duniani.

**DW**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres .

AFYA

# Kuchanganya methadone na mihadarati ni kujimaliza



Mmoja wa watumiaji wa dawa za kulevya akijidunga sindano. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

VIJANA takribani 1,983 wanatibiwa athari za mihadarati kwa kupatiwa dawa ya methadone, katika kituo kilichopo Hospitali ya Mwananyamala, jijini Dar es Salaam.

Vijana hao wamekuwa wakifika kila siku katika kituo hicho kwa ajili ya kupata ushauri na kisha kumeza dawa ya methadone ambayo kazi yake ni kutibu akili ili kuachana na utegemezi wa dawa nyingine za kulevya.

Matumizi ya dawa za kulevya imekuwa ni changamoto inayowakumba vijana, ambayo serikali na wadau wa vita dhidi ya dawa hizo wamekuwa wakipambana nayo kuhakikisha inamalizika.

Lakini kumekuwapo na madai kwamba baadhi ya vijana wanaokwenda kwenye vituo vya kunywa methadone, huwa wanarudi mitaani na kuendelea kujidunga sindano au kunywa dawa nyingine za kulevya. Wapo ambao wamewahi kutajwa kwa majina wakiwamo wasanii waliopelekwa katika nyumba ya kutibu watu walioathirika na dawa za kulevya (sober house), lakini wakatoroka.

> **Kuchanganya dawa ya methadone na dawa nyingine za kulevya kunaweza kusababisha mwili kuzidiwa na dawa (overdose), hali ambayo inaweza kuhatarisha maisha.**

Hata hivyo, msimamizi wa kituo cha kutolea dawa za methadone katika Hospitali ya Mwananyamala, Dk. Jofu Hongo anasema, mtu anayekunywa methadone na kisha anachanganya na dawa za kulevya, ana hatari kubwa ya kupoteza maisha.

### ATHARI ZA KUCHANGANYA

Dokta Hongo anasema, mhusika anapoanza dozi, anapaswa kumweleza mfamasia au daktari kuhusu dawa ulizokunywa kabla ya kutumia methadone, kwa vile kama amekunywa pombe au dawa ya usingizi kama valium, fenegan au piriton, anaweza kufa iwapo atachanganya na methadone.

"Kuchanganya dawa ya methadone na dawa nyingine za kulevya kunaweza kusababisha mwili kuzidiwa na dawa (overdose), hali ambayo inaweza kuhatarisha maisha," anasema Dk. Hongo.

Mtaalam huyo wa afya anafafanua kuwa methadone ni dawa ya usingizi na ni maalumu kusaidia muathirika kurudia hali ya kawaida, lakini akichanganya na za kulevya, mhusika anaweza kupatwa na umauti ghafla.

"Hivyo mtu akitoka kunywa methadone kisha akanywa hizo za kulevya, ajue anaweza kufa ghafla kwasababu atakuwa amejizidishia dozi na pia anaathiri ini lake na mwisho ni kifo tu," anasema.

Anasema, wakati mwingine methadone hutumika kutuliza maumivu makali ya muda mrefu au yanayosababishwa na magonjwa yasiyotibika na kwamba watu wakianza kutumia tiba ya methadone, baadhi hujisikia raha iliyozidi na kujiskia kusinzia hali ambayo pia huletwa na baadhi ya dawa za kulevya.

"Tiba ya kila siku ya methadone inaweza kuendelea hadi miaka miwili kufikia hatua muathirika kupona kabisa, na pia wakati mwingine inategemea ametumia dawa za kulevya kwa muda gani," anasema.

Anafafanua kuwa iwapo methadone itasitishwa ghafla dalili za tumbo kusokota, kuharisha, maumivu ya misuli na mifupa hutokea, na kwamba dalili hizo hujitokeza ndani ya siku moja hadi tatu tangu dozi ya mwisho na kisha baadaye hupungua polepole ingawa dalili nyingine kama matatizo ya usingizi na hamu kali ya dawa za kulevya zinaweza kuendelea kwa miezi kadhaa.

"Hapa kituoni tumewekeana mkataba kwamba wasirudi kwenye uteja wanapotoka kunywa dawa, tukishagundua kuwa kuna mtu wa aina hiyo tunafuta jina lake, hivyo wako makini sana," anasema.

### SABABU ZA TIBA

Mtaalamu Dk. Hongo anasema kuna sababu nyingine zinazochangia watu kutumia dawa za kulevya, lakini kuu ni nne, mojawapo ikiwa ni mtu kujaribu baada ya kushawishiwa na wenzake na kujikuta akiwa teja.

"Hapa pia kuna tatizo la kisaikojia, kwamba mtu anaweza kupata changamoto za maisha na kujikuta akitumia dawa za kulevya kwa lengo la kupunguza msongo wa mawazo na kumbe anajiharibu," anasema.

Anasema wakati mazingira nayo yanachangia, kwamba mtu anaweza kukulia katika mazingira ambayo anaona dawa za kulevya zinatumiwa kila siku na kumfanya naye ashawishike kuzitumia.

"Wakati mwingine wapo wanaoathiriwa na vinasaba kutoka kwa wazazi wao, ambao hutumia dawa hizo nao wao wanapokua hujikuta wakitumia pia, au inawezekana mwingine akawa na afya ya akili, ambayo humsababisha atamani kutumia dawa za kulevya," anasema.

### VITA YA MIHADARATI

Serikali inasema imefanikiwa kudhibiti biashara ya madawa ya kulevya kwa asilimia 90 na sasa watumiaji wamebuni mbinu nyingine ambazo tayari zimebainika na zinashughulikiwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama ndiye anasema hayo kwamba asilimia kubwa ya vijana kwa sasa wamebianika kutumia kemikali za sumu baada ya serikali kudhibiti biashara ya madawa ya kulevya.

"Serikali imebaini mbinu mpya ya vijana kutumia sumu ya panya na dawa za usingizi kama mbadala wa dawa ya kulevya baada ya serikali kudhibiti biashara ya uingizwaji wa dawa ya kulevya hapa nchini," anasema Mhagama.

MAZINGIRA

# NEMC kuna kelele nyingine nyingi zinazotibua mazingira

Na Mwandishi Wetu

KELELE ni uchafuzi wa mazingira, tena zisizo na mpangilio kama mziki unaotoka kwenye bajaji, bodaboda na kwenye magari ya matangazo na ya binafsi, ni kero mitaani na barabarani.

Si hivyo tu hata muziki unaotokana na sherehe mitaani nao unatibua utulivu na uzuri wa mazingira. Iwe ni harusi au 'kitchen party' wengine huona kama ni kero na huchafua amani, hali ya ngoma za masikio na utulivu wa akili.

Suala la kelele zinazodaiwa kusikika kutoka misikitini na kwenye makanisa limeibuka tena wiki hii kwenye mkutano wa Amani uliofanyika kwenye maonyesho ya Biashara ya Kimataifa jijini ar es Salaam.

Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), likitajwa kuwa linataka hatua zichukuliwe kuzidhibiti kwa mujibu wa sheria. Misikitini zinatoka adhana, wakati kwenye makanisa inasikika milio ya kengele ambayo kwa mujibu madai yanayoelezwa kuwa yanatolewa na NEMC, ni kilele zinazodumu kwa zaidi ya dakika mbili hivyo, kwa mujibu wa sheria hazikubaliki.

Licha ya kwamba NMC imeshafafanua na kukanusha kuingilia uhuru na haki za watu kuabudu kwa kukataza adhana na kengele zisikike, suala hili linahitaji kutizamwa na kwa kushirikisha wadau wengi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Amani Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Sheikh Musa Salum, anasema NEMC wanataka uchokozi . Kuwaambia waamini waachane na adhana ama kengele makanisani viongozi wa dini hawatakubali.

Sheikh Salum anawaeleza washiriki wa kongomano la Amani lililofanyika kwenye viwanja vya Saba Saba jijini Jumanne wiki hii kuwa ni vyema kuwa makini kwenye kutunga sheria na kutoa matamko.

Anaikumbusha NEMC: "Ukitaka watu wakutii ni vyema kuwa na sheria ama kanuni ambazo watu watazitii."

Vingine anasema wataweza wasiafikiane na serikali ama NEMC, kupitia miongozo na maelekezo hayo.

### SAUTI ZA KELELE

Pamoja na kwamba NEMC ndiyo wakala mwenye jukumu la kusimamia mazingira , hoja za kutaka kuondoa ibada ya kengele na adhana kwa maelezo kuwa ni kelele kwenye mazingira ni jambo ambalo linahitaji kujadiliwa na wahusika, kupimwa na kuona kama linachukuliwaje.

Kengele na adhana ni mambo ambayo hufanyika kwa muda mfupi na si wakati wote na yapo katika taratibu za ibada. Kwa vile watu wanao uhuru wa kuabudu ni vyema viongozi wa dini wakazungumza na serikali kuona hatma ya suala hilo.



> Bajaji na bodaboda zenye muziki mkali hukatiza mitaani, shuleni na hata jirani na hospitali, hizi nazo NEMC inasemaje?

Sheikh Salum, anapotoa kilio hicho, anamweleza Naibu Spika, Tulia Aksoni, kuwa Waislamu na Wakristo hawakubaliani na NEMC kuhusu ibada zao kuhusishwa na kelele.

Hata hivyo, Spika Tulia Aksoni, anasema kama kiongozi wa muhimili wa kutunga sheria, analichukua na kuondoka na jambo moja nalo ni: "Kama unataka watu wa kutii huwezi kuwa na sheria ambazo ni vigumu kuzitii."

NEMC kama chombo cha kusimamia uhafadhi na usalama wa mazingira kina mambo ambayo kinapaswa kuyatizama kabla ya kuingilia adhana na kengele makanisani hata kwa siku zijazo.

Waamini wengine wanaweza kuhisi kuwa baraza hilo limeanza kumchukia Mungu. Pengine kuna hoja lakini kabla ya kwenda huko, NEMC ingetumia sheria kuzibana kelele za miziki mizito inayosikika kwenye bajaji, bodaboda, daladala na magari ya matangazo.

Huko kuna kelele za kutisha na huenda kunaweza kuwa mwanzo wa ajali za barabarani kwa kuwa vyombo kama bajaji zama hizo hufungwa spika au vipaza sauti vikubwa na vyenye uwezo wa kuchuja mziki na ukasikika kwa sauti kali zijulikanazo kama sub hoofer (sab ufa)

Bajaji na bodaboda zenye muziki mkali hukatiza mitaani, shuleni na hata jirani na hospitali, hizi nazo NEMC inasemaje?

Muziki mzito husikika kutoka kwenye baa na hoteli zilizo mitaani, hili nalo NEMC imeliona? Kwanini baa zisiwe na mitambo ya kuzuia kelele kama zilivyo kumbi za shughuli za kijamii?

Ni jukumu la NEMC kudhibiti kelele , lakini hata muziki unaochezwa mtaani iwe harusi, 'sendiof' na ngoma za kuwacheza wali , inayosikiwa kuanzia mchana hadi saa 6.00 usiku nazo ni kero kwa wananchi. Baraza liangalie namna ya kuupunguzia umma kelele hizo kama si kuzikomesha.

Magari barabarani yana kelele nyingi na muziki mkubwa mko wapi NEMC hamuoni hasa ya matangazo? Hili nalo ni kero kwenye masikio ambayo yanafurahia adhana na kengele, zinazosikika kutoka nyumba za ibada.

### MOSHI BARABARANI

Wakati mwingine ni rahisi kusikia kelele zinazotoka kwenye nyumba za ibada , lakini wadau wa kusimamia mazingira hawaoni kitanzi kinachotokana na kutumia magari yenye moshi mzito yanayopita barabarani?

NI kawaida mijini na vijijini kukutana na magari makubwa kwa madogo yanayofuka moshi mzito yakipita barabarani hata mbele ya vyombo vya usalama bila kuonywa.

Haya nayo NEMC hawayaoni? Kama hawajayaoni vipi mamlaka ya kusimamia usafiri wa ardhini nayo haijakutana na vyombo hivyo ikalishauri baraza la mazingira, kulikemea na kulikomesha?

NEMC inawezekana moshi wa injini ukawa kitisho kwa afya za watu kuliko suala la kelele. Moshi wa injini una kemikali za sumu ambazo husababisha magonjwa na uchafuzi wa mazingira na kuchangia ongezeko la joto duniani.

Mwishoni mwa mwezi uliopita huko Bonn Ujerumani mkutano wa kimataifa wa mazingira ulilizungumzia suala la ongezeko la joto duniani na kuonya kuhusu uzalishaji wa hewa ukaa.

Hewa ya ukaa au karboni ni uchafu ambao umo ndani ya injini za magari. Jopo la wataalamu wa mazingira wa kimataifa wanaoshughulikia tafiti na mapendekezo ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, linaeleza kuwa kwa sasa joto la dunia limepanda.

Ripoti za jopo hilo zinasema limeongezeka kwa nyuzi joto 1.5 na kwamba kama hatua hazitachukuliwa ifikapo mwaka 2052 huenda likaongezeka zaidi na kufikia nyuzi mbili na kueleza kuwa kuna hatari zaidi baharini na visiwani kutokana na kina cha maji kuongezeka. Huenda visiwa vikazama, huku viumbe wa baharini wakitishiwa uhai na ongezeko hilo.

Kwa hiyo NEMC isifumbie mienendo ya kuchafua mazingira kama kuacha magari yanayofuka moshi kutembea barabarani, itumie sheria kudhibiti na hatua zichukuliwe.

Inawezekana NEMC hawajazungumzia suala la adhana na kengele, lakini kuna wananchi wamelitaja suala hilo kwenye mitandao, hivyo ni vyema kutumia changamoto hiyo, iliyotolewa na wazalendo kuangalia maeneo mengine yanayoongeza kero na uchafuzi wa mazingira ambayo hayagusi imani wala ibada za Watanzania.

AFYA

# Teknolojia ikutumiwa ipasavyo itaongeza ulaji nyama Tanzania



Mizani ya kidijitali inamwezesha kila mlaji kupata nyama kulingana na fedha zake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wengi nyama inawashinda kununua licha ya kwamba Tanzania ni taifa la tatu au la pili kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika.

Ya kwanza kwa mujibu wa Shirika la Kilimo na Chakula Duniani kwa idadi kubwa ya ng'ombe barani Afrika ni Ethiopia, ikifuatiwa na Sudan. Kitoweo cha mifugo ni muhimu kwa afya kwa vile ni chanzo cha protini na vitamin B12.

Nyama nyekundu kama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo husaidia mwili kuwa na vitamin za kutosha na kuimarisha mfumo wa fahamu. Huzipa seli za mwili afya bora na kuimarisha mfumo wa kinga ikiuwezesha kufanyakazi kikamilifu. Protini ambazo ni muhimu kwa afya ya mifupa na misuli inapatikana kwenye nyama hivyo ni chakula muhimu.

Kwa mujibu wa mujibu wa Shirika la Chakula na Lishe Duniani (FAO), mtu mzima anatakiwa kula wastani wa kilo 50 za nyama kwa mwaka, lakini kwa Watanzania , FAO inaeleza kuwa wananchi hawamudu, hula viwango vidogo vya wastani wa kilo 15 pekee kwa mwaka ikiwa ni upungufu wa kilo 35 ili kutimiza kiwango kinachohitajika kitaalamu.

> **Inampa nafasi kila mmoja kupimiwa kile anachostahili kulingana na fedha yake. Mizani inapima, aidha inakokotoa gharama.**





Mizani ya kukatia nyama (kushoto) inayochukua nafasi ya gogo na shoka.

Nipashe inaifikisha changamoto hii kwa Bodi ya Nyama ya Taifa (TMB), yenye wajibu wa kukuza na kuendeleza sekta ya nyama ili kuongeza pato la mfugaji, taifa na kuleta tija kiuchumi, inayotoa maelezo yafuatayo.

Anayetoa ufafanuzi ni Meneja Masoko na Utafiti TMB, Nicholai Chaweka, wakati akizungumza na gazeti hili kwenye maonyesho ya Saba Saba yanayoendelea jijini Dar es Salaam...

**NIPASHE: Unaelezea madai kuwa gharama kubwa ya nyama ndiyo inayosababisha watu wengi kutomudu kitoweo hicho?**

**BODI:** Watanzania wengi wanaweza kujitetea kuwa hawali nyama kwa sababu ya ughali na kwamba kipimo cha nyama kipo katika kiwango mahsusi ni kilo moja inayouzwa wastani wa Sh 6,000, nusu kilo 3,000 na robo kilo 1,500.

Kama una Sh.700 au 1,000 ni vigumu kupata nyama lau kama una 2,000 pia huwezi kununua kitoweo kulingana na thamani ya fedha hiyo. Hata pale unapokuwa na Sh 2,800 ni vigumu pia kwa sababu imepungua sh 200 ili kupata kilo moja. Hii ni kwa sababu uzani umekadiriwa kwa utaratibu wa kilo moja, nusu kilo , au robo na mawe ya mizani yapo kwa kupima uzito huo na sivinginevyo.

Nyama ni tofauti na dagaa ambazo wateja wanaweza kupata dagaa wa Sh 500, hata 700 au zaidi kutegemeana na fedha walizonazo lakini si kitoweo. Hata mshikaki ni Sh 500, japo una finyango tatu.

**NIPASHE:Ni nini ufumbuzi kuwawezesha wateja wenye viwango tofauti vya uchumi na mapato kumudu kitoweo?**

**BODI:** Hili kama mamlaka tumeliona na tunafanya jitihada kuhamasisha matumizi ya mizani ya kidijitali ambayo inaweza kupima nyama ya uzito wowote tena kulingana na kiasi cha fedha mteja alichonacho.

Kwa mfano nyama ya Sh 500 au 1,000 ama 1,200 inaweza kupimwa kwa kutumia mizani hiyo ya kisasa zaidi.

"Inampa nafasi kila mmoja kupimiwa kile anachostahili kulingana na fedha yake. Mizani inapima, aidha inakokotoa gharama. "

Bodi inahamasisha hili kwa wauza nyama na kitoweo kwenye bucha na sehemu zote chakula hicho kinapouzwa. Lakini zaidi kwenye mabucha ambako Watanzania wengi wananunua nyama.

Tunawahimiza wafanyabiashara kufahamu umuhimu wake na kutumia fursa hiyo ya kiteknolojia ili angalau kila mmoja ale nyama na kiwango kiongezeke kutoka kilo 15 kwa mwaka hata mara mbili au zaidi.

**NIPASHE: Vipi suala la bei na upatikanaji ukoje? Na gharama zake ni rafiki au ni changamoto?**

**BODI:** Mizani hizo ziko sokoni na hata hapa kwenye maonyesho ya SabaSaba zinapatikana (wateja) au wafanyabiashara wanaweza kumudu. Bei zake zinaanzia Sh. 300,000 na kuendelea. Tuna wenzetu wa sekta binafsi tunashirikiana nao wanahusika kwenye uuzaji vifaa vya biashara ya nyama.

## GOGO NA SHOKA

**NIPASHE: Teknolojia haiishii kwenye mizani pekee, unazungumziaje kukata nyama kwa kutumia teknolojia ya kisasa badala ya gogo na shoka?**

**BODI:** Nianze kwa kueleza kuwa nilazima tukubali sasa na kuanza kuikata nyama kwa msumeno. Wengine huita meat saw au born saw.

"Shoka tangu mwanzo halikukusudiwa kutumiwa kukata nyama wala kitoweo chochote. Lile matumizi yake ya kukata kuni na miti msituni ama kwenye mapori. Shoka haliwezi kukata nyama kikamilifu kwani linapasua mifupa na kutawanya vipande vya mifupa ndani ya nyama na kukifanya kitoweo kisilike na hata supu kujaa mifupa."

Lakini pia katika mchakato wa kulitumia huacha vibanzi vya gogo na kusababisha nyama kuwa vibanzi pamoja na vipande vya mifupa. Kubwa zaidi nyama ikikatiwa kwenye gogo hujaa vimelea vya maradhi kwa kuwa halioshwi kwa miaka yote linapotumika, hali inayoweza kueneza magonjwa na kusababisha maambukizi.

Wakati mwingine vibanzi na vipande vya mifupa ni hatari kwa afya kwani vinaweza kuleta athari kwa mlaji hasa vikimchoma tumboni.

> **Ni wazi kuwa ukataji nyama kwa kutumia shoka pamoja na kuharibu nyama si salama kwa mteja lakini pia humpa mjasiriamali hasara kubwa.**

## UPOTEVU WA NYAMA

Shoka linapotumiwa kila wakati linasababisha upotevu wa nyama. Tena kila mara kuna vipande husambaratishwa na kurukia pembeni au chini kila mara nyama inapokatwa.

Yote hii husababisha hasara kwa mjasiriamali na hata mfanyabiashara mkubwa. Kitaalamu tunakadiria kuwa wastani wa kuanzia gramu 500 hadi kilo mbili hupotea kila siku shoka linapotumika.

"Hebu fikiria iwapo wastani wa kilo moja hadi mbili zitapotea kila siku. Itakuwaje kwa wiki, mwezi hata mwaka? Ni wazi kuwa ukataji nyama kwa kutumia shoka pamoja na kuharibu nyama si salama kwa mteja lakini pia humpa mjasiriamali hasara kubwa."

Kwa kutumia msumeno wa nyama ni rahisi kukata nyama ipasavyo kukatakata na kuusaga mfupa kwa utaratibu unaofanya kitoweo kipendeze bila kuwa na mifupa na vibanzi vinavyokera wakati wa kutafuna nyama au kunywa supu hata kula chakula kilichochanganywa na nyama mfano ndizi.

Upatikanaji wa misumeno ya nyama pamoja na mizani ya kidijitali inaweza kuwa changamoto vijijini ambako hakuna umeme wa kuendesha mashine hizo.

Hata hivyo uchunguzi uliofanywa na Nipashe kwenye maonyesho ya Sabasaba uliobaini bei ya msumeno wa nyama huuzwa kuanzia Sh. 450,000 na kuendelea.




## Kliniki yashtakiwa kuzalisha watoto waliochakachuliwa

WENZA wenye asili ya Asia ambao walijaribu kupata watoto kwa njia ya kupandikiza (IVF), wamedai kuwa kumetokea mkanganyiko katika hospitali ya mjini California nchini Marekani, kitendo kilichosababisha wapate watoto wasio wao.

Mashtaka yaliyofunguliwa na wenza hao jijini New York yanasema wawili hao walipata mshtuko baada ya kuzaa watoto wawili wa kiume ambao hawakuwa na chembe yeyote ya Asili ya Asia kama ilivyo kwa wazazi hao.Vyombo vya habari nchini Marekani vimeripoti.

Vipimo vya nasaba, DNA vinathibitisha kuwa watoto hao hawakuwa na uhusiano wowote na wapenzi hao.

Kliniki hiyo haijasema chochote kuhusu shutuma hizo. Wapenzi hao ambao wamepewa majina ya AP na YZ wamesema kwa muda mrefu walikuwa wakitafuta watoto kisha wakatumia kiasi cha pauni 80,000 kama gharama za hospitali na kupandikiza.

Inaripotiwa kuwa baada ya kujifungua Machi 30, wapenzi hao walishtuka kuona watoto ambao waliambiwa walipandikizwa kwa kutumia jeni (genes) zao hawakuwa waliowatazamia.

Kulikuwa na dalili awali kuwa vitu havikuwa sawa baada ya kufanyiwa uchunguzi wakati wa ujauzito na kuambiwa kuwa walitegemea watoto wa kiume, ingawa madaktari waliwaambia hawakupandikiza viinitete vya kiume wakati wa matibabu yao.

Madaktari wameripotiwa wakiwaambia wapenzi hao kuwa uchunguzi huo umetoa majibu yasiyo sahihi, kabla ya kwenda kujifungua watoto wawili wa kiume mwezi Aprili.

Mbali na kuwa watoto hawakufanana na wazazi hao, watoto wenyewe pia hawakufanana.

Kwenye tovuti ya kliniki hiyo ya uzazi, iitwayo CHA imesema inatoa huduma hizo kwa umakini wa hali ya juu na huduma zilizo bora kabisa. **BBC**

MAZINGIRA

# Kuwanyima leseni mabondeni si kuondoa makazi hatarishi



Mafuriko ni athari zinazotokea kwa wakazi wanaokaa mabondeni kama inavyoonekana katika picha. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MVUA za masika zimemalizika na sasa kinachoendelea ni watu kujiandaa kwa msimu wa vuli. Japo hakukuwa na taarifa za maafa na mafuriko kutoka kwenye msimu wa mvua zilizopita, lakini ni wakati wa kutafakari na kuangalia usalama wa makazi, hasa kwenye mikondo ya maji, kwa vile watu wengi ndipo wanapoishi.

Ikumbukwe kuwa kila mwaka Oktoba 13 ni Siku ya Kimataifa ya Kupunguza Maafa. Maadhimisho hayo hufanywa ili kutekeleza Azimio Namba 64/200 lililopitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa Desemba 21, 2009.

Siku hiyo ilichaguliwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili kukuza utamaduni wa kupunguza maafa kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuzuia maafa, kujitayarisha kuyakabili na kupunguza madhara ya maafa yanapotokea.

Katika maadhimisho hayo umma unakumbushwa kuhusu kuwa na makazi bora na salama.

Siku ambayo watu hukumbushwa kujenga ufahamu na kupunguza maafa kwani bila makazi bora hakuna maendeleo.

Katika kuadhimisha siku hiyo ni wakati wa kuangalia namna ya kuondokana na makazi duni.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imenza kupima makazi yasiyo rasmi na kutoa leseni za makazi , kwa Tanzania nzima.

> **Pengine kuwaambia watu kuwa serikali haitawapimia hakutoshi, ni lazima kuwa na malengo ya kimkakati ya kuhamasisha watu kuhama mabondeni na maeneo hatarishi.**

Kama ilivyo nia ni kuondoa au kupunguza makazi katika maeneo hatarishi, kupunguza athari na kuhama kutokana na maafa.

Upimaji unaofanyika haupimi maeneo hatarishi hasa kwenye mabonde na katika mikondo ya maji.

Wapimaji hawawapimii wananchi wanaokaa maeneo hayo, hivyo hawatapata leseni ya makazi na pengine hawatahusika kuchangia kodi ya ardhi.

Lakini hakuna anayeamuru kuondoka maeneo hayo. Hivi kama watabaki na kuendelea kujenga na kuwekeza azma ya kuondokana na makazi duni itakuwa imetimia?

Siku ya makazi duniani inalenga kutoa fursa ya kutambua maendeleo yanayofanywa ili kupunguza madhara na hasara katika maisha, mfumo wa maisha na afya, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na rasilimali za mazingira ya watu, biashara, jamii na nchi.

Iwapo watu wataachiwa kuendelea kujenga kwenye maeneo hatarishi ni dhahiri kuwa kupunguza madhara ya maafa kunaweza kusifanikiwe.

Pengine kuwaambia watu kuwa serikali haitawapimia hakutoshi, ni lazima kuwa na malengo ya kimkakati ya kuhamasisha watu kuhama mabondeni na maeneo hatarishi.

Pamoja na kwamba serikali inapima na kutoa hati za makazi bila kuwa na mikakati ya kuwaondoa watu kwenye makazi duni, inawezekana kusiwe na tija kwenye kupunguza maafa.

Umoja wa Mataifa katika kupunguza maafa umeandaa mikakati kadhaa ambayo ni lazima kuisimamia hii ni pamoja na kuzuia, kulinda na kupunguza idadi ya watu wanaoathirika na majanga wakiwamo hao wanaoishi kwenye mabonde ukanda wa mafuriko na sehemu hatarishi.

Kuangalia usalama wa watu wote, lakini hasa wale walio katika hatari zaidi ya kifo, kuumia, kuathirika kiafya, madhara ya mfumo wa maisha, kuhama makazi yao na ukosefu au uduni wa huduma za muhimu na za msingi.

Hali hiyo huibuka kutokana na matukio ya maafa hasa kwa wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wazee.

Katika kudhibiti maafa na makazi duni, makundi haya ni muhimu kwa kuwa yana viwango tofauti vya uwezekano wa kuathirika na majanga.

Katika upimaji wa makazi na kutoa leseni ni vyema pia kuangalia watu wanaoishi kwenye makazi duni, huenda idadi kubwa ikawa ni wanawake na watoto maskini.

Wapimaji wanapaswa kuangalia umuhimu na ubora wa nyumba za kuishi badala ya kukwepa kuwapimia. Ikumbukwe nyumba ya familia mahali rasmi na salama pa kuishi wakati wa maafa.Iwapo hawatapewa leseni za makazi na wakaruhusiwa kuishi ni itakuwa hatma yao wakati wa maafa?

Mwaka 2017 taarifa za makazi za Umoja wa Mataifa ilieleza kuwa watu waliokuwa wanaishi mabondeni walikuwa ni milioni 24.2 walihama makazi yao kutokana na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali duniani.

Ikumbukwe kuwa maafa ni miongoni mwa vyanzo vya umaskini na dhiki kwa watu wengi walio katika mazingira magumu hasa wanaoishi katika nchi zinazoendelea.

Kupunguza madhara yanayotokana na kuongezeka watu kuhamia maeneo hatarishi ni jambo linalohitaji kupewa kiupaumbele.

Ikumbukwe kuwa kuishi mabondeni kunaongeza uwezekano wa kuharibifu mazingira kwani kunatishia na kuchafua na kukausha vyanzo vya maji.

Wakati mwingine ni chanzo cha mabadiliko ya tabianchi hivyo ni vyema kuzuia kusiwapo makazi hayo au kukabiliana nayo yasiongezeke ikibidi kuwahamisha wanaokaa mabondeni badala ya kuwabakiza kwa kuwanyima leseni za makazi.

Pamoja na kuwaongezea leseni ni vyema kuhimiza na kuongeza ufahamu kuhusu hatua za kuchukua ili kuboresha makazi, kuwa na sera za kupunguza uwezekano wa jamii kuathirika kutokana na kuishi maeneo hatarishi.

Ni dhahiri kwamba kuchukua hatua katika suala hili kutaonyesha mafanikio endapo kutachangia matokeo chanya katika kuokoa maisha, kupunguza hasara za kiuchumi na kupunguza uharibifu wa miundombinu muhimu na mazingira.

AFYA

# Utafiti: Upungufu wa mbegu za kiume unahatarisha maisha

WANAUME wenye mbegu chache za kiume wako katika hatari ya kupata magonjwa kwa mujibu wa utafiti mpya.

Kazi ya kitafiti iliyofanywa kwa wanaume 5,177 ilibaini kwamba wanaume wenye mbegu chache za kiume wana mafuta mengi mwilini, shinikizo la damu na mafuta machafu katika mishipa ya damu.

Pia wana uwezo mkubwa wa viwango vidogo vya homoni za kiume.

Waanzilishi wa utafiti huo wanasema kuwa, wanaume wenye mbegu chache za kiume ni muhimu wakafanyiwa vipimo vya magonjwa mengine.

**HATARI**

Upungufu wa mbegu za kiume na matatizo ya ubora wa mbegu hizo ni masuala yanayoathiri mmoja kati ya wanandoa watatu kushika mimba kulingana na utafiti huo uliofanywa nchini Uingereza.

Lakini katika utafiti huu mpya wanasayansi walichanganua wanandoa wasioweza kupata watoto nchini Italia, kujua iwapo ubora wa mbegu hizo pia unaathiri afya ya mtu kwa jumla.

Waligundua kwamba wanaume wengi walio na mbegu chache walikuwa na matatizo kadhaa ya kiafya ikiwamo mwili ulionenepa na shinikizo la damu.

Hatua hiyo huongeza hatari ya kupata ugonjwa wa kisukari, magonjwa ya moyo na kiharusi.

Wanaume hao pia walionekana kuwa na viwango vya juu vya kuwa na homoni chache za kiume ambazo hupunguza ukubwa wa misuli na mifupa na huenda vikasababisha ugonjwa wa kudhoofika kwa mifupa.

Daktari Albert Ferlin ambaye aliongoza utafiti huo anasema:

"Wanaume wasio na rutuba hukumbwa na matatizo ya kiafya ambayo yanaweza kuhatarisha hali yao ya maisha na kupunguza kiwango cha maisha wanayoishi," anaongeza:

"Rutuba huwapatia wanaume fursa isiyo ya kawaida ya kutathmini afya na kuzuia magonjwa."

Hata hivyo, wamiliki wa utafiti huo wanasisitiza kuwa utafiti wao haukuthibitisha kuwa ukosefu wa mbegu za kiume za kutosha husababisha matatizo ya kimetaboliki badala yake ni vitu viwili vinavyohusiana.

Wanasema kuwa uhaba wa homoni za kiume huhusishwa na matatizo haya ya kiafya.

Dk. Ferlin anasema kuwa utafiti unaonyesha ni muhimu kwa wanaume wanaotibiwa matatizo ya ukosefu wa rutuba kuangaziwa vizuri kimatibabu.

"Wanaume walio na matatizo ya kuwapatia mimba wake zao wanafaa kukaguliwa vizuri na kufuatiliwa na wataalam wao wa rutuba kwa sababu huenda wana viwango vya juu vya kupata maradhi na vifo," anasema.



Mihogo, karanga, nazi mbata huuzwa kwenye barabara nyingi jijini Dar es Salaam na mijini mingine kwa maelezo kuwa huongeza nguvu za kiume. Ndivyo mteja anavyochangamkia tiba. **PICHA: MTANDAO**

> Rutuba huwapatia wanaume fursa isiyo ya kawaida ya kutathmini afya na kuzuia magonjwa.




**NGUVU ZA KIUME**

Taarifa ya BBC inataja kuwa maeneo mengi nchini vijijini na mijini kuna mabango mengi yanayotoa matangazo mbalimbali rasmi na yasiyo rasmi kuhusiana na kutoa dawa za asili hasa za kuongeza nguvu za kiume.

Miongoni mwa dawa hizo ni zile zenye majina kama 'ujana' ambayo kazi yake ni kusaidia kuongeza nguvu za kiume.

Dawa zingine zinatajwa na kuwa na majina kama sudhi, vatari, IH Moon na coloidal silver ambazo kazi yake ni kudhibiti vimelea mbalimbali mwilini na kuongeza nguvu za kiume.

Baraza la dawa nchini linaeleza kuwa hatua hiyo imekuja baada ya uchunguzi wa kina uliofanywa na kubaini kuwa dawa hizo hazina madhara kwa afya ya binadamu, hivyo hawana budi kuzikubali.

Aidha, Paul Muhame ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa dawa za asili nchini anasema baada ya baraza kupitisha vigezo vyote vilivyohitajika kutoka katika dawa hizo, iliyokuwa Mamlaka ya Dawa na Chakula m(TFDA) pia imethibitisha hilo.

"Suala la muhimu ambalo tumeliangalia zaidi ni usalama wa mtumiaji...katika upande wa kuthibitisha kuwa dawa hizo zinaponyesha au la, linabaki kwa mnunuzi na mtumiaji wa dawa hiyo," anasema Muhame.

Makala ilifanya jitihada za uthibitisho wa dawa za asili nchini Tanzania ambao umezua mjadala mkali katika vipindi vya radio nchini hasa kwa upande wa serikali kuthibitisha dawa za nguvu za kiume kuuzwa kihalali.

BBC ilipata maoni mbalimbali kutoka kwa Watanzania kuhusiana na uthibitisho wa dawa hizo:

"Watu watazinunua lakini hakuna mtu atakuwa na uhakika kwamba dawa hizi zinatibu, sana sana atabahatisha tu," anasema Thomas Hemed, mkazi wa jiji la Dar es Salaam na kuongeza:

"Inaweza isilete madhara, lakini huwezi kujua baadaye...kiukweli inabidi ziangaliwe kwa watu maalum kwa watu wanaouza ili mtu akidhurika ajue ataenda kwa nani."

**SABABU ZA KUKOSA NGUVU ZA KIUME**

Sababu za kukosa nguvu za kiume zinaainishwa kuwa ni pamoja na magonjwa (kisukari, saratani), msongo wa mawazo na kutumia aina fulani ya dawa kwa mfano dawa za kudhibiti msukumo wa damu (BP)

Pia umri mkubwa, kukosa usingizi wa kutosha na matatizo ya kihomoni. **BBC**

AFYA

# Kunyonyesha kikamilifu ni chanzo cha akili nyingi

Na Gaudensia Mngumi



Watoto hawa huenda ni matokeo ya unyonyeshaji ambao wataalamu wanasema huwawezesha kuwa na akili na kiwango kikubwa cha maarifa wakiwa na umri mdogo na wengi huvutiwa na kupenda masomo: **PICHA MTANDAO**

MWEZI wa nane unawakumbusha wazazi kuwanyonyesha watoto wachanga kwa miezi sita. Na pale mtoto anapozaliwa anatakiwa kuanza kunyonya ndani ya dakaki 30 au nusu saa.

Anahitaji kula maziwa ya mama kwa miezi sita mfululizo bila kunywa maji, kulambishwa asali wala, uji wa mhogo au chai ya rangi.

Mwezi wa kunyonyesha unapokaribia kumalizika, huenda wanawake wa Tanzania hawazingatii kikamilifu maelekezo ya kuwanyonyesha watoto wachanga kwa miezi sita mfululizo.

Nipashe ilihojiana na baadhi ya wazazi wa Dar es Salaam, kuhusu kuzingatia maelekezo hayo ya kitaalamu na kubaini kuwa inakuwa vigumu wengi kuzingatia maelekezo.

Mathalani, Ziada Mselemu ni mkazi wa Mbezi Msumi ana mtoto wa wiki sita lakini amemkaribisha duniani kwa kumlambisha asali.

Ziada mwenye watoto watatu anasema kadhalika, hawanyonyeshi wanae miezi sita kwa sababu wanapata njaa na anaona wana dalili za kuhitaji chakula.

Anaeleza kuwa ni mazoea kwa baadhi ya makabila kumpa 'mgeni' kitu kitamu ili kumpa upendo na kuzuia kulia kwa mara nyingi wamezoea kulia. Jane Mkwawa, anayefanya usafi katika benki moja Mbezi anasema kuwa anampa mwanae maji yenye asali na dawa nyingine za asili ili kumzuia asilie.

Mama huyu wa watoto wawili anasema hawanyonyeshi wanae kwa miezi sita kwa sababu wanalia na anahisi wana njaa.

**SABABU ZA KULIA**

Hivi mtoto anapolia ana njaa? Mitandao ya afya kama 'Mayo Clinic', inaeleza kuwa watoto wachanga duniani kote wanalia wengine usiku na hata mchana kutwa, hivyo si kila anapolia ana njaa.

Mtandao unataja baadhi ya sababu za kulia kuwa ni kutaka kukueleza tatizo lake. Ana shida ndiyo sababu ya kulia muda.

Pengine anaumwa ni vyema ukampeleka hospitali badala ya kubuni kuwa ana njaa na kuanza kumlisha uji bila sababu.

**UMUHIMU WA KUNYONYESHA**

Wakati dunia inatarajiwa kuadhimisha siku ya unyonyeshaji itakapofika Agosti, wazazi wakijua faida ya kunyonyesha na umuhimu wa maziwa ya mwanzo kabisa ya mama kwa mtoto wake itakuwa suala la tija kwa mtoto wa Tanzania.

Makala ya BBC iliyoko kwenye mtandao wa shirika hilo, inasema takriban asilimia 40 ya watoto wachanga wenye umri kati ya miezi sifuri hadi sita ndiyo wanaoishi kwa kunyonyeshwa pekee, kulingana na taarifa zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

> Kunyonyeshwa kwa muda mrefu pia huchangia afya na maisha bora ya mama kwani humpunguzia hatari ya kupata saratani ya mfuko wa mayai ya uzazi na matiti.

Kadhalika shirika hilo linasema kuwa zaidi ya maisha ya watoto 820 000 walio na umri wa chini ya miaka mitano yanaweza kunusurika kila mwaka, ikiwa watoto wenye umri kati ya miezi sifuri hadi miezi 23 wangenyonyeshwa kikamilifu.

BBC inasema ni muhimu kunyonyesha kwani ni moja ya njia sahihi ya kuhakikisha mtoto anakuwa mwenye afya na kuendelea kuishi kuanzia muda anapozaliwa.

Kama viwango vya kunyonyesha vingekuwa vya hali ya juu duniani, takriban maisha ya watoto 820 000 yangenusurika kila mwaka, kwa mujibu wa WHO.

Unyonyeshaji wa mtoto kwa miezi sita mfululizo una faida nyingi za kiafya kwa mama na mtoto na kuanza kumpa maziwa mara anapozaliwa kwa kipindi cha saa moja, humkinga na maambukizi yanayowapata watoto wachanga na kupunguza vifo vya watoto wachanga. Maziwa ya mama pia ni chanzo muhimu cha nguvu na virutubisho kwa watoto wa kati ya miezi sita hadi 23, wataalamu wanasema yanaweza kuchangia nusu au zaidi ya nguvu za mtoto katika umri wa miaka sita hadi 12

Tafiti zinaonyesha kuwa watoto na vijana wadogo walionyonyeshwa wakiwa wachanga wana uwezekano mdogo wa kuwa na uzito wa mwili wa kupindukia, kwa maana nyingine maziwa hayo hudhibiti unene kupindukia miongoni mwa watoto.

BBC inaeleza kuwa unyonyeshaji wa mtoto kikamilifu humsaidia kuboresha uwezo wa utambuzi wa akili (IQ), kuwa mwerevu na kuwa na mahudhurio makubwa shuleni na pia huhusishwa na mapato ya juu katika maisha yake ya utu uzima.

"Kunyonyeshwa kwa muda mrefu pia huchangia afya na maisha bora ya mama kwani humpunguzia hatari ya kupata saratani ya mfuko wa mayai ya uzazi na matiti."

BBC, inawakumbusha wazazi na kuongeza kuwa aidha hutengeneza vichocheo vya mwili (hormone) ambazo humtuliza mama na mtoto wake mchanga.

**KUTONYONYESHA**

Wakati mwezi ujao ni maadhimisho ya kunyonyesha kimataifa, baadhi ya wanawake duniani wanashindwa kuwanyonyesha watoto wao ipasavyo kutokana na sababu mbali mbali.

Licha ya juhudi mbali mbali ambazo zimekuwa zikifanyika kuelimisha kinamama na jamii nzima juu ya umuhimu wa kunyonyesha na maziwa ya mama kwa mtoto, baadhi ya mila na tamaduni hususan za Kiafrika zimekuwa na changangoto kubwa ya kuelewa na kukubali umuhimu wa kunyonyesha kutokana na kukosa elimu ya kunyonyesha.

Miongoni mwa changamoto zinazochangia wanawake kushindwa kuwanyonyesha watoto wao ni pamoja na kazi, magonjwa pamoja na tamaduni nyingi zisizomruhusu mwanamke kunyonyesha maeneo ya umma.

Aidha, baadhi yao wamekuwa na imani potofu kuhusu suala zima la kunyonyesha na faida zake. Hili limechangia pakubwa katika kudhoofisha jitihada za kuhakikisha kila mama mwenye mtoto mchanga anamyonyesha ipasavyo.

**BAADHI YA IMANI POTOFU KUHUSU KUNYONYESHA**

Yapo baadhi ya makabila ya Afrika na Tanzania yanayoamini kuwa maziwa ya kwanza ya mama si mazuri ni machafu humdhuru mtoto hivyo yanapaswa kumwagwa. Wengine huamini kuwa kumnyonyesha pekee hayawezi kumshibisha mtoto wa umri wa miezi sifuri hadi sita.

Yapo makabila yanayoamini kuwa ni lazima mtoto mchanga anywe maji mara baada ya kuzaliwa,kwani maziwa ya mama humfanya mtoto ajihisi mwenye kiu. Shirika la watoto la Save the Children linasema kuwa watoto wenye utapiamlo unaochangiwa na kutonyonyeshwa ipasavyo unakadiriwa kusabisha vifo vya watoto 2.7 kila mwaka.

Katika maelezo yanayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu unyonyeshaji watoto, faida mojawapo ni kuwawezesha kuwa na kinga ya magonjwa ya binadamu. Lakini iwapo watapewa maziwa ya ng'ombe wanakuwa na kinga ya maradhi ya wanyama. Lakini hakuna tija kumpa mtoto maziwa ya kiwandani au ya kopo kwa vile hayamkingi na magonjwa ya wany





# Waomba serikali kutatua mgogoro wakulima, wafugaji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kijiji cha Itamboleo katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuingilia kati na kutatua mgogoro wa mipaka baina yao na wafugaji wa jamii ya Kimasai kwa madai kuwa mgogoro huo unawakosesha amani.

Walitoa kilio hicho juzi walipokuwa wanazungumza kijijini hapo kwa madai kwamba mgogoro huo umedumu kwa muda mrefu hali ambayo inaweza ikasababisha mapigano baina yao.

Mmoja wa wananchi hao, Juma Mzee, alisema kwa muda mrefu wafugaji hao wa jamii ya Kimasai wamekuwa wakichungia mifugo yao kwenye mazao ya wakulima hali ambayo inawasababishia hasara kubwa.

Alisema wakati mwingine wakijaribu kuwahoji au kuiondoa mifugo hiyo kwenye mashamba, wanashambuliwa na vijana wanaochunga mifugo hiyo hali inayopelekea mgogoro baina yao kutoisha.

"Wafugaji wana eneo lao huko matebete lakini kutokana na mipaka kutoeleweka vizuri kati yetu na wao, ndio maana huwa tunaingia kwenye migogoro, baadhi ya mashamba yetu huwa hatuambulii kitu kabisa," alisema Mzee.

Alisema katika kijiji chao wengi ni wakulima wa mahindi na mihogo lakini wanapata hasara kubwa kutokana na mifugo hiyo.

Alisema mgogoro huo ulianza baada ya Wamasai hao kupewa eneo la iliyokuwa ranchi ya serikali ili waliendeleze na kwamba baadhi ya mipaka inaingia kwenye mashamba ya wakulima.

Kwa upande wao wafugaji wa Matebete walikiri kuwepo kwa mzozo wa muda mrefu baina yao ambao wakati mwingine umekuwa ukisababisha mapigano miongoni mwa jamii hizo.

Katibu wa ranchi ya Matebete, Leteo Kisota, alisema serikali ilishamaliza mgogoro huo kwa kuwakabidhi eneo lote la ranchi lakini bado wakulima wamekuwa wakiwaingilia bila kuheshimu mipaka iliyoainishwa kwenye hati miliki.

Alisema wao hawana tatizo na wenzao hao na wanapenda amani lakini wamekuwa wakichokozwa na majirani zao ambao hawapendi amani na upendo.

"Wale ni wenzetu na tunapenda tuishi kwa amani na kushirikiana kwenye shughuli zetu, lakini hawa wenzetu ni wakorofi na wao ndio wanakuwa wa kwanza kulalamika, wanaingia kwenye mipaka ambayo sisi tumemilikishwa kisheria," alisema Kisota.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Itamboleo, Samwel Kaganga, alisema walishafikisha kilio chao kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, ambaye aliwaahidi kuwa ataushughulikia mgogoro huo na kuumaliza kabisa.

Alisema waliahidiwa kuwa vitafanyika vipimo vya mipaka ili kubaini mipaka halisi na kwamba baada ya hapo pande zote zitakaa na kukubaliana kuheshimu mipaka hiyo.

# Wapewa mchongo kuuza mazao nje

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WANANCHI wa Halmashauri ya Busokelo katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameshauriwa kuchangamkia fursa ya kuuza mahindi nje ya nchi kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ili wanufaike na kilimo chao.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mbunge wa Busokelo, Fredy Mwakibete, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu maendeleo ya miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali katika halmashauri hiyo ambayo ni changa.

Mwakibete alisema kwa sasa serikali imewaruhusu wakulima na wafanyabiashara kuuza mazao yao katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Botswana, Zimbabwe na baadhi ya nchi jirani.

Alisema kinachotakiwa kwa mtu yeyote anayetaka kuuza mazao hayo ni kuiarifu serikali kabla ya kufanya hivyo ili apate kibali maalumu cha kusafirisha mazao hayo.

Aliwashauri wafanyabiashara na wakulima wenye mitaji midogo katika jimbo lake inayoweza kuwawezesha kuuza mazao nje ya nchi, kuuza zao hilo NFRA ili wao ndio wafanye hivyo.

Mwakibete alisema wakazi wengi wa Busokelo ni wakulima wa mazao mbalimbali yakiwamo mahindi na viazi na kwamba kwa sasa kuna masoko ya uhakika ya kuuza mazao yao, hivyo miongoni mwa fursa walizo nazo kwa sasa ni kuchangamkia soko kwenye mataifa yaliyoainishwa.

"Wafanyabiashara na wakulima wakubwa ndio wenye uwezo wa kuuza mahindi nje ya nchi kwa sababu wana mitaji mikubwa, hivyo nikiwa mwakilishi wa wananchi, lazima niwashauri njia rahisi ya kunufaika na kilimo chao," alisema Mwakibete.

Alisisitiza kuwa mfumo wa wakulima wadogo kuuza mahindi kupitia NFRA unawasaidia kuongeza tija kwenye kilimo chao kwa maelezo kuwa bei inakuwa nzuri kuliko za mitaani ambako kumejaa walanguzi.

Akizungumzia upatikanaji wa huduma ya afya katika jimbo hilo, Mwakibete alisema katika mwaka wa fedha 2019/2020 serikali imeongeza Sh. milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Alisema awali walipokea Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi huo na kwamba wanatarajia kuendelea kuboresha miundombinu ya hospitali hiyo kila wakati kadri watakavyokuwa wakipata fedha.

"Katika halmashauri yetu tumekamilisha vituo vitatu vya afya. Tunaendelea na ujenzi wa vituo vingine na zahanati kwa kutumia nguvu za wananchi na serikali inamalizia ili kuimarisha huduma za afya katika halmashauri yetu," alisema Mwaki Alisema wananchi katika halmashauri hiyo wamehamasika kwa kiasi kikubwa kushiriki shughuli za maendeleo hasa ujenzi wa miundombinu ya afya kutokana na adha waliyokuwa wanaipata awali.



Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya (Mbeya- WSSA), Mhandisi Simon Shauri (kushoto), akimkabidhi baadhi ya nyaraka Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo (kulia), katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Dk. Lwitiko Mwakalukwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Saccos yaingia mfumo kidigitali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Mwanjelwa (Mwanjelwa – Saccos) cha jijini Mbeya, umesema chama hicho kimeingia kwenye mfumo wa kidigitali ambao unawawezesha wanachama na wateja wake kuhudumiwa hata wakiwa nyumbani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama hicho, Anyingisye Mwangoge, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu maendeleo ya chama hicho na kwamba wamefikia hatua hiyo ili kuendana na wakati.

Alisema kwa sasa kuna maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, hivyo hata wao wanapambana kwa kila namna ili kuhakikisha wanaendana na maendeleo hayo kisha kufikia hatua ya kuwa taasisi kubwa ya kifedha. "Kwa kutumia mfumo huu, mwanachama wetu ana uwezo wa kuomba mkopo na akapata. Anaweza pia kuangalia salio la akiba yake akiwa popote. Si lazima aje ofisini ndiyo ahudumiwe," alisema Mwangoge.


Kuhusu historia ya chama hicho, Mwangoge alisema kilianza mwaka 2003 kikiwa na wanachama 34, lakini baadaye kilishindwa kujiendesha baada ya ofisi yake kuungua moto wakati soko la Mwanjelwa lilipoungua mwaka 2006.

Alisema walianza upya mwaka 2007 na kuendelea mpaka sasa na kinajiendesha kwa faida na kwamba wamepata mafanikio makubwa ikiwamo kuongeza wanachama kutoka 34 wa wakati huo mpaka 513 wa sasa. Pia alisema wakati chama hicho kinaanzishwa, kilikuwa na mtaji wa Sh. 375,000 lakini kwa sasa kina mtaji wa zaidi ya Sh. milioni 376.6 huku kikiwa kimeshakopesha zaidi ya Sh. bilioni 3.7.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho, Deo Mwamakula, alisema kwa sasa chama kinajitegemea kwa mtaji na hakitegemei kupata mikopo kutoka taasisi zingine za kifedha.

Alisema mpaka sasa wanamiliki jengo ambalo walilinunua kwa Sh. milioni 24 ambalo kwa sasa linatumika kama kitega uchumi na wamesaidia kujenga ofisi za baadhi ya watendaji wa mitaa ndani ya Kata ya Maanga jijini Mbeya.

Pamoja na mafanikio hayo, alisema chama kinakabiliwa na baadhi ya wanachama kushindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati hali inayokwamisha shughuli za chama.





## Madarasa 160 yapungua shule za msingi Kibaigwa

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WAKAZI wa Mji Mdogo wa Kibaigwa wilayani Kongwa mkoani Dodoma, wamewaomba wadau kuwasaidia kukabiliana na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa 160, ulipo katika shule za msingi.

Ombi hilo lilitolewa na Diwani wa Kata ya Kibaigwa, Richard Kapinye, wakati wa uzinduzi wa mnara wa mawasiliano wa 4G, wa kampuni ya simu za mkononi ya Tigo iliyofanyika katika mji mdogo wa Kibaigwa jana.

Kapinye alisema mji huo unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa zaidi ya 160 katika shule tano za msingi zilizopo katika mji huo.

"Tunawashukuru kwa kutusaidia kwenye mawasiliano, lakini naomba nitoe kilio kingine tulichonacho wananchi wa eneo hili la Kibaigwa, tunazo shule, lakini zimejaa wanafunzi tunahitaji msaada wa ujenzi wa vyumba zaidi vya madarasa," alisema.

Alibainisha kuwa kila shule iliyopo katika eneo hilo imebeba idadi ya wanafunzi wa shule mbili kutokana na kila shule kuwa na wanafunzi zaidi ya 2,000.

Kapinye aliongeza kuwa wananchi wa eneo hilo wamejaribu kuchangishana na kufanikiwa kujenga baadhi ya vyumba, lakini bado inahitajika nguvu zaidi ya wadau wengine kujitokeza kusaidia.

Aliitaja changamoto nyingine inayowakabili wakazi wa eneo hilo kuwa ni maji kutokana na ongezeko kubwa la watu wanaohamia katika mji huo na hasa eneo la Ndulugumi ambalo halina huduma hiyo.

Meneja wa Tigo Mkoa wa Dodoma, Gidion Morris, alisema kampuni hiyo ina wateja zaidi ya 600,000 na mawakala zaidi ya 6,000 wanaotoa huduma za Tigopesa pamoja na huduma nyingine za simu.

Morris alisema, baada ya kampuni hiyo jana kuzindua mnara wa huduma ya mawasiliano wa 4G, katika Wilaya za Kongwa, kwa sasa huduma hiyo inapatikana katika wilaya za Dodoma mjini, Chamwino, Kondoa na hivi karibuni wanategemea kuzindua huduma hiyo wilayani Mpwapwa.

Mkurungenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini inayojumuisha mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro, Manyara, Arusha na Kilimanjaro, Aidan Komba, alisema wamezindua huduma hiyo ili kuwasaidia wananchi na wakulima hao kupata huduma ya intaneti yenye kasi.

"Hapa kuna wakulima wakubwa na wafanyabiashara wa mazao hivyo huduma hii itawasaidia kufanya mawasiliano yenye ubora zaidi," alisema.

Hata hivyo, kuhusu changamoto hizo aliwashauri wananchi hao kufuata utaratibu wa kuandika barua makao makuu ya kampuni, ili kuangalia uwezekano wa kusaidiwa katika eneo mojawapo.

# Chamwino yaomba shamba la zabibu Chinangali II

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

KUTOKANA na wakulima kushindwa kuendesha mradi wa shamba la zabibu la Chinangali II lililopo Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Halmashauri ya Wilaya hiyo imeomba kuuchukua mradi huo ili kuunusuru kutokana na kusuasua uendeshaji wake.

Wakulima ambao wanamiliki mradi huo wenye ekari 290 wameshindwa kuuendesha kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo madeni.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Athuman Masasi, alitoa ombi hilo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, katika shamba hilo ambapo uamuzi huo utawezesha halmashauri kulipa deni lililopo baina ya wakulima na benki ya CRDB la kiasi cha Sh. bilioni 2.7 ambazo zilikuwa zikiongezeka kila mwaka kutokana na riba.

Masasi alisema halmashauri hiyo itakapolichukua shamba hilo inakusudia kulipanua na kufikia ekari 1,250.

"Mradi huu tunataka uwe wa kimkakati badala ya kujenga soko au stendi, tunafanya hivi ili tuweze kuuendesha na kupunguza deni lililopo, lengo letu sio kuwanyang'anya au kuwaondoa wananchi kwenye umiliki wao bali ni kusaidia katika uendeshaji na usimamizi," alisema Mkurugenzi.

Alisema mradi huo ukisimamiwa vizuri una uwezo wa kuingiza mapato ya Sh. bilioni tatu hadi nne kwa mwaka na hivyo kuongeza mapato ya halmashauri.

Awali, akitoa maelezo ya mradi huo, Ofisa Kilimo wilaya hiyo, Godfrey Mnyamale, alisema shamba hilo lina ukubwa wa ekari 1,250 likiwa na wamiliki na kuomba kubadilishwa kwa mfumo wa uendeshaji kutoka kwa mtu mmoja kwenda wa pamoja ili kuongeza uzalishaji.

"Sasa changamoto tunayopata ni kipindi cha kupuliza dawa baadhi ya wakulima hawapulizi na hivyo kuleta madhara kwa wakulima wengine pale wanapotokea wadudu waharibifu wa mazao," alisema.

Akijibu ombi hilo, Dk. Mahenge aliiagiza halmashauri hiyo kuwasilisha kwake Jumatatu ijayo mapendekezo ya kitaalamu ya kufufua mradi wa shamba hilo ili uweze kuwa na tija. Alisisitiza kuwa ni lazima deni lililopo lilipwe na kuwataka wakulima wa shamba hilo kujituma na kulima kwa moyo huku wakifuata maelekezo ya wataalamu ili wapate wanachotarajiwa.



Mjasiriamali wa biashara za majiko, Paulo Venance mkazi wa Kibaigwa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, akimwonyesha mteja wake Issa Abdalah majiko hayo, kama walivyokutwa eneo hilo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakiwa kutumia Tehama kwa changamoto ya ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kuzitumia fursa zilizopo kupitia ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa ajira ambayo imekuwa ikiongezeka kila siku duniani.

Rai hiyo ilitolewa jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Twaweza, Aidan Eyakuze, katika kongamano la changamoto na fursa zilizopo katika mfumo wa kidijitali ili kuyafikia masoko pamoja na kazi zenye staha kwa vijana.

Akizungumza katika kongamano hilo lililoandaliwa na Shirika linalojihusisha masuala ya vijana (YPC), Eyakuze alisema kuwa kupitia dijitali vijana wanaweza kuitumia mitandao ya kijamii katika kuzalisha huduma mpya ambazo zitatumika katika jamii ili wao kujipatia kipato.

"Kupitia mitandao ya kijamii vijana wana uwezo wa kutengeneza bidhaa na kuzitangaza kupitia mfumo wa teknolojia iliyopo, lakini pia vijana wanaweza kubuni nyimbo, sinema na kuziweka katika 'U tube' na kuwafikia watu zaidi ya milioni nne kwa muda mchache na wao kujipatia kipato," alisema Eyakuze. Pia alisema changamoto iliyopo kwa vijana hivi sasa ni mfumo wa elimu nchini ambao umekuwa ukiwaandaa kuwa na wazo la kufanya kitu kimoja pekee ambacho wamekisomea darasani.

"Dijitali inatutaka kuwa wabunifu zaidi ya mipaka yetu ya kazi tuliyoisomea unaweza kuwa na mtaji mdogo, lakini kupitia dijitali ukajitangaza biashara yako ikakuwa zaidi, ni vizuri tukawa na mawazo mapana zaidi ya kile tulicho kisomea," alisema.

Vile vile alisema ipo haja ya serikali kuona namna ya kuongeza kitu katika mitaala ya elimu nchini ili kuwezesha vijana kuwa na ubunifu pamoja na kuthubutu katika masuala ya ujasiriamali.

Alisema kwa namna ambavyo teknolojia inakuwa hivi sasa duniani kazi nyingi zipo hatarini kuchukuliwa na mashine (roboti).


Eyakuze alisema zipo baadhi ya tafiti ambazo zimefanywa na watafiti mbalimbali duniani zikionyesha kuwa katika miaka 20 ijayo kazi nyingi zitachukuliwa na mashine, lakini pia patakuwapo na kazi nyingi mpya.

"Ni wakati sasa kuanza kujiandaa kuwa wabunifu kwa kuwa inasemekana kazi nyingi ambazo zina fomula zipo mbioni kuondoka kwa watu na kuchukuliwa na mashine katika miaka ijayo," alisema.

Naye, Ofisa Maendeleo ya Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu Godfrey Chacha, alisema kongamano hilo limekuwa muhimu hasa katika wakati huu ambao Tehama imekuwa kila kitu katika maisha.

Alisema serikali inahamasisha vijana kutumia Tehama katika kutafuta masoko, pia kujipatia ajira.

Chacha alisema katika kuhakikisha kuwa taifa linafikia uchumi wa viwanda matumizi ya Tehama, hayakwepeki kwa kuwa ndiyo sehemu pekee inayoweza kutoa majibu ya changamoto zilizopo nchini.





Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, akipata maelezo kutoka kwa Meneja Masoko wa Kampuni ya Tropical inayotengeneza vifaa vya umeme katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# IES kushirikiana na SMZ upanuzi wa gati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya kimataifa ya uhandisi wa mtandao wa viwanda ya nchini Misri (I E S), imejitolea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika upanuzi wa ujenzi wa gati ya Malindi ili Unguja iendelee kutoa huduma za uteremshaji na upakiaji wa mizigo kwa uhakika.

Timu ya wataalamu watano wa tawi la kampuni hiyo inayojishughulisha na masuala ya uhandisi wa umeme iliyopo Afrika Mashariki ikiongozwa na Mhandisi Ibrahim Qamar, ilisema hayo wakati wa mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, Vuga mjini hapa.

Mhandisi Ibrahim Qamar, alisema uongozi wa kampuni hiyo umeridhika na harakati za uchumi na biashara Zanzibar zinazohudumiwa na bandari hiyo ambayo kwa sasa inahitaji kuongezewa nguvu za upanuzi ili itoe huduma zilizo bora zaidi.

Alisema Zanzibar ni kituo cha biashara cha kimataifa kinachoendelea kuyaunganisha mataifa mengi yaliyomo ndani ya ukanda wa Bahari ya Hindi kwa masuala ya biashara kwa karne kadhaa zilizopita ambacho kwa sasa kinastahiki kurejeshewa hadhi yake ya asili.

Mhandisi Ibrahim alisema kutokana na umuhimu mkubwa wa Bandari ya Malindi Zanzibar katika utoaji wa huduma zake, uongozi wa kampuni yake umeshajitolea katika harakati za utanuzi huo muda wowote kuanzia sasa endapo utapatiwa fursa hiyo adhimu.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Iddi, alisema ni vyema ukaandaliwa utaratibu maalum kwa wahandisi wao kukutanishwa na wataalamu wazalendo ili kulifanyia kazi suala hilo muhimu.

Balozi Iddi alisema mkutano huo wa pamoja utawezesha kuangalia njia za kufanya utafiti utakaotoa jibu la namna bandari hiyo inavyoweza kushughulikiwa katika upanuzi wake.

Kampuni ya IES iliyoasisiwa mwaka 1938 imekuwa ikitoa huduma katika mataifa mbalimbali barani Afrika pamoja na Mashariki ya Kati ikishirikiana pia kwa kuingia ubia miradi tofauti na kampuni kadhaa ulimwenguni.

Wakati huo huo, Balozi Iddi alikutana kwa mazungumzo na ujumbe wa viongozi wa wafanyabiashara kutoka Jimbo la Shadong, nchini China ukiongozwa na Meya wa Manispaa ya Mji wa Jimbo hilo Zhaogang Wang.

Katika mazungumzo yao Balozi Iddi alisema Zanzibar bado ina fursa nyingi za uwekezaji na kutoa mfano wa sekta viwanda, utalii, mawasiliano na biashara, lakini mtazamo wa sasa ni kuona eneo la uvuvi wa Bahari Kuu linapewa msukumo kama ilivyopewa sekta ya utalii.

Alisema Zanzibar imezungukwa na bahari sehemu zote mazingira ambayo wawekezaji wa Jimbo la Shadong wanaweza kuitumia fursa hiyo kwa masuala ya uwekezaji kwa vile nchi hiyo tayari imeshapiga hatua kubwa katika kuimarisha uvuvi wa Bahari Kuu.

Meya wa Manispaa ya Jimbo la Shadong, Zhaogang Wang, alisema China imefanya mabadiliko katika sekta zake za uwekezaji kwa kuwaruhusu wafanyabiashara binafsi kuzitumia fursa hizo katika mataifa mbalimbali duniani.

Wang alisema ipo miradi ambayo wawekezaji wa jimbo hilo wameshaipanga katika mfumo wa ubia na taasisi tofauti duniani zikiwamo nchi za Bara la Afrika katika sekta za uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na kilimo cha kisasa.

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Balozi Amina Salum Ali, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeshatiliana saini mkataba wa ushirikiano kati yake na uongozi wa jimbo hilo katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Balozi Amina alisema miongoni mwa maeneo yaliyoguswa katika mkataba huo ni pamoja na ushirikiano wa pamoja katika mbinu za utunzaji wa mazingira kwenye mji wa Rosha, jimboni Shadong na Zanzibar.

# Vijana wa CCM vyuo vikuu wapewa somo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Amin Salmin Amour, amewataka vijana wa CCM wanaosoma vyuo vikuu nchini kutokubali kutumiwa kisiasa na baadhi ya viongozi wanaoweka mbele maslahi binafsi kuliko ya chama.

Aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya uongozi kwa vijana wa Idara ya vyuo na vyuo vikuu vya UVCCM Zanzibar, Jimbo la Jang'ombe Matarumbeta, Unguja.

Alisema kuna baadhi ya viongozi wamekuwa na tabia ya kuwatumia vijana katika mambo yao binafsi yanayohatarisha uhai wa chama, hivyo aliwaasa kuepuka kuingizwa katika makundi yasiyofaa.

Alieleza kuwa endapo vijana watafuata miongozo na kanuni za UVCCM na CCM, wataendelea kuwa msaada mkubwa wa kuivusha CCM katika masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Alisema maendeleo ya taifa lolote duniani yanaletwa na vijana wasomi na wenye ujuzi wa fani mbalimbali zinazochochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi husika.

Amin aliwasihi vijana hao kuhamasisha wenzao waliopo mitaani na wa vyama vya upinzani wajiunge na CCM ili kuongeza jeshi la kufanikisha ushindi wa 2020.

Akizungumzia hafla hiyo, aliwapongeza vijana hao kwa kukubali kupewa mafunzo hayo ya uongozi na itikadi kwa kuwa wamejifunza mambo mbalimbali yenye tija yanayowajengea kujiamini katika safari yao ya kielimu.

"Chama Cha Mapinduzi na serikali zake wamewaamini vijana kwa kuwapatia fursa za uongozi na utendaji hivyo nanyi mnatakiwa kufanya kazi kwa bidii na kuwa waaminifu ili kulinda heshima hiyo," alisema Amin.

Aliongeza kwamba vijana wanapopewa dhamana ya uongozi wajitahidi kuliwakilisha vyema kundi hilo ili kujenga matumaini kwa jamii.

Mwenyekiti wa idara hiyo, Masoud Shibli, alisema Idara ya vyuo na vyuo vikuu kwa upande wa Zanzibar imekuwa ni kitovu cha kutoa mafunzo mbalimbali kwa vijana wake ili wawe na uthubutu wa kujiamini kwa kukitumikia Chama Cha Mapinduzi kwa uadilifu zaidi.

Awali akitoa taarifa ya mafunzo hayo, Katibu wa Idara ya vyuo vikuu, William Dikson, alisema zaidi ya vijana 300 wamepatiwa mafunzo hayo yenye lengo la kuwajengea uwezo wa masuala ya uongozi.

# Polisi yamchunguza anayedaiwa kutumikisha kingono wasichana 6

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limesema kuwa linaendelea na uchunguzi kuhusu tuhuma zinazomkabili mfanyabiashara wa vileo, Salome John, mkazi wa Kizimkazi Unguja anayetuhumiwa kuwatumikisha wasichana katika biashara ya ngono.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kuwatumikisha kingono wasichana sita, ambao walifika Kituo cha Polisi Makunduchi, kumlalamikia mfanyabiashara huyo anayedaiwa kwenda kinyume na makubaliano yao.

Wasichana hao wanadaiwa kutolewa Tanzania Bara na mfanyabiashara huyo kwa lengo la kufanya biashara ambayo inakubalika kisheria katika baa yake huko Kizimkazi na sio kuuza miili yao.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Hassan, alisema Jeshi la Polisi litakapokamilisha uchunguzi wa kesi hiyo, linatarajia kuwasilisha jalada kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili mtuhumiwa huyo aweze kufikishwa mahakamani.

Alisema kufanya biashara ya ngono ni kinyume na sheria ya makosa ya jinai hivyo upelelezi wa kesi hiyo utakapokamilika mtuhumiwa atashtakiwa kwa sheria hiyo.

Alieleza kuwa hivi sasa mtuhumiwa huyo amepewa dhamana na atatakiwa kuripoti polisi kila atakapohitajika.

"Ingawa mtuhumiwa huyo kwa sasa hayupo Kizimkazi kama alivyotoa agizo Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja kuwa aondoke katika kijiji hicho, lakini kutokuwapo kwake si kwamba Jeshi la Polisi litashindwa kufanya kazi yake ya kuchunguza kesi hiyo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Idrisa Mustafa Kitwana, alisema kitendo cha kumhamisha mfanyabiashara huyo katika Kijiji cha Kizimkazi hakikuhusisha dini, wala sehemu anayotoka bali ni kukiuka taratibu zilizowekwa za kibali alichopewa cha kufanya biashara yake na kuwalazimisha wafanyakazi wake kufanya biashara ya ngono bila ya wenyewe kuridhia.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu kuwapo kwa taarifa ya kuwa alimfukuza mfanyabiashara huyo Zanzibar, alisema yeye hakuwa na uwezo wa kumfukuza Zanzibar kwa kuwa anafahamu kuwa Katiba ya Zanzibar inaruhusu Mtanzania akae popote anapotaka ikiwa atafuata sheria za nchi aliyopo.

# Majaliwa akaribisha Wamisri uwekezaji viwanda vya ngozi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Misri ikiwamo kampuni ya Cairo for Investment and Development inayoshughulika na usimamizi wa kiwanda cha ngozi waje kuwekeza nchini.

Alitoa rai hiyo juzi alipotembelea kiwanda kikubwa cha ngozi cha Robbiki kilichoko katika mkoa wa Sharkia nchini Misri, hivyo kutumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji hao waje wawekeze nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha.

Waziri Mkuu ambaye jana alikuwa katika siku ya pili ya ziara yake ya kikazi nchini Misri, alisema Tanzania ina mifugo mingi, hivyo inahitaji wawekezaji watakaojenga viwanda vya kuchakata bidhaa mbalimbali zitokanazo na mifugo hiyo, ikiwamo ngozi.

Alisema Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais John Magufuli imeboresha mazingira ya biashara na ya uwekezaji pamoja na kusimamia uwajibikaji kwa watumishi wa umma, hivyo Tanzania ni mahali bora na salama kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kampuni ya Cairo for Investment and Development, ambayo inasimamia kiwanda cha ngozi cha Robbiki, Yasser Mohamed Ahmed Al Maghraby, alisema kiwanda hicho kina uhitaji mkubwa wa ngozi kutoka Tanzania.

Awali, Waziri Mkuu alitembelea mradi mkubwa wa mabwawa ya kufugia samaki, mradi wa upanuzi wa awamu ya pili ya mfereji wa Suez Canal, ambapo aliipongeza Serikali ya Misri kwa ujenzi wa mradi huo mkubwa kwa kutumia fedha za ndani (Dola bilioni 8.2).



Mkurugenzi wa 'M-Commerce' Vodacom Tanzania (wa pili kushoto), Epimarck Mbeteni, Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Herieth Lwakatare na Mkurugenzi wa Wateja wa Mikataba (Business Enterprise Unit), Arjun Dhillon, wakishikana mikono na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Habari na Utekelezaji, Moses Manyatta, kuashiria uzinduzi wa huduma mpya ya M-Pesa Songesha. Wengine katika picha ni Mkurugenzi wa Masoko na Maendeleo ya Biashara, Deogratius Kwiyukwa (wa tatu kushoto) na Mkuu wa Matawi, Bonaventura Paul, kutoka Tanzania Postal Bank (TPB). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gesi asilia ya Tanzania yafagiliwa

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya kimataifa ya mafuta ya Shell, imesema kwamba gesi asilia ambayo imegunduliwa Tanzania ni maridhawa na ni tunu kwa Watanzania.

Taarifa ya kampuni hiyo ilitolewa baada ya mkutano wa wadau wa ndani na nje ya Tanzania wa sekta hiyo ambao ulifanyika jijini Dar es Salaam.

Imeueleza mkutano huo upekee wa mradi wa gesi (Tanzania LNG) wa Tanzania na uzito wake duniani.

Kampuni hiyo ikitumia uzoefu wake katika mradi wake wa Canada ambao kwa sehemu kubwa unafanana na mradi wa Tanzania, imesema mradi wa Tanzania utakuwa ni kati ya miradi nadra katika tasnia ya mafuta na gesi kwa sababu ya ubora wa gesi na uchache wa kaboni daiokisaidi (gesi mkaa).

Sheli ikishirikiana na wabia wake Ophiri Energy na Pavilion Energy katika muongo mmoja uliopita imechimba visima 22 vya uchunguzi na upembuzi na kupata gesi kubiki futi za gesi trilioni 23, na kutumia dola za Marekani bilioni mbili katika shughuli hiyo. Shell imesema haijutii uwekezaji huo.

Mabingwa na watendaji wa sekta hiyo walikutana Dar es Salaam kutokana na ukweli kwamba kidunia kwa sasa kampuni kubwa na wawekezaji wanaangalia namna ya kupambana na tabianchi kwa kujali mazingira na athari zake vimekuwa vigezo muhimu kwa kampuni yoyote na shughuli zake kukubalika katika jamii. Mchumi kiongozi wa Shell, Beatus Rwechungura, aliuambia mkutano huo kuwa gesi iliyogunduliwa Tanzania ni raslimali ya daraja la juu kwa kuwa ina kaboni kidogo mno ikilinganisha na miradi yote ya Shell kote dunia. "Kutokana na changamoto zinazotokana na tabianchi, hiki ni kigezo muhimu cha kupata ufanisi katika uendelezaji wa gesi asilia. Na ukweli huu ndiyo unaoufanya mradi wa Tanzania LNG kuwa na sifa za kipekee na kuufanya mradi huu uwe amana muhimu kwa Shell," alisema Rwechungura.

Meneja Mkazi wa Shell, Dirk Nevelsteen, ameuambia mkutano huo kuwa dunia inabadilika haraka sana, na kwamba nishati imekuwa ni kanuni ama sifa inayotumiwa kama msingi wa kutolea maamuzi. Amesema maisha ya watu na vipato vyao, chumi za mataifa na jamii vinategemea nishati yenye kuaminika na isiyokuwa na adha na ambayo watumiaji wanaimudu ili kuinua maisha yao.

"Kuna haja ya kuangalia kwa makini masuala ya mazingira, hasa tabia nchi, umuhimu wake ni mkubwa mno wakati huu," aliwaambia wajumbe wa mkutano huo.

Shell imekumbusha kwamba ifikapo 2070 dunia itakuwa inahitaji walau asilimia 50 zaidi ya nishati inayohitajika wakati huu duniani. Umoja wa Mataifa unakadiria kuwa mwaka 2050 dunia itakuwa na watu bilioni 9.7 kutoka bilioni 7.6 za sasa.

Tanzania ina watu takribani milioni 54.2 kwa sasa, na inakadiriwa itakuwa na watu milioni 77.5 ifikapo 2030, kwa hiyo mahitaji ya nishati yanapaswa kufiriwa sana kuanzia sasa.

# Wazee wapata ukombozi afya

**Na Christina Haule**, MOROGORO

JUMLA ya kaya za wazee 10 katika Kata ya Ngerengere wilayani Morogoro mkoani hapa, zimekabidhiwa kadi za Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa bure ili kupata huduma ya matibabu na dawa kwa wepesi.

Akipokea kadi hizo mmoja wa wazee hao, Saidi Tanganyika (71), mkazi wa kijiji cha Ngerengere, aliipongeza serikali kupitia mradi wa Tuimarishe Afya (HPSS) unaofadhiliwa na Serikali ya Uswisi kwa kuwapatia kadi hizo kwa kuwa zinazotolewa kwa gharama kubwa ambayo kwao ingekuwa shida kuimudu.

Tanganyika alisema wamepokea kadi hizo kama mkombozi wa maisha yao, kwa kuwa awali walipata matibabu kwa shida kutokana na kutokuwa na uwezo wa kugharamia matibabu wala kupata kadi hizo.

Naye Haruna Mohamed (80), mkazi wa Ngerengere, alisema watapata huduma ya matibabu na dawa kwa urahisi kutokana na kadi za sasa kuboreshwa tofauti na za awali.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Kebwe Steven Kebwe, aliwashauri wakulima kukitumia vyema kipindi cha mavuno katika kupata kadi za CHF kwa sababu ndio mkombozi katika maisha yao.

Meneja wa HPSS, Dk. Haruni Machibya, aliitaka jamii kuhamasika na kujiunga kwenye CHF kwa kuwa ugonjwa haupigi hodi ili mtu ajiandae.

# Umuonapo mtoto huyu toa taarifa



**Na Mwandishi Wetu**

MUSLIM Abdalah (13) mwanafunzi wa darasa la sita, Shule ya Msingi Mwakidila Tanga, mwenye tatizo la akili anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka na kwenda kusikojulikana.

Mama mdogo wa mwanafunzi huyo, Mwantumu Hussein, alisema alitoweka juzi majira ya saa tano asubuhi nyumbani kwa dada yake, Tegeta A, jijini Dar es Salaam.

"Aliletwa Julai 7, mwaka huu kwa ajili ya kupata matibabu, lakini kesho yake akatoweka, hatujui aliko na tumetoa taarifa polisi na kufungua jalada namba GB/RB/1639/2019," alisema Mwantumu.

Mwantumu amewaomba wasamaria wema watakaomuona mwanafunzi huyo atoe taarifa kituo cha polisi na pia kuwasiliana nao kwa simu namba **0713-318120 au 0712-249139.**

HABARI KIMATAIFA

# Rais Trump amng'oa balozi wa Uingereza

**NEWYORK,** Marekani

BALOZI wa Uingereza nchini Marekani, Sir Kim Darroch, amejiuzulu yakiwa ni matokeo ya kuvuja kwa barua pepe zinazoukosoa utawala wa Rais wa Marekani, Donald Trump.

Balozi huyo, aliitwa "mtu mpumbavu" na Rais Trump, baada ya barua pepe hizo zilizovuja kusema kuwa utawala wa Trump si stadi".

Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani imesifu hatua hiyo ya Balozi Darroch Kim ikiuita ni ya weledi mkubwa.

**Anataka kumaliza mzozo uliokuwapo na kuongeza kuwa kuvuja kwa barua pepe kumefanya utendaji kazi wake kuwa 'mgumu'.**

Balozi huyo amesema anataka kumaliza mzozo uliokuwapo na kuongeza kuwa kuvuja kwa barua pepe kumefanya utendaji kazi wake kuwa 'mgumu'.

Balozi Kim katika barua pepe zilizofichuliwa siku ya Jumapili aliutaja utawala wa Rais Trump kama usiofanya kazi na usiojielewa. Awali Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, alisema kuwa ana imani na Balozi Darroch Kim, lakini hakubaliani naye.

Katika matamshi yake kwenye mtandao wa Twitter Rais Trump pia alimshutumu Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May akisema kuwa "ni habari njema kwamba Uingereza itapata Waziri Mkuu mpya".

Theresa May alijiuzulu baada ya kukosa kuungwa mkono na bunge kuhusu mpango wake wa Brexit na chama tawala sasa kitalazimika kuchagua kati ya mgombea Boris Johnson au Jeremy Hunt kuchukua nafasi yake. **BBC**



Gari la kivita aina ya Bradley Fighting Vehicles la Marekani likiingia katika Uwanja wa Kumbukumbu wa Lincoln Memorial kwa ajili ya maandalizi ya salamu za Rais wa Marekani, Donald Trump kwa taifa, Siku ya Uhuru wa Marekani Alhamisi iliyopita. **PICHA: BBC**

## Huduma intaneti zarejea Sudan

**KARTOUM,** Sudan

HUDUMA za intaneti ya simu za mkononi zimerejeshwa tena nchini Sudan jana, kufuatia amri ya mahakama wiki kadhaa, baada ya watawala wa kijeshi kuzizuwia wakati wa operesheni ya ukandamizaji dhidi ya waandamanaji.

Wakili Abdelazim al-Hassan, amesema mahakama ya mjini Khartoum iliziamuru kampuni za mawasiliano ya simu za mkononi kurejesha huduma hizo.

Baraza la Kijeshi lilitetea hatua ya kuzima huduma hizo kwa kusema kuwa mitandao ya kijamii ilitoa kitisho kwa usalama wa taifa. Wateja wa kampuni za simu za Zain, MTN na Sudan, wamethibitisha kurejea kwa huduma za intaneti kwenye simu zao za mkononi.

Nchi ya Sudan imeingia kwenye matatizo ya kisiasa tangu majenerali walipomwondoa Rais wa muda mrefu, Omar Al-Bashir, kwa njia ya mapinduzi Aprili kufuatia miezi kadhaa ya maandamano ya umma nchi nzima.

Hivi karibuni, Wizara ya Mambo ya Nje Marekani ilitoa wito wa kukuza kile inachokiita baraza la uhuru lenye mzunguko wa madaraka kwa nafasi ya rais kutoka upande wa jeshi na kiraia kwa miaka mitatu.

Marekani ilisema inaukaribisha mkataba wa kushirikiana madaraka uliobuniwa kumaliza miezi kadhaa ya ghasia za kisiasa nchini Sudan. Mkataba huo uliafikiwa Ijumaa iliyopita kati ya viongozi wanaoandaa maandamano na majenerali wanaotawala nchi baada ya kufanyika mazungumzo ya siku mbili. **DW**

## Udhalilishaji watoto wamponza ofisa UN

**KATHMANDU,** Nepal

OFISA wa zamani wa Umoja wa Mataifa amefungwa jela nchini Nepal baada ya kukutwa na hatia ya udhalilishaji wa watoto.

Peter John Dalglish (62), raia wa Canada, alishikiliwa karibu na mji wa Kathmandu nchini Nepal mwaka 2018 na kuhukumiwa mwezi uliopita.

Alihukumiwa kifungo cha miaka tisa kwa kumdhalilisha mtoto wa kiume wa miaka 12 na kifungo cha miaka saba kwa kumdhalilisha kingono mtoto wa miaka 14.

Dalglish, alikuwa ofisa wa juu wa masuala ya kibinadamu tangu miaka 1980, alikana mashtaka na wanasheria wake waliliambia shirika la habari la Reuters kuwa wangekata rufani.

Dalglish pia aliamriwa kulipa fidia kiasi cha pauni 3,600 kwa kila mtoto. Watoto hao walikuwa nyumbani mwa ofisa huyo alipokamatwa.

Hata hivyo, Jaji hajaamua kama Dalglish atatumikia kifungo cha miaka 16 kwa ujumla au aachiwe baada ya miaka tisa.

"Katika kesi za namna hiyo, hukumu hutumikiwa kwa pamoja lakini ni juu ya jaji kuamua," Ofisa wa Mahakama aliliambia AFP.**BBC**

## Sakata la Khashoggi laibuliwa upya

**INSTANBUL,** Uturuki

MAREKANI inapaswa kuchukua hatua kuhusu ripoti ya uchunguzi kuhusu kifo cha mwanahabari wa Saudi Arabia, Jamal Khashoggi, kilichotokea mwezi Oktoba mwaka jana, Ofisa wa Shirika la Umoja wa Mataifa ameeleza.

"Hawawezi kuchagua kunyamaza, wanapaswa kuzungumza, lakini haitoshi. Tunapaswa kuchukua hatua", amesema Agnes Callamard.

Uchunguzi ulihitimisha kuwa kifo cha Khashoggi kwenye ubalozi wa Saudi Arabia mjini Instanbul "ilikuwa ni mauaji ya kinyama".

Akizungumza akiwa pembeni mwa mchumba wa Khashoggi, Callamard ameitaka Marekani kukiri kutowajibika ipasavyo katika kuchukua hatua.

Ripoti ya Callamard ya kurasa 101, iliyochapishwa mwezi Juni, imesema kulikuwa na "ushahidi wa kuaminika" kuwa mwana mfalme Mohammed bin Salman na maofisa wengine wa juu wanawajibika kwa mauaji ya Jamal Khashoggi.

Vyombo vya usalama vya Saudia vinahusika na mauaji ya mwandishi huyo wa habari ndani ya ubalozi wa Saudia mjini Instabul, lakini mamlaka zinasisitiza walikuwa hawatekelezi amri za mtoto wa mfalme Mohammed.

Callamard ametoa wito kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, kuanzisha uchunguzi wa tukio hilo, lakini alisema nchi mwanachama pekee ina mamlaka ya kufanya hivyo.

Amesema nchi za magharibi hazijawajibiki kwa kusikiliza vilio vya watu kuhusu mauaji. **BBC**

## Mazungumzo yaanza Venezuela

**CARACAS,** Venezuela

SERIKALI ya Venezuela na upinzani wameanza tena mazungumzo yaliyositishwa kwa wiki kadhaa, yenye lengo la kukomesha mzozo wa kisiasa unaolikabili taifa hilo.

Wawakilishi wa pande zote mbili wamekutana katika kisiwa cha Karibiki cha Barbados kwa upatanishi wa serikali ya Norway.

Kiongozi wa upinzani, Juan Guaido, amethibitisha lengo la kile alichokiita kutafuta njia ya kutoka kwenye udikteta.

Rais Nicolas Maduro ameelezea matumaini baada ya duru ya kwanza ya mazungumzo hayo iliyodumu kwa saa tano.

Wanasiasa hao wawili hawakuhudhuria mkutano huo wa Barbados. Kwa miezi kadhaa wamekuwa katika mapambano makali ya kuwania madaraka katika taifa hilo la Amerika Kusini linalokabiliwa na mzozo. DW

# Rai wazazi kuendeleza vipaji vya watoto

**Mwandishi Wetu**

WAZAZI nchini wametakiwa kulea vipaji vya watoto wao kama sehemu ya kuwajengea uwezo na maarifa yatakayowawezesha kujiajiri na hatimaye kutoa mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya warsha ya kueleza nguvu ya vipaji au talanta (The Power of Talent), Mwanasheria na Mtunzi wa Mashairi, Aisha Kingu, alisema wazazi au walezi wana nafasi kubwa ya kukuza talanta za watoto wao.

"Nimeandaa warsha hii ili kwa pamoja tujadili namna nzuri ya kutambua na kuendeleza vipaji vya vijana ili viwe nyenzo muhimu katika kujiinua kiuchumi," alisema na kuongeza: "Hayo yote yanawezekana iwapo tu wazazi na walezi wataamua kwa dhati kuunga mkono talanta za vijana na kuwafanya watimize ndoto zao za kimaisha."

Mmoja ya washiriki, Dk. Kingu Mtemi, alitoa ushuhuda wa wazazi kuendeleza talanta za watoto na kufafanua tabu inayoambatana na ulezi wa aina hiyo. "Sisi wazazi mwanzoni tulikuwa na wakati mgumu kwani tuliamini binti yetu angekuwa daktari. Lakini kadiri muda ulivyoenda tulizoea hali hiyo na kuamua kuunga mkono kipaji chake cha uandishi wa mashairi ambacho alikionyesha tangu hatua za awali ya masomo yake," alisema Dk. Mtemi.

Dk. Mtemi ambaye ni baba mzazi wa Aisha, alieleza kuwa baada ya kumwacha Aisha ajikite katika fani aipendayo alifanikiwa baada ya muda mfupi.

"Kwa kipindi kifupi binti huyu amepata mafanikio makubwa ikiwamo kuwaandikia mashairi viongozi wa ndani ya nchi akiwamo Rais mstaafu, Jakaya Kikwete. Lakini pia safari yake ya mashairi imemkutanisha na Rais Putin wa Urusi, Malikia Elizabeth wa Uingereza pamoja na watu maarufu mbalimbali duniani," alisema.

Dk. Mtemi alishauri wazazi na walezi wajitahidi kugundua na kuendeleza talanta za watoto na kusisitiza kuwa watoto wawe huru kufanya wanavyovipenda na kuepuka kuwalazimisha watoto kuingia katika fani wanazozipenda na wazazi au walezi.

Elham Mwema amepongeza waandaaji wa warsha ili wazazi waelewe umuhimu wa kugundua na kuendeleza talanta watoto wao.

"Warsha imekuwa nzuri na imetufanya vijana tuone nguvu za vipaji na kutambua njia za kuendeleza vipaji. Tumeona kwamba kipaji kikiendelezwa ni rahisi kufanikiwa kiuchumi na maana mafanikio yanatokana na kufanya kitu ambacho kwako unakifurahia," alisema. Mwema.




Balozi wa Uingereza nchini, Sarah Cooke, akijadiliana na wanahabari jijini Dar es Salaam jana, kuhusiana na uhuru wa vyombo vya habari. Waandishi wa habari 250 wa Tanzania walipata mafunzo kupitia serikali ya Uingereza. Wa pili kushoto ni Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnell. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Vodacom yazindua M-Pesa Songesha

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mtandao wa simu, Vodacom, imezindua huduma ya kwanza na ya kipekee ambayo inaruhusu wateja wa M-Pesa kukamilisha miamala wakati hawana fedha za kutosha katika akaunti zao za M-Pesa.

Uvumbuzi huu wa kibunifu uitwao M-Pesa Songesha ulizinduliwa jana katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Kwa kutumia huduma hii, wateja wa M-Pesa sasa wataweza kutumia huduma hii kwa urahisi zaidi wakiwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukamilisha miamala yao kama vile kulipia bili, kutuma pesa kwa ndugu, jamaa na marafiki au hata kununua bidhaa pasipo kuwa na fedha za kutosha katika akaunti zao.

Mkurugenzi wa M-Commerce, Epimack Mbeteni, alisema: "Dhamira yetu ya kuleta mifumo bunifu ya kifedha kwa kutumia simu za mkononi ilitupelekea kutazama kwa makini vikwazo vya mara kwa mara vinavyowazuia wateja wetu kukamilisha miamala yao kwa sababu ya upungufu wa fedha katika akaunti zao.

"Uchunguzi huo umepelekea kuja na ufumbuzi wa kibunifu wa wateja wetu kuweza kukamilisha miamala ya M-Pesa ambayo ingeshindikana kukamilika kwa sababu ya upungufu wa fedha."

Songesha ni moja kati ya huduma nyingi za M-Commerce zilizozinduliwa mwaka huu. Huduma hizi ambazo nyingi zinaendana na maisha ya kidijitali zimewezesha Vodacom kuendelea kuongoza katika huduma za simu na fedha nchini kupitia miamala ya simu, umiliki wa soko na wateja. Katika mwaka wa fedha uliomalizika Machi mwaka huu, M-Pesa iliongeza umiliki wa soko hadi kufikia asilimia 40 na kuingiza watumiaji zaidi ya milioni 9 katika mifumo rasmi ya kifedha ambao wanafanya miamala ya zaidi ya Sh. trilioni 4.1 kwa mwezi.

Watumiaji wa M-Pesa wanaweza kufikia Songesha kwa kupiga namba za huduma ya M-Pesa, *150*00#, kisha kuchagua huduma za kifedha na kujiunga na huduma hiyo ya M-Pesa Songesha. Mara tu baada ya mteja kujiunga na Songesha, atapata ujumbe wa kiwango ambacho anastahili na ataweza kutumia kiwango hicho kukamilisha miamala yake. Kiasi hicho kitarejeshwa pale ambapo mteja atapokea fedha katika akaunti yake ya M-Pesa.

"kiwango hicho kina riba ya asilimia 1 kwa siku 18 na wateja wetu wanaweza kufanya miamala kwa kutumia huduma hii kadri watakavyo ikiwa ni ndani ya kikomo cha kiwango chao. Tumeungana na benki ya TPB kuwezesha huduma hii na ili kuamua kiwango mteja anachostahili, benki itatumia taratibu zilizowekwa kulingana na miamala ya mteja husika katika matumizi yake ya M-Pesa," alisema Epimack.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPB, Moses Manyatta, alisema: "Lengo letu kama benki ni kuhamasisha huduma jumuishi za kifedha huku tukiwahamasisha Watanzania kujenga tabia ya kujiwekea akiba na kujipatia mikopo kwa urahisi, Songesha ni kila kitu na inapatikana saa 24 kwa siku saba kupitia simu yako ya mkononi! Tunajivunia kuwa na uhusiano huu na tuna imani kwamba mapinduzi haya yatasaidia katika huduma jumuishi za kifedha," alisema.

## Chadema kupinga uchaguzi mdogo jimbo la Lissu

INATOKA UK.3

Ijumaa iliyopita, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, alitangaza kufanyika uchaguzi katika jimbo hilo na alitaja sababu za Lissu kuvuliwa ubunge ni kushindwa kuwasilisha tamko la mali na madeni na kutohudhuria mikutano saba mfululizo bila ruhusa ya Spika.

"Tumezingatia matakwa ya kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi sura ya 343, kutoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Singida Mashariki," alisema Jaji Kaijage.

Jaji Kaijage alisema, fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa kati ya Julai 13 hadi 18 mwaka huu na uteuzi wa wagombea utafanyika Julai 18.

Alisema ratiba za kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia Julai 19 hadi 30 na siku ya uchaguzi itakuwa ni Julai 31, mwaka huu.

Juni 28, mwaka huu, Spika Ndugai katika hotuba yake ya kufunga kikao cha bajeti cha bunge mjini Dodoma, alitangaza kumvua ubunge Lissu wakati akiwa ameshawasilisha taarifa hiyo kwa NEC kwa ajili ya kuitisha uchaguzi mdogo wa jimbo hilo.

Ndugai alisema kanuni za bunge na katiba ya nchi zinataka mbunge huyo avuliwe ubunge kwa kutotimiza masharti ya kuendeleza ushiriki wake katika shughuli za bunge.

Lissu ambaye alikuwa mnadhimu wa kambi ya upinzani bungeni kuanzia 2015 alikwenda nje ya nchi tangu aliposhambuliwa kwa risasi na watu wasiyojulikana akiwa nyumbani kwake, Dodoma Septemba, 2017.

Baada ya kunusurika katika shambulizi hilo Lissu alisafirishwa hadi Nairobi, Kenya kwa matitabu ya dharura na baadaye nchini Ubelgiji ambako amekuwa akipata matibabu kwa miezi kadhaa sasa.

Mwanzoni mwa mwaka huu, Tundu Lissu akiwa ameanza kupata nafuu kubwa, alitembelea nchi kadhaa ikiwa ni pamoja na Uingereza, Marekani na kuilaumu serikali kwa kushindwa kupata ufumbuzi kuhusu shambulizi dhidi yake.

Mwanasisasa huyo pia alitangaza mwezi uliopita kuwa anapanga kurejea nchini Septemba, mwaka huu, ikiwa ni miaka miwili tangu kunusurika kifo katika shambulizi la kutaka kumuua.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**PROJECTS GENERATE INCOMES AND CREATE EMPLOYMENT**
*Learn DESIGNING projects *Find DONORS *Establish NGO 0784505108 /0769505108

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

### KUPOTEA KWA CHETI



**Charles Humphrey Zakaria Kimaro** anatangaza kupotea kwa cheti cha Kumaliza chuo elimu ya Shahada kilichokuwa na namba **5446/T.87** kilichotolewa na Chuo kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1991.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**KMR/RB/7049/2019**

115317502

### CHETI KIMEPOTEA



**THERESIA LALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Ualimu chenye index namba **E 513/0196** kilichotolewa na MANDAKA CHUO CHA UALIMU mwaka 2002. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/RB/113984/2019.**

115318402

### KUPOTEA KWA KADI

**Samwel Kaleb Kaaya** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T 293 ABZ** aina ya **TOYOTA COROLLA.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/KJN/RB/120311/2019**

115317602

### KUPOTEA KWA KADI

**Genesis Roters Ltd** wanatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T 733 DLP aina ya TOYOTA LITEACE** yenye engine namba **5KEAA9838.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/116160**

115317302

### KUPOTEA KWA KADI

**Thadel Linus Changula** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T 342 CRB** aina ya **SUZUKI CURRY** yenye engine namba **F6A524458**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/2003/2019**

115317402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KAHAMA MJINI WILAYA YA KAHAMA**

**SHAURI LA MADAI YA NO. 103/2019**

**FRANK SOMI.....................MDAI**

**DHIDI YA**

**CLARENCE CLAVERY................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: CLARENCE CLAVERY – POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake hapa Mahakama ya Mwanzo Kahama mjini katika shauri tajwa hapo juu, ambalo litatajwa tarehe 23/7/2019. Unaamriwa kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 23/7/2019, saa 2:30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa ili kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima kuleta utetezi wenu na Hati zote zinazohusu shauri hilo ili kujitetea katika shauri hilo. Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, shauri hilo laweza kuamriwa kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu upande mmoja bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi Julai, 2019.

H.A.Mtawala
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
KAHAMA

115318202

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZINA SAID NASSOR**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T. 624 ANW** aina ya **TOYOTA RAVA4** yenye Chassis namba **SXA110001213,** engine namba**351883222.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi. **NGR/TR/RB/05/2019.**

115318002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHRISTINE ROSE MAVULLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 760 CHR** yenye chasis namba **RZJ950011304** na injini namba **3RZ1631649.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IR/TR/RB/2059/2019.**

115317902

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KISHAN ENTERPRISES L.T.D**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba **T. 213 TYW** aina ya SANYA yenye Chassis namba **LK1PCKL1XB1137870** yenye engine namba **162FMS410705400** yenye rangi NYEKUNDU. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/TR/RB/549/2019.**

115318102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;142/2019**

**Ombi la JULIAS SONGO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANNA JULIAS SONGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/07/2019.

115318302

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# WEST HAM YAMWANIA BALOTELLI

**LONDON,** England

KLABU ya West Ham imempa ofa ya kumsajili Mario Balotelli kwa usajili huru, kwa mujibu wa Daily Mirror.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ni mchezaji huru kwa sasa baada ya mkataba wake kumalizika katika Klabu ya Marseille ya Ufaransa mwishoni mwa msimu uliopita.

Wagonga nyundo hao wa London wameamua kumgeukia Balotelli baada ya mpango wa kumsajili Maxi Gomez kwa ada ya rekodi klabuni ya pauni milioni 45 kushindikana.

Bournemouth pia wamewazidi kete West Ham kwa kukaribia kumsajili, Callum Wilson kwa mkataba wa miaka minne wiki hii.

Kocha, Manuel Pellegrini alikuwa anatarajia kumsajili Gomez ambaye sasa ametua Valencia ambapo alikuwa na nia ya kuwa mrithi wa Marko Arnautovic ambaye amehamia Shanghai SIPG kwa pauni milioni 22.5.

West Ham walikuwa tayari kulipa ada ya kumwachia Gomez, lakini sasa wamezidiwa kete na hivyo kuangalia upande mwingine.

Na sasa West Ham wanaona kwamba, Balotelli anaweza kuziba pengo hilo kwani watamchukua kama mchezaji huru.

## Inter Milan wamfuata Lukaku England

**MANCHESTER,** England

MAOFISA wa Klabu ya Inter Milan wanatarajia kuwasili nchini England wiki hii kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Manchester United juu ya usajili wa Romelu Lukaku, kwa mujibu wa Sky Sports.

Presha ya usajili wa mchezaji huyo kwa Inter sasa imekuwa kubwa baada ya wapinzani wao kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus nao kuonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji huyo.

Inaeleweka kwamba, United wanataka kiasi cha pauni milioni 75 kutoka kwa Inter kama wanataka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

Lukaku yupo na United kwenye mandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England nchini Australia.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022, lakini inaeleweka wazi kwamba anataka kuondoka hapo Old Trafford.

Huku Lukaku akiwa akihusishwa na uhamisho huo wa kwenda Inter Milan, klabu hiyo imeamua kuchukua jukumu la haraka kuharakisha mazungumzo yao kabla dili hilo halijapokonywa.

Kwa mujibu wa Sky Sports Lukaku anaweza kusajiliwa Inter Mila ndani ya siku chache zijazo.






## *Sturridge aibiwa mbwa Marekani*

**LOS ANGELES,** Marekani

MCHEZAJI wa zamani wa Liverpool, Daniel Sturridge ametoa ofa ya zawadi kwa yeyote atakayeweza kumpata mbwa wake, Lucci baada ya kuibiwa nyumbani kwake jijini Los Angeles Jumatatu wiki hii.

Kwa mujibu gazeti la Daily Mail, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ambaye kwa sasa hana klabu baada ya kumaliza mkataba wake na Liverpool, hakuwapo nyumbani kwake wakati mbwa huyo akiibiwa.

Taarifa zinasema kwamba, nyumba yake hiyo ilivunjwa madirisha na 'watu wasiojulikana' na wakamuiba mbwa pamoja na mabegi kadhaa.

"Kuna watu walivunja nyumba yangu ya Los Angeles na kumuiba mbwa wangu," alisema Sturridge katika video yake akitangza ofa kwa atakayempata.

"Sikilizeni, yeyote ambaye atampata mbwa wangu, nitamlipa chochote, kwa uhakika kabisa.

Mshambuliaji huyo ametangaza ofa ya pauni 20,000 hadi pauni 30,000 kwa yoyote atakawezesha upatikanaji wa mbwa huyo.

"Inakuwaje mtu anakuja kuvunja nyumba yangu na kuiba mbwa wangu. Ni chizi au ana akili timamu kweli? Anamua kuiba mbwa wangu, naomba kwa yeyote atakayempata nitampa zawadi.

Sturridge ambaye alicheza kwa mafanikio makubwa pale Liverpool msimu uliopita alimaliza mkataba wake na sasa yupo kama mchezaji huyu na bado haijafahamika ni timu gani ataichezea msimu ujao.

## HABARI MICHEZO

# Baba wa Neymar akasirishwa na PSG

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

NEYMAR ataripoti kwenye mazoezi ya klabu ya Paris Saint-Germain Jumatatu ijayo, na taarifa hiyo klabu ilipewa wiki chache zilizopita, kwa mujibu wa wakala na baba mazazi wa nyota huyo.

PSG juzi ilitangaza kwamba itamchukulia hatua kali za kisheria mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil baada ya kushindwa kuhudhuria kwenye mazoezi ya kwanza ya klabu hiyo Jumatatu iliyopita.

"Tulikuwa kwenye matangazo ya biashara na majukumu ya taasisi ya Neymar Ijumaa na Jumamosi," alisema Neymar Sr. aliiambia Fox Sports ya Brazil.

"Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, taasisi ya Neymar imekuwa na kazi maalumu kila inapofika tarehe kama hizi.

"PSG, pamoja na rais wake, Nasser Al-Khelaifi walikuwapo kwenye tukio hilo. Sielewi sababu ya kusema kwamba, Neymar amekacha mazoezi. Tumekasirishwa na hili na PSG walikuwa wanajua ratiba yake."

Taasisi ya Neymar isiyo na faida husaidia maelfu ya watoto masikini pamoja na familia zao," kwa mujibu wa NR Sports, na taasisi hiyo ndio yenye haki za picha za nyota huyo wa zamani wa Barcelona.

Mkurugenzi wa michezo wa PSG, Leonardo alisema kwamba tarehe hizo zote hazikukubaliwa na PSG na ameongeza kuwa Neymar atakabiliana na adhabu kama mwajiriwa mwingine yoyote ambaye hakutokea kazini bila taarifa.






# EDU APATA ULAJI ARSENAL

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imemteua kiungo wake wa zamani, Edu, kuwa Mkurugenzi mpya wa ufundi wa klabu hiyo.

Msimu uliopita Arsenal walikuwa wanatafuta Mkurugenzi wa Ufundi, tangu alipoondoka Sven Mislintat Februari mwaka huu na wameamua kumchukua mchezaji huyo wa zamani wa Brazil, ambaye aliichezea klabu hiyo kati ya mwaka 2001 hadi 2005.

"Arsenal mara zote imekuwa sehemu ya moyo wangu na ninafurahia kurudi kwenye klabu kubwa kama hii na kupewa majukumu mapya," alisema Edu.

"Tuna kikosi imara na wachezaji vijana wenye vipaji na pia tukiwa na mashabiki wenye upendo wa kweli.

"Kwa sasa naangalia mbele jinsi ya kujaribu kuleta tofauti kwenye nafasi yangu hii mpya."

Arsenal wamepanga kurejea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 2016 na wanatumaini Edu, ambaye alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu England na klabu hiyo, anaweza kuwasaidia kurudi kwenye mashindano hayo.

"Tuna furaha kwamba Edu amejiunga na timu yetu," Mkuu wa soka wa klabu hiyo, Raul Sanllehi alisema akiwaambia waandishi wa habari wakati wa utambulisho wake.

# *Ivory Coast, Algeria hapatoshi Afcon leo*

**CAIRO,** Misri

IVORY Coast leo Alhamisi inatupa karata yake kwenye robo fainali ya michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, kwa kuwavaa Algeria, huku 'wageni' kwenye michuano hiyo Madagascar wakicheza na Tunisia.

Mchezo wa Ivory Coast dhidi ya Algeria utachezwa kwenye Uwanja wa Suez kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Ivory Coast walitinga hatua hiyo baada ya kuwafunga Mali bao 1-0 kwenye hatua ya mtoano wa timu 16, huku Algeria ikiwafunga bila huruma, Guinea mabao 3-0. Madagascar ambayo imefuzu michuano hiyo kwa mara ya kwanza, huku ikiwashangaza wengi, ilifuzu hatua hiyo baada ya kuwafunga Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC) kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-2.

Huku wao Tunisia iliwafunga Ghana kupitia mikwaju ya penlati na kutinga robo fainali michuano hii. Mchezo wa Madagascar dhidi ya Tunisia utapigwa majira ya saa 4:00 usiku katika dimba la Al-Salam.


Robo fainali nyingine za mashindano hayo zitachezwa kesho kati ya Senegal dhidi ya Benin wakati Nigeria yenyewe itawakabili Afrika Kusini maarufu Bafana Bafana, ambayo ilitinga hatua hiyo kwa kumfunga mwenyeji Misri (Mafarao) bao 1-0.

Cameroon ambayo iliondolewa na Nigeria kwa kukubali kichapo cha mabao 3-2, ndio walikuwa mabingwa watetezi wa fainali hizo ambazo zitamalizika Julai 19 mwaka huu.



HABARI MICH

# DONDOO SOKA
## MAGAZETI Y AYA




# SOLSKJAER AAMUA KUMPASHA POGBA

●●● Amweleza United haina mpango wa kumuuza mchezaji mwenye mkataba...

**PERTH,** Australia

OLE Gunnar Solskjaer amemwambia, Paul Pogba kwamba, Manchester United haihitaji kuuza wachezaji baada ya kiungo huyo na wakala wake kusema hadharani kwamba anataka kuondoka pale Old Trafford kipindi hiki cha majira ya joto.

**Pogba amebainisha nia yake ya kwenda kutafuta changamoto mpya, huku wakala wake, Mino Raiola, akiwa anamtetea mteja wake na kusisitiza kwamba suluhisho litapatikana kabla ya kufungwa kwa pazia la usajili.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye anatakiwa na Real Madrid na Juventus, yupo nchini Australia pamoja na kikosi cha United kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England.

Akizungumza kabla ya mchezo wao wa kwanza wa maandalizi ya ligi, Solskjaer amesema klabu yake haina presha yoyote ya kumuuza mchezaji ambaye bado ana miaka mitatu kwenye mkataba wake, na bado wakiwa hawajapata ofa yoyote.

"Sisi ni Manchester United hatuhitaji kuuza wachezaji wetu," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Hatuna ofa yoyote kwa ajili ya wachezaji wetu. Paul kamwe hajajiweka nje ya timu, mara zote amejitahidi kadiri ya uwezo wake na siwezi kuzungumza lolote kuhusu hilo.

"Kuna wakala anazungumza wakati wote na nimesema kwamba hatuna ofa yoyote iliyopo mezani, hili ndio pekee ninaloweza kusema kwa sasa."

Kabla ya United kusafiri kuelekea Australia, klabu hiyo ilikuwa haina uhakika kama Mfaransa huyo atajiunga na kambi kutokana na kutojulikana alipo.

Hata hivyo, Pogba aliungana na wenzake kwenda kwenye kambi hiyo, licha ya kuendelea kusisitiza kwamba anataka kuondoka United kwa sababu anataka kujifunza changamoto mpya.

United haitashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kutokana na kumaliza nje ya "Top Four" katika Ligi Kuu England msimu uliomalizika.

## ZISIKUPITE

### LINDELOF ATAKIWA BARCA

BARCELONA inajiandaa kuweka nguvu kumwania beki wa Manchester United kutoka Sweden, Victor Lindelof (24), kufuatia beki wa kati wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt (19), kuchagua kujiunga na Juventus. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### PSG KUIKAMUA BARCELONA

PARIS St-Germain itahitaji kulipwa pauni milioni £200 na Barcelona kama watahitaji kumsajili mshambuliaji Mbrazil Neymar, kiasi ambacho mabingwa hao wa Ufaransa walilipa wakati wanamnunua nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa klabu hiyo ya Hispania. ***(Mirror)***

### ARTETA, VIEIRA SOKONI

KOCHA Msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta na Kocha wa Nice, Patrick Vieira wametajwa kuchukua mikoba ya Rafael Benitez ambaye ameondoka Newcastle United. ***(Sun)***

### MADRID KUVUNJA REKODI

REAL Madrid inatarajia kuweka rekodi ya kulika kiasi cha pauni milioni 162 kwa ajili ya kumnasa kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba ili kumwondoa katika kikosi cha Manchester United. ***(Marca)***

### ERIKSEN KUMRITHI POGBA

KIUNGO wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen, anatajwa kuwa ndiye mchezaji atakayeziba pengo litakaloachwa na Pogba kama mchakato wake wa kuihama klabu hiyo utakamilika. ***(Evening Standard)***

### LUKAKU ATAKIWA UTD

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anamtaka straika wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, ambaye ana umri wa miaka 26, kusitisha uamuzi wake wa kuelekea Inter Milan na badala yake kubakia hapo Old Trafford katika msimu ujao. ***(Sun)***

### BAYERN YAMGANDA SANE

KLABU ya Bayern Munich bado inahitaji kumsajili winga, Leroy Sane kutoka Manchester City, licha ya dau la kumnunua Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 23 kutajwa kuwa ni pauni milioni 90. ***(Mirror)***

### DELPH AGOMBEWA

EVERTON imeingia kwenye vita ya kuwania saini ya kiungo wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Fabian Delph, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

### EVERTON YAMWANIA KEAN

KLABU ya Everton imetajwa kuonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Italia mwenye umri wa miaka 19, Moise Kean, ambaye Juventus inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 31 ili kumuuza, lakini kukiwa na kipengele cha kumrejesha klabuni kwake kwenye mkataba huyo mpya. ***(Mail)***

### DIAZ AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL imepewa ofa ya kumsajili straika wa Real Madrid ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidominiki, Mariano Diaz (25), kwa dau la pauni milioni 18. ***(Star)***

## HABARI MICHEZO

## Tanzanite kuchuana Cosafa bondeni

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite) imepata mwaliko wa kwenda kushiriki katika mashindano ya COSAFA ambayo yatafanyika kuanzia Agosti Mosi hadi 11 mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Mashindano hayo yanazihusisha timu za Jumuiya ya Ukanda wa Afrika Kusini ambazo ni Zimbabwe, Eswatini (zamani Swaziland), Botswana, Namibia na wenyeji Afrika Kusini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kuwa shirikisho limekubali mwaliko huo na linaamini kikosi chake kitakachokwenda kushiriki kwenye mashindano hayo kitafanya vizuri.

Ndimbo alisema kuwa tayari kikosi cha Tanzanite ambacho kiko chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime, kimeshaingia kambini kwa ajili ya kujiweka sawa kuelekea michuano hiyo.

Wakati huo huo, TFF imeingia mkataba na Shule ya Fountain Gate wa kudhamini soka la vijana wa umri chini ya miaka 15.

## Mjini Magharibi walalamikia vijeba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa Timu ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Ramadhani Madundo, amesema kufanya vibaya timu yake katika mashindano ya U-17 yanayoendelea nchini kumetokana na kupoteza wachezaji wake mahiri.

Madundo aliliambia gazeti hili kuwa, tatizo kubwa lililowakabili lilikuwa ni la kuzidi umri wa wachezaji baadhi ambao walilazimika kuondolewa.

"Makocha wa timu za vijana sio wa kweli katika kuwasajili wachezaji kulingana na madaraja yao, jambo hili linapelekea hata ikichaguliwa timu kuwakilisha mkoa wanapatikana vijana ambao wengi wao, wanakuwa na umri mkubwa," alisema Madundo.

Alisema hali hiyo ilisababisha kikosi chake kupoteza wachezaji 15, ambao walikuwa wazuri na alikuwa akiwategemea, lakini waliachwa kutokana na kutokidhi sifa za kushiriki mashindano hayo na hivyo kuondolewa katika hatua ya makundi.

"Tatizo la umri linazigharimu timu nyingi za vijana, sio tu kwetu hata kwa wenzetu, mie niwaombe tu makocha wa timu za vijana kutoka katika madaraja ya chini kuhakikisha wanazingatia kanuni, wasisajili wachezaji ambao umri wao si sahihi, itatugharimu huko mbele," Madundo alisema.

Hata hivyo Madundo alimpongeza Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Kombo Pandu, kwa mkakati wake wa kuhakikisha anasimamia suala la umri katika michuano ya vijana jambo ambalo litasaidia mwakani kuanza maandalizi mapema.

# SERIKALI YAKUMBUSHWA KUWEKEZA KWA WATOTO

**Na Mary Geofrey**

ILI kuwa na kikosi imara cha Taifa (Taifa Stars), serikali imetakiwa kuwekeza vema katika timu za watoto wa mitaani ambako kuna wachezaji wenye vipaji, lakini wanashindwa kufikia malengo ya kuwa wachezaji wakubwa kwa sababu ya changamoto mbalimbali zinazowakabili, imeelezwa.

**Ushauri huo, ulitolewa jana na Kocha wa Timu za Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, Ally Difuti, katika bonanza la mpira wa miguu lililohusisha watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi jijini Dar es Salaam pamoja na timu ya After School ya Kituo cha JMK Park.**

"Tunachoimba serikali iangalie hizi timu za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wana vipaji vikubwa, wana ndoto za kuwa wachezaji wakubwa lakini wanashindwa kufikia malengo yao kwa sababu ya changamoto zinazowakabili," alisema Difuti.

Alitolea mfano mshambuliaji wa timu ya Juventus ya Italia, Cristiano Ronaldo, ambaye naye alikuwa mtoto wa mtaani lakini ameweza kuwa mchezaji mkubwa na anayetambulika duniani kwa sababu alipata msaada katika kutimiza ndoto zake.

"Ninachoweza kusema hizi timu za watoto wa mitaani ziangaliwe kwa karibu na serikali, Waziri wa Habari, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, atambue tu kuwa kuna vipaji vikubwa kutoka kwa hawa watoto, waviendeleze. Sisi tumefanya kazi ya kuviibua, kama serikali ikitusaidia tulipofika itakuwa vyema kuviendeleza," alisema mwalimu huyo wa michezo kutoka kituo cha watoto wa wanaoishi katika mazingira magumu cha Dogodogo.

Naye mshiriki wa bonanza hilo, John Alfred (15), anayefanya biashara ya kuchambua samaki katika soko la Feri, alisema ana ndoto ya kuwa mchezaji wa Taifa Stars, hivyo anaiomba serikali kuwawezesha kufikia malengo yao kwa kuwapatia vifaa vya michezo.

"Nina ndoto za kuwa mchezaji wa timu ya Taifa, nina imani nitafikia malengo yangu kwa sababu ninajituma katika kucheza mpira na kufanya mazoezi. Naomba serikali ituwezeshe vifaa vya mazoezi na zaidi kutufanya tufikie ndoto zetu kwa sababu ndoto za kusoma zilishapotea," alisema John.

Aliongeza kuwa anacheza vema namba 9 katika timu ya watoto wa Feri na anatamani kuwa kama nahodha na mshambuliaji wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, John Bocco.




Wafanyakazi wa Kampuni ya Simu ya mikononi ya Vodacom Tanzania, Kanda ya Kati wakiwa tayari kuanza mbio za Capital City Marathon zilizofanyika jijini Dodoma wiki iliyopita. Kampuni hiyo ilidhamini wanafunzi 51 kutoka vyuo vikuu vilivyoko jijini humo pamoja na wafanyakazi wake 35 ili kuhamasisha kufanya mazoezi kwa lengo la kuboresha afya zao. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Lipuli wajipanga kusajili 9 wapya*

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Lipuli FC ya Iringa umesema kuwa unatarajia kusajili wachezaji wapya tisa kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi kuu Tanzania Bara ambao utachezwa kuanzia Agosti 23 mwaka huu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu Mkuu wa Lipuli FC, Julius Leo, alisema kuwa mpaka sasa wanaendelea na mazungumzo na wachezaji mbalimbali, ambao wanataka kuwasajili kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi.

Kiongozi huyo alisema kuwa wanaamini wakiwapata nyota hao wapya, pamoja na wachezaji wengine waliopo, kikosi chao kitakuwa imara na kitaendelea kutoa ushindani kama ilivyokuwa katika msimu uliopita.

"Tutaongeza wachezaji tisa kwenye timu yetu, lengo letu ni kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita, tunataka kila namba iwe na wachezaji wawili wenye uwezo, ili tusiwe na wasiwasi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilisha mchakato huo wa usajili, kikosi chao kitaingia kambini kuanza maandalizi ya msimu huo mpya.

"Nafikiri keshokutwa (kesho) kila kitu kitakuwa sawa, tunasubiri mwalimu wetu atupe ratiba nzima ya maandalizi ya msimu mpya," katibu huyo alisema.

Msimu uliopita Lipuli ilimaliza katika nafasi ya sita lakini ikifika fainali ya mashindano ya Kombe la FA, ambalo lilichukuliwa na Azam FC.

# Michezo

Alhamisi Julai 11, 2019

Nipashe




Solskjaer aamua kumpasha Pogba

UKURASA 30

# Yanga kushusha mashine mpya

## ●●● Ni beki wa kushoto wa Uganda Cranes, baada ya Metacha kumwaga...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI tayari imefanikiwa kupata saini ya golikipa wa Mbao FC ya jijini Mwanza na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Metacha Mnata, uongozi wa Yanga umetua Kampala ili kumwania beki wa kushoto wa KCCA na Uganda (Cranes), Timothy Awanyi, imefahamika.

**Golikipa huyo anatarajiwa kuwa chaguo la kwanza la Yanga ambayo ilishindwa kumbakisha Beno Kakolanya aliyesajiliwa na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.**

Metacha alikuwa langoni wakati Taifa Stars inacheza mechi yake ya mwisho ya Kundi Cdhidi ya Algeria na kufungwa mabao 3-0, alikuwa akiichezea Mbao FC kwa mkopo, akitokea Azam FC.

Hata hivyo, kutokana na kuonyesha kiwango kizuri msimu uliopita, Azam ilitaka kumpa mkataba mpya, lakini mlinda mlango huyo hakukamilisha mazungumzo na mabingwa hao wa Kombe la FA, na badala yake ametua Jangwani akiwa ni mchezaji.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi mmoja wa Yanga, alisema kuwa Metacha, amesaini mkataba wa miaka mitatu na wanaamini ujio wake utasaidia kukiimarisha kikosi chao.

Kiongozi huyo alisema kuwa wachezaji wote wapya ambao wamesajiliwa Yanga ni wazuri na wataisaidia timu hiyo kufikia malengo yake.

"Tunapenda kuwaambia mashabiki wetu wa Yanga kuwa Metacha ni mali ya Yanga, amesaini mkataba wa miaka mitatu, tutaamini tutakuwa na mambo mazuri zaidi katika msimu ujao," alisema kiongozi huyo.

Chancho hicho kiliendelea kusema kuwa bado Kamati ya Usajili ya timu hiyo inaendelea na mipango ya kusaka saini ya beki wa kushoto wa Uganda Cranes, ambaye tayari walishaanza mazungumzo naye.

Metacha anakuwa mchezaji mpya wa 14 kusajiliwa na Yanga kwa ajili ya msimu ujao ambapo wengine ni Muharami Salum Issa 'Marcelo' kutoka Malindi, Zanzibar, Ally Mtoni 'Sonso' (Lipuli FC), Ally Ally (KMC FC), Abdulaziz Makame (Mafunzo), Mapinduzi Balama (Alliance FC) na Sadney Urikhob kutoka Namibia.

Nyota wengine ambao watavaa jezi ya Yanga ambayo itashiriki pia mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ni Lamine Moro wa Liberty Academy ya Ghana, Juma Balinya (Polisi-Uganda), Issa Bigirimana, Patrick Sibomana (APR- Rwanda), Mrundi Mustapha Seleman na Maybin Kalengo kutoka Zesco ya Zambia.

Wakati huo huo, wachezaji wa Yanga ambao walikuwa katika kikosi cha Taifa Stars, akiwamo Kelvin Yondani, Sonso na Feisal Salum, waliokuwa kwenye likizo fupi, wanatarajiwa kuripoti kambini mkoano Morogoro leo ili kuungana na nyota wenzao.

Yanga inatarajia kutambulisha kikosi chake kamili katika tamasha litakalofanyika Julai 27 mwaka huu na itafungua msimu mpya kwa kucheza dhidi ya Ruvu Shooting ya Mlandizi, Pwani.



Beki wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, akiwa katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Carton House kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu England. **PICHA: MTANDAO**

# Okwi: Heshima zote kwa Simba

**Na Somoe Ng'itu**

SITAISAHAU Simba! Hayo ni maneno ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uganda (Uganda Cranes), Emmanuel Okwi, ambaye anatarajia kukamilisha mchakato wa kujiunga na klabu ya Fujairah FC inayoshiriki Ligi Kuu Falme za Kiarabu (UAE).

Okwi anajiunga na Waarabu hao akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake wa kuitumikia Simba ambayo msimu uliopita, aliisadia kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mganda huyo ambaye alionyesha kiwango cha juu katika mechi zote nne za Cranes kwenye fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), amefikia uamuzi wa kuondoka Simba baada ya kuridhika na ofa ambayo ameipata kutoka kwa Fujairah.

Akizungumza na Nipashe jana, Okwi, alisema kuwa anaamini atarejea Tanzania, na atarudi kama mchezaji wa Simba kwa sababu klabu hiyo imemfanyia mambo mengi mazuri. Okwi, mshambuliaji wa zamani wa SC Villa ya Uganda na Yanga alisema kwamba ameishi vema na viongozi, wachezaji na mashabiki wa Simba, hivyo klabu hiyo itaendelea kubakia kwenye kumbukumbu zake nzuri wakati wote.

"Sitaweza kuisahau Simba, ni kama nyumbani, mimi ninaichukulia hivyo, ila maisha ya mpira hubadilika kulingana na wakati, ninahitaji kutumia kila fursa ninayopata, ninawashukuru na nitaendelea kuwashukuru," alisema mshambuliaji huyo.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema kuwa mazungumzo kati ya Okwi na klabu hiyo ya Uarabuni yako katika hatua za mwisho.

"Mpaka muda huu naweza kukwambia kuwa mazungumzo kati ya Okwi na Fujairah yamefikia zaidi ya asilimia 80, nafikiri hatarudi Simba. Inaonekana msimu huu alitaka kuondoka na kujaribu maisha sehemu nyingine, Afcon alifanya kazi kubwa, " kilisema chanzo chetu.

Okwi ambaye pia aliwahi kucheza soka la kulipwa Tunisia na Denmark, amekuwa makini zaidi katika suala la usajili na alikataa kusaini mkataba mapema na Simba, akifahamu wazi, thamani yake itaongezea baada ya Afcon.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002